

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Tatu – Tarehe 7 Septemba, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Tukae. Katibu.

NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
(MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (*NEMC*) kwa mwaka wa fedha ulioisha tarehe 30 Juni, 2016 (*The Annual Report and Audited Accounts of National Environment Management Council (NEMC) for the year ended 30th June, 2016*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Malawi (*Convention on the Establishment of a Joint Songwe River Basin Commission Between the*

Government of the United Republic of Tanzania and the Government of the Republic of Malawi).

MHE. SALUM MWINYI REHANI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):

Maoni ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji juu ya Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe Kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Malawi (*Convention on the Establishment of a Joint Songwe River Basin Commission Between the Government of the United Republic of Tanzania and the Government of the Republic of Malawi*).

MHE. HAMIDU H. BOBALI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mta Songwe Kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Malawi (*Convention on the Establishment of a Joint Songwe River Basin Commission Between the Government of the United Republic of Tanzania and the Government of the Republic of Malawi*).

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):

Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Community Protocol on Peace and Security*).

MHE. ROSE C. TWEVE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):

Maoni ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama juu ya Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Community Protocol on Peace and Security*).

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM - NAIBU MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Maoni ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Community Protocol on Peace and Security*)

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali na tunaanza na Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 30

Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Sumbawanga na Nkasi

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA aliuliza:-

Halmashauri za Wilaya ya Nkasi na Sumbawanga Mjini hazina Hospitali ya Wilaya; wanawake na watoto wanapata shida ya matibabu wakati wa kujifungua na huduma za watoto.

Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali katika Wilaya hizo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Selemani Jafo, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa umeanza taratibu za ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa katika eneo la Milanzi. Hospitali ya Mkoa inayotumika sasa itabaki kuwa Hospitali ya Manispaa ya Sumbawanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa wananchi wa Manispaa ya Sumbawanga wanapata huduma za afya katika Hospitali Teule ya Dkt. Atman inayomilikiwa na Kanisa ambayo imeingia mkataba na Serikali wa utoaji huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari zaidi ya 100 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Taratibu za kulipa fidia wananchi waliopisha ujenzi huo zinakamilishwa. Kwa sasa wagonjwa wanapata huduma katika Hospitali Teule iliyopo pamoja na vituo vya afya na zahanati. Serikali itajitahidi kutafuta fedha na kushirikiana na wananchi wa Nkasi ili kufanikisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, swali la nyongeza.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini maswali mawili ya nyongeza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa Sera ya Afya inasema itajenga zahanati kila kijiji na pia itajenga vituo vya afya kila kata na pia itajenga Hospitali za Wilaya kila wilaya. Je, ni lini sera hii itatekelezwa kikamilifuto?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa afya ni kipaumbele cha mwanadamu hasa kwa mama na mtoto, je, Serikali haioni umuhimu wa kuupa kipaumbele Mkao wa Rukwa kwa kuwa hauna Hospitali ya Wilaya hata moja? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli sera yetu inatueleza hivyo na ndiyo maana ukiangalia mchakato wa Serikali kwa kushirikiana na ninyi Waheshimiwa Wabunge, wananchi na wadau mbalimbali mnaona ni jinsi gani tunajitahidi kwa kadri iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naomba nitoe pongezi zangu za dhati, katika maeneo mbalimbali nilikopita nimekuta Wabunge wengi sana na wengine wakitumia Mfuko wa Jimbo na kuungana nguvu na wananchi katika suala zima la ujenzi wa zahanati na vituo vya afya. Nilishawahi kuzungumza hapa siku za nyuma kwamba katika bajeti ya mwaka 2017/2018 tumetenga shilingi bilioni 251 lakini katika hizo shilingi bilioni 68 ni kwa ajili ya ku-*top up* shughuli hizo za ujenzi wa zahanati huko tunakokwenda kumalizia haya maboma.

Kwa hiyo, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunafanya kila liwezekanalо sera hii iweze kutekelezwa. Najua kila jambo lina *time frame*, katika miaka hii mitano mtaona mabadiliko makubwa sana katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mahsusni katika Mkao wa Rukwa, ni kweli kuna changamoto kubwa sana ndiyo maana Serikali tukaona katika Halmashauri zake kutokana

na changamoto lazima tuboreshe kwanza vituo vya afya vilivyopo. Leo hii kwa kaka yangu Mheshimiwa Ally Keissy kule Nkasi amepigia kelele sana Kituo chake cha Kirando, tumefanya utaratibu tunaenda kujenga *theatrena* majengo mengine. Ukienda pale *Sumbawanga DC* halikadhalika kuna suala la ujenzi wa Kituo cha Afya cha Mirepa lakini hilo tutafanya kwa kadri iwezekanavyo na ndiyo maana katika Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo hivi sasa tumepeleka karibia shilingi milioni 340 kwa ajili ya zoezi la ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

Kwa hiyo, ni jukumu la Serikali kuhakikisha Mkoa wa Rukwa nao uweze kujengewa miundombinu ili wananchi wa kule waweze kupata huduma nzuri za afya.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Badwel, swali la nyongeza.

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya ya Bahi nayo ni mionganoni mwa Wilaya hizo kadhaa ambazo hazina Hospitali ya Wilaya na kumekuwa na matatizo mengi sana, lakini pale Bahi tuna kituo cha afya ambacho hakijafikia *level* ya upasuaji.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuwaambia wananchi wa Bahi kwamba labda upo mpango wowote mzuri wa kusaidia kile Kituo cha Afya Bahi ili angalau hatua ya upasuaji hasa akina mama na huduma zingine muhimu ziwepo? Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nimefika mara mbili kwenye Halmashauri ya Bahi na juzi juzi tulikuwa na Mheshimiwa Mbunge jimboni kwake takribani mwezi

mmoja na nusu na bahati mbaya Bahi hawana Hospitali ya Wilaya wala vituo vya vya afya na kile kimoja kiko katika hali mbaya. Kutokana na maombi ya Mbunge tayari tumeshapeleka shilingi milioni 500 ndani ya wiki hii. Tunaenda kukiimarisha Kituo cha Afya cha Bahi, tunakijengea miundombinu ya upasuaji na maabara. Nia yetu ni kwamba Bahi pale huduma zote za msingi ziweze kupatikana kwa ukaribu zaidi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, ombi lako limekubaliwa na Serikali na tunalifanyia kazi. Lengo letu ni kwamba wananchi wa Bahi wapate huduma nzuri kama wananchi wengine.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa ni zaidi ya miaka 53 toka nchi imepata uhuru sehemu yenyehadhi ya mkoa kama Mkoa wa Rukwa hatuna Hospitali ya Wilaya hata moja. Serikali haionti umuhimu sasa wa kuondoa aibu hiyo angalau hata wilaya mbili zipate hospitali ya wilaya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu, Wabunge wote wa Rukwa wakisimama hapa ajenda kubwa ni afya kwa sababu ni kweli siyo jambo la uongo. Ndiyo maana hata nilivyokuwa nikimjibu Mheshimiwa Bupe swali lake lile la msingi la kwanza nilizungumza kwa ujumla wake. Ndiyo maana tumesema mipango ya Serikali katika Halmashauri ya Kalambo sasa hivi kati ya shilingi bilioni 1.4 tulioitenga tumepeleka karibu shilingi milioni 340 lakini hili tutalisimamia vizuri katika mwaka huu wa fedha angalau Kalambo ujenzi uende kukamilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika ukiangalia pale *Sumbawanga DC* hali ni mbaya vilevile, lakini hivi sasa katika Kituo cha Afya cha Mwimbe tumepeleka fedha

karibuni shilingi milioni 500 lakini kule Nkasi tumeshaanza kushughulikia matatizo yake. Jukumu hili lote ni la Serikali. Naomba muwe na imani kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano, *commitment* yake ile mikoa ambayo ina changamoto kubwa sana tutafanya kila liwezekanaloo kuhakikisha wananchi wa mikoa hiyo wanapatiwa huduma.

Kwa hiyo, Mheshimiwa dada yangu naomba nikusihii kwamba Serikali hii iko nanyi Wabunge wa Rukwa wala msiwe na hofu, tutajitahidi kufanya kila liwezekanaloo kuhakikisha huduma ya afya inapatikana vizuri zaidi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima Bulembo, swali la nyongeza.

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *RCC* ya Mkoa wa Kagera ilishatoa kibali kuhusu ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Karagwe, lakini suala hilo linakwamishwa na Wizara ya TAMISEMI kwa sababu haitaki kutoa usajili ili hospitali hiyo itengewe bajeti na ujenzi uanze mara moja. Je, ni lini Wizara ya TAMISEMI itaamua kutoa usajili huo ili ujenzi uanze mara moja ili kuokoa akina mama na watoto?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la dada yangu Mheshimiwa Halima Bulembo na kwanza nimpe hongera sana kwa kazi kubwa aliyofanya katika sekta hii ya afya, hongera sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, bahati nzuri nimefika Karagwe, bahati nzuri pia anafahamu hata pale Karagwe kulikuwa hakuna *DMO*. Sisi TAMISEMI ndiyo tukamchukua kijana mmoja anaitwa Sobo tukampeleka pale, ni daktari mzuri sana wa upasuaji. Hata Karagwe pale tulikuwa hatuna *centre* ya Serikali ya kufanya upasuaji sasa hivi upasuaji pale Karagwe katika kituo cha afya umeanza.

Si hivyo tu, lilivyotokea tetemeko la ardhi, Serikali imefanya juhudii kubwa sana kuboresha kile kituo cha afya na hivi sasa tunapeleka takribani shilingi milioni 500 kufanya wananchi wa Karagwe wanapata huduma nzuri ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwahakikishie kwamba katika ofisi yetu hakuna kibali kitakachokwama isipokuwa wakati mwagine ni changamoto ya bajeti. Tunachukua mawazo yote ya Wabunge wa Karagwe, tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo kutekeleza vipaumbele vyenu mlivyoweka katika mpango wa bajeti maana siyo suala la kibali, kibali sisi hamna tatizo isipokuwa ni pamoja na kuona ni jinsi gani tutenge bajeti kuhakikisha tunajenga hospitali ya wilaya.

Kwa hiyo, ni jukumu la Serikali, tutafanya kila liwezekanalo wananchi wa Karagwe kama tunavyofanya sasa tutaendelea kufanya hivyo ili mradi huduma ya afya ipatikane vizuri katika Wilaya ya Karagwe na Halmashauri yake kwa ujumla. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Swali la mwisho, Mheshimiwa Kakoso.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Tanganyika ni mionganini mwa wilaya mpya ambazo hazina huduma ya hospitali ya wilaya. Kwa nyakati tofauti, Serikali imekuwa ikiahidi Kituo cha Afya kijiji cha Majalila ambako ni Makao Makuu ya Wilaya. Nilikuwa nataka kujua kauli ya Serikali, je, Kituo kile cha Majalila, ni lini kitaanza kupewa fedha na hatimaye kuanzisha ujenzi wa kituo cha afya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Wilaya ya Tanganyika imegawanyika kutoka Mpanda na mimi

Mbunge nafahamu tulifika pale kwake ni kweli kuna tatizo kubwa sana. Kwa mfano wananchi wanaotoka Mwese wakija Mpanda Mjini ni tatizo na tulifika pale Majalila ambapo Makao Makuu ya Wilaya ile inataka ijengwe, nikuuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi sasa tumetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya Halmashauri yako ya Wilaya. Juzi nilikuwa naongea na Mkurugenzi wako wa *Mpanda DC* kuangalia jinsi gani tutafanya.

Kwa hiyo, kuna shilingi milioni 500 tunawaleta na hii sisi tunasema kama ni *kingiambago* tu, ni fedha ya kwanza tutatoa fedha nyingine kwa ajili ya kununua vifaa ambayo jumla yake itakuwa karibuni shilingi milioni 720. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie wananchi wa Tanganyika hili ni jukumu la Serikali kuwafikia watu wote hata ndugu yangu wa Kakonko tulifanya jambo hili kwa sababu siku ile tuliyofika shida ilikuwa kubwa. Hii ni kazi ya Serikali na itafanya kazi kila mahali kwa manufaa ya wananchi wake wa Tanzania.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea, Mheshimiwa James Francis Mbatia, Mbunge wa Vunjo, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Selasini.

Na. 31

Ujenzi wa Barabara Inayoanzia Uchira - Kolaria

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. JAMES F. MBATIA) aliuliza:-

LEKIDIA imeweza kushirikiana na wananchi wa Kata ya Kirua Vunjo Mashariki na kufanikiwa kukarabati barabara za kata hiyo zenye urefu wa kilometra 17 kwa gharama ya shilingi milioni nane, lengo kuu ni ujenzi wa barabara inayoanzia Uchira hadi Kolaria yenyе urefu wa takribani kilometra 12 kwa kiwango cha lami; na LEKIDIA wamefanikiwa kufanya harambee na kupata shilingi milioni 130 ambapo shilingi milioni 60 zimetumika kununua mapipa 300 ya lami na kubakiwa na shilingi milioni 70.

Je, Serikali itashirikianaje na LEKIDIA kutekeleza mradi huo kwa ajili ya maendeleo endelevu ya wananchi wa Kata ya Kirua Vunjo Mashariki?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Francis Mbatia, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Uchira - Kisomachi - Kolaria yenye urefu wa kilometra 12 ilijengwa kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya shilingi milioni 300 kutoka katika Mfuko wa Barabara katika mwaka wa fedha 2013/2014. Barabara hiyo imeendelea kufanyiwa matengenezo ambapo katika mwaka wa fedha 2016/2017 zilitumika shilingi milioni 74.2 ili kuifanya ipitike wakati wote. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imepanga kutumia shilingi milioni 31 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida kilometra nane na matengenezo ya sehemu korofii kilometra mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapongeza juhudii kubwa inayofanywa na LEKIDIA. Serikali kuititia Wakala wa Barabara Mijini na Vijiji (TARURA) itafanya tathmini ya barabara zote nchini pamoja na barabara ya Uchira hadi Kolaria ili kuona namna bora ya kuziboresha barabara hizo kwa kiwango kinachohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kushirikiana na wananchi na wadau wengine wa barabara ili kuhakikisha barabara hiyo inafanyiwa matengenezo kurahisisha usafiri na usafirishaji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Selasini, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, LEKIDIA imekuwa ikishirikiana na wananchi katika kuibua vipaumbele vyta maendeleo katika Kata ya Kirua Vunjo Mashariki kwa muda mrefu na kipaumbele cha sasa ni hii barabara ya Uchira - Kisomachi - Kolaria ambao wamejitahidi kuchanga fedha na sasa wana lami pipa 300. Kipaumbele chao ni kwamba hii barabara ijengwe kwa kiwango cha lami.

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kusaidia ili lami hii isije ikaharibika kujenga walau hatua kwa hatua kilometra tano na baadaye kilometra nyingine tano ili hatimaye hii barabara iweze kukamilika kwa kiwango lami badala ya kutumia fedha nyingi kwa ukarabati mara kwa mara?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, wananchi wamekuwa wakishiriki sana katika kuchangia maendeleo, wamekuwa wakichangia ujenzi wa zahanati, vituo vyta afya, shule na kadhalika. Katika Jimbo langu la Rombo karibu kila kijiji kuna miradi ya maendeleo inayoendelea kwa michango ya wananchi lakini kwa upande wa Serikali fedha zimekuwa haziendi kwa wakati jambo ambalo sasa linawavunja moyo wananchi.

Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusu upelekaji wa fedha za maendeleo jinsi ambavyo zimekubaliwa kwenye bajeti ili kuwatia moyo wananchi hao waendelee kuchangia shughuli za maendeleo ambazo tayari zimeshaanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli LEKIDIA wamechanga wamenunua mapipa takribani 340 kwa rekodi niliyokuwa nayo. Ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimesema kwa sababu sasa hivi tumeunda Wakala mpya wa TARURA na bahati nzuri tumepata Meneja maalum wa mradi katika Halmashauri ya Rombo na katika Halmashauri

zote Tanzania. Meneja hawa jukumu lao sasa ni kufanya *needs assessment* katika kila Halmashauri. Tuagize Meneja wetu apitie barabara hiyo *then* ataleta tathmini halafu tutajua nini cha kufanya katika barabara hiyo. Kwa hiyo, njukumu kubwa la Serikali kuhakikisha barabara hizi zote zinafanyiwa matengenezo. Kwa hiyo ni *commitment* yetu Serikali kwa Tanzania nzima, hili jambo tutaenda kulifanya nikitambua juhudii kubwa ya wananchi wanayoendelea kuifanya, lazima tuwaunge mkono. Kwa hiyo, kazi itafanyika baada ya tathmini ya Mameneja wetu walioko *síté* kuangalia kipi kilichopo na kipi kifanyike katika utaratibu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala zima la upelekaji wa fedha, nimesema hapa kwa mfano fedha za barabara tumetenga karibuni shilingi bilioni 263 lakini hizi kuna fedha za barabara zenyé vikwazo lakini zingine za *road fund* na maeneo mbalimbali. Ni jukumu la Serikali kuhakikisha tunapata fedha hizi na bahati nzuri jana tulikuwa na Waziri wa Fedha katika kikao chetu cha mambo ya lishe amesema *commitment* ya Serikali katika mwaka huu wa fedha ni kuhakikisha fedha zote za maendeleo zinafika katika maeneo husika. Kwa hiyo, ondoa hofu, jukumu letu sasa hivi naomba tuungane mkono wote kwa pamoja tukusanye mapato, tulipe kodi na mwisho wa siku kwamba fedha hizo zitapelekwa katika vijiji vyetu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma nzuri katika maeneo mbalimbali.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Mgimwa.

Na. 32

**Kupandisha na Kuongeza Morali ya
Kazi kwa Watumishi wa Umma**

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (K.n.y. MHE. COSATO
D. CHUMI) aliuliza:-**

Serikali ina utaratibu wa kuwalipa watumishi wa umma gharama za nauli ya likizo mara moja katika miaka miwili wakati wanaenda likizo.

Je, Serikali ipo tayari kuanzisha utaratibu wa kuwalipa gharama za nauli za likizo watumishi wa umma kila mwaka katika kuongeza, kupandisha morali ya kazi na pia kupunguza makali ya maisha?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, likizo ya mwaka ni haki ya kila mtumishi wa umma na haki hii imebainishwa katika kifungu cha 31 cha Sheria ya Kazi na Mahusiano Kazini Namba6 ya mwaka 2004 na Kanuni ya 97 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kulipa gharama za nauli kwa watumishi wa umma kwa ajili ya likizo umeainishwa katika Kanuni H. 5 (1) (a), (b) na (c) ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009. Kwa mujibu wa kanuni hiyo, mtumishi wa umma anatakiwa kulipiwa gharama ya nauli kwa ajili yake, mwenza wake na wategemezi wasiozidi wanne kutoka kituo chake cha kazi hadi nyumbani kwake mara moja katika kipindi cha miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali ni kuwapa motisha watumishi wa umma ili kuwaongezea morali ya kazi. Hata hivyo, motisha inayotolewa inapaswa kuzingatia hali ya uchumi wetu. Hali ya uchumi wetu kwa sasa inaruhusu

utaratibu huu wa kulipa gharama za nauli ya likizo kwa watumishi wa umma mara moja katika kipindi cha miaka miwili. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha motisha kwa watumishi wa umma kadri uchumi unavyoimarika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, swalil la nyongeza.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalil la kwanza, nataka tupate tamko la Serikali lini wataanza kulipa malimbikizo hayo ya likizo za wafanyakazi ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakisubiri haki zao hiso za msingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalil la pili, ni mwaka wa pili sasa hakuna *increment* yoyote kwa walimu wala kupandishwa madaraja. Nataka kauli ya Serikali ni lini wataanza kupandisha madaraja na kuongeza *increment* hasa za walimu ambao morali zao zimeanza kushuka katika maeneo yao ya kazi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipende tu kusema kwamba Serikali imekuwa ikijitahidi kulipa malimbikizo mbalimbali ya mishahara pamoja na madai mengine yasiyokuwa na mishahara kwa watumishi wa umma na itaendelea kufanya hivyo kila mara. Nipende tu kusema kwamba katika mwaka huu wa fedha kupitia bajeti za *OC* mbalimbali za waajiri wetu wametenga ulipaji wa madeni, lakini vilevile kupitia Serikali kwa ujumla wake tumetenga fedha zaidi ya shilingi triloni moja kwa ajili ya kulipa madeni ya watumishi pamoja na madeni ya wazabuni wengine mbalimbali waliotoa huduma katika

Serikali. Kwa hiyo, wakati wowote tu kuanzia sasa pindi tu madeni hayo yatakapokuwa yameshahakikiwa basi watumishi wataweza kuona madeni hayo yakilipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusiana na *increment* na kupanda madaraja, nilipokuwa nikijibu swali hapa Jumatatu au Jumanne nilieleza kuhusiana na suala hili. Tayari taratibu zimeanza na hivi sasa tunakamilisha tu taratibu za mwisho ili kuweza kuanza kulipa nyongeza hiyo ya mwaka ya mishahara kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa upandishwaji wa madaraja, nilishasema fedha zimeshatengwa na niwahahakishie tu watumishi wote wa umma wenye stahili za kupanda madaraja hakuna ambaye ataachwa. Niendelee tu kuomba waajiri wahakikishe kila ambaye anastahili kupanda daraja basi ameingizwa katika orodha, lakini bila kuacha kuzingatia *seniority list* ili watumishi wenye stahili waweze kupatiwa madaraja hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kurudia kusema tena tumeshatenga fedha kwa ajili ya watumishi 193,166 ambaao watapanda madaraja mwaka huu. Niendelee kuwatoa hofu watumishi wa umma hakuna ambaye atakakosa daraja lake analostahili katika mwaka huu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa hapa mbele sijalijua jina lako hebu jitambulisse, taja jina lako unapouliza swali la nyongeza.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naitwa Nuru Awadh Bafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa kuna baadhi ya walimu mfano katika Halmashauri ya Jiji la Arusha katika Shule ya Msingi Olkerian, Kata ya Olkerian mpaka leo wanasumbuliwa kulipwa fedha zao za likizo na wakati huo huo tayari walishatumia fedha

zao. Wanapouliza wanaambiwa andikeni barua ili muweze kulipwa pesa zenu. Je, Waziru anatuambiaje kuhusu suala hilo? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nimpongeze kwa kurudi tena Bungeni, alikuwa ni Mbunge kipindi cha mwaka 2005-2010, hongera sana na karibu tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua yako madeni mbalimbali ya watumishi wanaodai fedha zao za likizo. Nipende tu kusititza kwa waajiri kila mwaka pindi wanapoandaa mapendekezo ya bajeti za mwaka wahakikishe wanatenga fedha kwa ajili ya nauli za likizo katika bajeti ya matumizi ya kawaida au bajetiza *OC*. Vilevile nipende kusema kwamba kwa yejote ambaye hakulipwa fedha hizo hilo ni deni na kama Serikali tunalitambua na tunalichukua na tutaendelea kufuatilia kuhakikisha kwamba watumishi hawa wanapatiwa malipo yao. Niombe tu anisaidie huko baadaye taarifa kamili ili tuweze kushirikiana katika ufuatilaji, lakini ni haki ya msingi ya mtumishi na ni lazima walipwe.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bashungwa, swalii la nyongeza.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa mpango wa kupandisha watumishi madaraja wale wanaostahili lakini kuna changamoto ya wale watumishi ambao wanapandishwa madaraja mishahara huwa inachelewa *ku-reflect* lile daraja ambalo

amepandishwa. Je, ni nini maelezo ya Serikali kuhusu suala hili?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niseme kwamba ni kweli wako baadhi ya Maafisa Utumishi ambao wamekuwa hawatekelezi wajibu wao kama inavyopaswa na wamekuwa wakichelewesha kurekebisha mishahara katika mfumo wetu wa ulipaji wa malipo ya mshahara wa *LAWSON*. Nipende kutoa tamko hapa na maelekezo kwa mara nyingine tena, tulishachukua hatua katika Halmashauri ya Bagamoyo, Kilombero, Temeke na nyingine nyingi, hatutamvumilia Afisa Utumishi ye yote au mhusika ye yote katika mamlaka ya ajira ambaye atachelewesha kurekebisha malipo ya mshahara baada ya mtumishi kupandishwa daraja.

Nipende kusema sasa hivi tumeenda mbali itafika wakati tutaanza kuwafungia hata Wakurugenzi wa Halmashauri mishahara yao ili na wenyewe waweze kuona uchungu wa kuchelewesha upandishwaji wa madaraja wa watumishi hao.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 33

Kuiboresha MSD

MHE. NEEMA W. MGAYA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaboresha *MSD* ili dawa zifike kwa wakati?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya mabadiliko makubwa katika utendaji wa *MSD*. Kutokana na malalamiko mengi juu ya utendaji wa *MSD* siku za nyuma, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Serikali iliajiri Kampuni ya Ushauri wa Kitaalam ya Deloitte ili kupitia mfumo wa utendaji kazi wa *MSD* kwa minajili ya kuuboresha. Deloitte walitengeneza ripoti ya utendaji wa *MSD* na kuleta mapendekezo ya maboresho ambayo iliwasilishwa Wizarani mnamo mwezi Januari, 2016. Taarifa hiyo ilikuwa na mapendekezo 21 ya utekelezaji ili kuiboresha *MSD* na kuhakikisha dawa zinafika vituo vya afya kwa wakati kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo hayo yalikuwa pamoja na kuimarisha mifumo ya uwajibikaji ya *MSD*, kuongeza mtaji wa usambazaji dawa, kulipwa kwa deni la *MSD*, kuboresha mifumo ya kusimamia rasilimali watu, kuupitia mnyororo wa ugavi wa dawa nchi nzima na kuondoa kero ya uhaba wa dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupokea ripoti hiyo, Wizara iliunda timu maalum ya kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya Deloitte kuhusu uboreshaji wa *MSD* ikiongozwa na Mganga Mkuu wa Serikali. Napenda kukujulisha kuwa hadi kufikia tarehe 31/7/2017 *MSD* ilikuwa imetekeleza mapendekezo 19 kati ya 21 ya Deloitte. Mapendekezo mawili yaliyosalia ya kuongeza upatikanaji wa dawa na kufuta deni la *MSD* yanaendeea kufanyiwa kazi na yanatarajiwa kukamilika kabla ya Juni, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maboresho hayo ndani ya *MSD*, kwa sasa hali ya upatikanaji wa dawa muhimu imeendelea kuimarika hadi kufikia wastani wa asilimia 80. Aidha, ununuaji wa dawa kutoka moja kwa moja kwa wazalishaji kumepunguza gharama za ununuzi wa dawa kwa wastani wa asilimia 40 na hivyo kuwawezesha wananchi wengi kupata dawa nyingi zaidi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kukujulisha kuwa ili kuhakikisha dawa zinafika kwa wakati, Wizara kuititia msaada wa Mfuko wa Dunia (*Global Fund to Fights Aids, Malaria and Tuberculosis*) inatarajia kuipatia *MSD* magari ya usambazaji 181 kwa ajili ya usambazaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba ili ufanyike kila baada ya miezi miwili badala ya miezi mitatu ya sasa. Utaratibu huu utaongeza upatikanaji wa dawa kuanzia mwezi Januari, 2018.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Neema William Mgaya, swalii la nyongeza.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, napenda kumuuliza kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, deni la *MSD* lilikuwa ni kiasi gani na kiasi gani kimeshalipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, nataka kujuia *MSD* tayari wameshapewa pesa, ni maboresho gani waliofanya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata dawa kwa wakati? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza kwa jitihada anazofanya kuzungumzia masuala mbalimbali yanayohusu afya za wananchi wa Mkoa wa Njombe na ndiyo maana amenialika

kwenye mkoa wake mara mbili ili kwenda kutatua changamoto zinazowakabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, deni la *MSD* mpaka kufikia mwezi Juni, 2016 lilikuwa linafikia shilingi bilioni 143.4 na uhakiki ulikuwa bado unaendelea. Sehemu kubwa ya deni lilikuwa imehakikiwa na mpaka sasa bado uhakiki wa deni hilo unaendelea kufanywa na wenzetu wa Hazina. Tayari pia hatua mbalimbali za kuanza kulipa deni la *MSD* zilikwishaanza kuchukuliwa kwa wenzetu wa Wizara ya Fedha kutuletea pesa kwa ajili ya kulipa deni hilo kila baada ya muda wa miezi mitatu. Mpaka sasa tayari deni la *MSD* limeshapunguzwa kwa takribani shilingi bilioni 12 na linaendelea kuhakikiwa lakini pia kulipwa taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuna changamoto moja kwamba kuanzia 2016 - 2017 Juni, kipindi hiki cha mwaka mmoja hapo, deni pia limeongezeka tena kwa shilingi bilioni 11 na ni kwa sababu ya miradi misonge ambapo kwa kiasi kikubwa inafadhiliwa na taasisi mbalimbali za kimataifa ikiwemo *Global Fund to Fight Malaria, HIV/AIDS and Tuberculosis*. Kwa msingi huo, wanatupa dawa na vifaa tiba lakini tunatakiwa sisi tuingie gharama za ku-clear. Sasa pesa hizi zimekuwa zikichelewa kuja kutoka kwa wenzetu wa Hazina. Kwa hiyo, deni limeendelea tena kuongezeka mpaka kufikia tena shilingi bilioni 144 kufikia Julai, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye majibu ya swalii ya msingi niliyoyatoa hapa nilieleza maboresho mbalimbali ambayo tumeendelea kuyatekeleza kufuatana na ushauri wa kitaalam tuliopewa na taasisi ya kutoa ushauri ya kimataifa ya Deloitte and Touche na mpaka sasa tunaendelea kufanya kazi mapendekezo yao 21 ambayo yalitolewa. Kutilia msisitizo tu ni kwamba changamoto kubwa ambazo zilijionesha katika ripoti ile, pamoja na kuwepo changamoto ya deni, magari machache ya kusambaza dawa na mtaji wa *MSD* kwisha kutokana na madeni kuwa makubwa lakini pia kulikuwa kuna

changamoto nyingine ya kukosekana kwa maoteo (*quantification*) kutoka kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mambo ambayo tumekuwa tukiyaboresha kwa ukaribu sana katika kipindi hiki na sasa upatikanaji wa dawa kwa kweli imekuwa ni suala la kihistoria. Mimi nazunguka sana kwenye vituo vya afya, Hospitali za Wilaya nakuta upatikanaji wa dawa upo kwa zaidi ya asilimia 90 na mpaka sasa wastani umefika asilimia 80. Hakuna mtu atasimama leo hii na kulalamika kwamba kuna upungufu wa dawa kwenye eneo lake. Ukiona imejitokeza hivyo basi ujue *DMO* ama *Mkurugenzi* hawafanyi kazi yao ipasavyo na wala siyo suala la *MSD* ama Serikali Kuu. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khadija Nassir, swali la nyongeza.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunionna.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kwenye Halmashauri zetu juu ya uhaba au ukosefu wa dawa lakini taarifa za Naibu Waziri hapa anasema kwamba dawa zipo. Sasa nilikuwa naomba tu Mheshimiwa Naibu Waziri atupe maelezo juu ya hili kwa kina zaidi. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, utakapokuja kujibu hapa naomba uchukue muda mfupi kwa sababu umeshatoa maelezo marefu ya mwanzo, kwa hiyo, ye ye anahitaji tu msisitizo. Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nisimame kwa sababu Naibu Waziri ametoa majibu mazuri sana lakini bado mdogo wangu Mheshimiwa Khadija Nassir anauliza swali kuhusu upatikanaji wa dawa. Kwa hiyo, nataka kidogo nitoe uelewa, tunapima viyi upatikanaji wa dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapima upatikanaji wa dawa, dawa ziko zaidi ya elfu mbili, elfu tatu, elfu nne, lakini katika ngazi ya *MSD* tumechagua dawa 135 muhimu zaidi kwa mujibu wa Mwongozo wa *WHO* kwamba hizo ndiyo dawa muhimu zaidi ambazo zinatakiwa kuwepo muda wote katika ngazi ya *MSD* katika nchi. Kwa hiyo, kama alivyosema Naibu Waziri, *MSD* kat iya hizo aina 135 za dawa, tuna zaidi ya asilimia 82. Kwa hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri au *DMO* anapoomba aina 100 za dawa atapata angalau aina 82 za dawa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ya kupima upatikanaji wa dawa, katika zile dawa 135 tumechagua aina 30 za dawa ambazo tunaita *life serving medicines*, za malaria, maambukizi ya bakteria, *HIV*, dawa za akina mama wajawazito na kila kitu. Kwa hiyo, ndiyo maana Naibu Waziri sasa hivi na mimi ambavyo tunaenda kwenye vituo tunamuuliza Mganga Mkuu wa Wilaya katika zile *tracer medicine* 30 leo mgonjwa akiumwa ziko aina ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo taarifa ya TAMISEMI, anachosema Naibu Waziri ni sahihi. Mikoa hii imeonesha kwamba sasa hivi hali ya upatikanaji wa dawa katika mikoa na katika vituo ni zaidi ya asilimia 80 mpaka 90. Kwa hiyo, huo ndiyo ufanuzi na ndiyo ukweli...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka kutoa changamoto moja, dawa hazipatikani bure, wananchi wanatakiwa kuchangia kupata dawa. Kwa hiyo, lazima pia tuwahimize watu wakate bima za afya.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, tuko vizuri na nataka kurudia, hata *NGOs* kama SIKIKA ambazo ziliikuwa zinatuandikia taarifa mbaya kuhusu hali ya upatikanaji wa

dawa wametoa taarifa na kuthibitisha dawa ni zaidi ya asilimia 80. (*Makofii*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, pia Jarida la Kimataifa la Famasia limethibitisha hali ya upatikanaji wa dawa muhimu Tanzania ni zaidi ya asilimia 80. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuwekeza kwenye upatikanaji wa dawa nchini Tanzania. Ahsante sana. (*Makofii*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Heche, kama unataka kuzungumza na Waziri, zunguka huku nyuma uende ukazungumze naye pale.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Mbunge wa Pangani, sasa aulize swali lake.

Na. 34

Barabara Kichocheo Kikubwa cha Maendeleo

MHE. JUMAA H. AWESO aliuliza:-

Ujenzi wa barabara ni kichocheo kikubwa cha maendeleo ya kiuchumi na hata ajira na mawasiliano.

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani – Saadani hadi Bagamoyo utaanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Tanga – Pangani – Saadani - Bagamoyo yenye urefu wa kilometra 246 unajumuisha madaraja makubwa ya Pangani na Wami Chini, barabara za mchepuo katika Jiji la Tanga na Mji wa Pangani pamoja na barabara zinazoingia kwenye hoteli za kitalii za ufukwe wa Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni sehemu ya Mradi wa Kikanda wa Barabara ya Malindi – Mombasa – Lungalunga – Tanga – Pangani - Saadani haadi Bagamoyo na unaratibiwa na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya upembizi yakinifu na usanifu wa kina ilikamilika mwezi Juni, 2015 chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*African Development Bank*). Aidha, kutohana na gharama za mradi huu kuwa kubwa, taratibu za kupata fedha kutoka *African Development Bank* na washirika wa maendeleo wengine zimechukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetenga shilingi milioni 4,435 kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Tanga – Pangani – Saadani - Bagamoyo wakati taratibu za kupata fedha zaidi kutoka *African Development Bank* na washirika wa maendeleo zinaendelea.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, swalii la nyongeza.

MHE. JUMAA H. AWESO: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Napozungumzia ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani – Saadani, nazungumzia uchumi na maisha ya wananchi wangu wa Jimbo la Pangani.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa barabara hii ni ahadi ya muda mrefu na ujenzi wake umekuwa wa kususua yaani ahadi hii tangu mimi sijazaliwa mpaka sasa hivi nimekuwa Mbunge. Kwa kuwa Serikali imesahatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii ya Tanga – Pangani – Saadani, nini kinachokwamisha kuanza kwa ujenzi wa barabara hii na wananchi wangu kulipwa fidia? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, pamoja na nia njema ya Serikali kuhakikisha kwamba inajenga barabara ya Tanga – Pangani – Saadani, yapo maeneo korofii ambayo yanasa babisha matatizo na usumbufu kwa wananchi wangu, mfano ni eneo la kutoka Mkwaja kwenda Mkaramo, Tundaua kwenda Kirare.

Je, Serikali ina mkakati gani wa muda mfupi na wa haraka ili kuhakikisha kwamba maeneo haya yanarekebishwa ili wananchi wangu wasipate tabu kwa muda huu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika swalii la msingi, barabara hii imetengewa fedha shilingi milioni 4,435. Nimhakikishie tu hiyo ndiyo dalili njema, huo ndiyo ushahidi kwamba sasa Serikali imedhamiria kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara hii ni pamoja na kuwalipa fidia wale wote wanaostahili fidia namna barabara hii itakavyopita.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Pangani na wengine ambaao wanaguswa na barabara hii, dhamira ya Serikali ya kuijenga barabara hii iko palepale na tumeshaanza na tunatarajia muda si mrefu washirika wa maendeleo pamoja na *African Development*

Bank kwa namna mazungumzo yanavyoendelea tutakuja kuongezewa fedha ili tukamilishe kazi hiyo kwa umakini unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kipande cha Mkaramo hadi Mkwaja, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Meneja wetu wa *TANROADS* Mkoa wa Tanga ataliangalia hili alete taarifa yake, ghamama ya kurekebisha hiki kipande kidogo ili mawasiliano yawepo katika muda wote wa mwaka.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hussein, swali la nyongeza.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Rais wa Awamu ya Nne alifanya ziara yake katika Wilaya ya Nyang'hwale na kuahidi ujenzi wa barabara kutoka Kahama – Nyang'holongo – Bikwimba – Karumwa – Nyijundu – Busolwa – Ngoma - Busisi (Sengerema) kwa kiwango cha lami. Pia 2010 Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano na ye ye alifanya ziara katika Wilaya hiyo ya Nyang'hwale na kuahidi ahadi hiyo hiyo ya ujenzi wa barabara hiyo hiyo. Je, kauli ya Serikali ni lini upembuzi yakinifu utaanza kwa ujenzi wa barabara hiyo ya lami kutoka Kahama - Karumwa - Busisi? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia sana kuhusu ujenzi wa barabara hii na kwa sababu hiyo anafahamu mimi niliamua kupita barabara hii wakati nikotoka Mwanza na Geita na kweli nimeona umuhimu wa barabara hii walau sasa wataalam watakachokuwa wanaeleza nitakuwa nafahamu wanachosema ni nini. Nikuhakikishie, mara fedha zitakapopatikana kwa shughuli hii kazi hii itafanyika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bwanausi, swali la nyongeza.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala – Masasi imeshaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kuanzia Mtwara. Je, Mheshimiwa Waziri anawathibitishia nini wananchi ambao walipaswa kulipwa fidia zao wanalipwa fidia haraka ili kupisha ujenzi huo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Mbunge, tulishajadiliana kuhusu suala hili na tulikubaliana kwamba tuangalie namna zile fedha zilizotengwa ni kiasi gani kitumike kwa ajili ya fidia na kiasi gani kiendelee kukamilisha ujenzi wa barabara ile. Nimuombe tu tuwasiliane ili hatimaye tukubaliane yeye na sisi. Ninachomhakikishia wote wanaostahili kulipwa fidia katika barabara ile watalipwa fidia, hakuna ambaye hatalipwa fidia. Hilo ndilo ninalokuhakikishia na nilikwambia hivyo kabla, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rhoda Kunchela, swali la nyongeza.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nilitaka nipate ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kuna ujenzi wa barabara ambao unaendelea ya kutoka Sumbawanga – Stalike – Kigoma. Barabara ile kuna maeneo ambayo tayari ujenzi umeshapita na wananchi wanaoishi pembezoni mwa barabara ya kwenda Kigoma wameshahamishwa na baadhi ya wananchi tayari walishalipwa fidia lakini kuna wengine wamerukwa. Sasa

Serikali inatumia utaratibu gani kuendelea kuwabagua kuwalipa baadhi ya wananchi fidia na wengine kuwaruka?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ujenzi wa barabara hii ya kutoka Sumbawanga - Stalike - Kigoma unaendelea na unafahamu kwamba kwa sasa tunajenga vile vipande viwili ambavyo wakandarasi wako kwenye eneo na lingine lile la kutoka Mpanda - Tanganyika unafahamu kwamba tuna fedha lakini napo tunatarajia mkandarasi hivi karibuni atakuwepo *site* na tunaendelea kutafuta fedha kukamilisha kabisa hadi Kigoma. Nikuombe tu kwa kawaida ulipaji wa fidia ni kutegemea na makadirio yaliyofanywa na *valuers* wallopita katika maeneo hayo. Mara nyingi inatokea maeneo mengine kuna watu ama wanarukwa na wakati mwingine wanarukwa kwa sababu wakati ule *valuation* inafanyika pengine yule mtu hakuwepo. Kwa hiyo, nikuombe tu suala hili tutaendelea kulishughulikia na tushirikiane kuhakikisha kwamba wale waliosahaulika na kama kweli wana haki wapate haki yao. Sisi muda wote tunasema mwenye haki ya kulipwa fidia ni lazima alipwe fidia na kwa vyovypote kama kuna watu ambao hawana haki ya kulipwa fidia hatutawalipa fidia.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Mheshimiwa Omar Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 35

**Ujenzi wa Barabara ya Handeni - Kiberashi
- Kiteto - Nchemba**

MHE. OMARI A. KIGODA aliuliza:-

Serikali iliahidi kutoa kipaumbele kwa barabara zinazounganisha mikoa.

Je, ni lini barabara ya Handeni – Kiberashi – Kiteto – Nchemba na Singida itaanza kujwengwa ili kuunganisha mikoa minne ambayo ni ya kiuchumi hususan kilimo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kijungu – Chemba – Kwamtoro hadi Singida yenye urefu wa kilometra 461 umekamilika. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii kiuchumi na kijamii, Serikali inaendelea kuhakikisha kuwa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii unatekelezwa ili kuunganisha mikoa inakopita na maeneo mengine hasa ukizingatia hivi sasa tuna mradi wa kujenga bomba la mafuta linalotoka Uganda kwa maana ya Hoima hadi Tanzania kwa maana ya Tanga.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda, swali la nyongeza.

MHE. OMARI A. KIGODA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kila kitu karibia kimeshakamilika, wananchi wa Handeni, Kiberashi, Kijungu, Kiteto na Nchemba wao wanataka kujua ni lini huu mradi utaanza? Ahsante sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu kuwahakikishia wananchi wa maeneo hayo yote aliyoyataja kuanzia Handeni – Kiberashi – Kijungu – Kiteto – Nchemba - Kwamtoro hadi Singida ambako barabara hii itapita, Serikali imedhamiria kwa dhati kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Mwaka huu wa fedha ndiyo tunaanza kufanya maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami na tumetenga shilingi milioni 500 kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la nyongeza.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niishukuru Serikali kwa ujenzi wa barabara ya lami inayotoka Nela kuelekea Kiwanja cha Ndege. Niulize swali dogo, kwa kiwango hicho hicho ni lini Serikali sasa itaanza mpango wa kuboresha barabara kwa kiwango cha njia nne kutoka mjini katikati kwa maana ya barabara ya Kenyatta kwenda Shinyanga kuititia Kata za Mkuyuni, Igogo, Mkolani, Nyegesi pamoja na Buhongwa ili na yenyewe iweze kufanana na yale mazingira yaliyopo? Nakushukuru. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Stanslaus Mabula na wananchi wa Mkoa wa Mwanza, ni kweli Jiji lile sasa lina hadhi kubwa na kwa kweli barabara zake nazo lazima tuhakikishe zinakuwa katika hadhi inayostahili Jiji lile. Nimepokea

maombi yake, mimi nimechukulia hayo kama ni maombi, nitakwenda niyawasilishe kwa wataalam waanze kuangalia uwezekano wa kufikiria hilo ombi ambalo Mheshimiwa Stanslaus Mabula amelieleza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mussa Mbarouk, swali la nyongeza.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza niseme nashukuru kwa Serikali kutenga takribani shilingi bilioni nne kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Pangani. Je, ni lini kazi rasmi ya ujenzi wa barabara hiyo itaanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba kumpongeza sana huyu Mheshimiwa Mbarouk kwa sababu anashirkiana vizuri na Wabunge wenzake wa Tanga katika kuhakikisha maendeleo katika maeneo yao yanafanikiwa bila kujali itikadi. Nikupongeze sana kwa sababu hatimaye ni wananchi wanaotuleta humu ndani na hatimaye ni wananchi watakaotuondoa tusipoangalia *interest* za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie kama ambavyo nilijibu kwenye swali la msingi la Mheshimiwa Aweso ni kwamba mwaka huu wa fedha tumetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza maandalizi ya kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara una hatua, hii ndio hatua ya kwanza tunaianza mwaka huu wa fedha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hussein Bashe, swali la nyongeza.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nataka nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba mwaka 2010 wananchi wa Jimbo la Nzega

waliahidiwa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete kilometra 10 za lami ndani ya Mji wa Nzega. Mwaka 2014, Waziri wa Ujenzi ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sasa aliwaahidi tena mbele ya Rais Kikwete ahadi hiyo hiyo. Mwaka 2015 Rais wa sasa, Rais John Pombe Magufuli aliwaahidi wananchi wa Jimbo la Nzega ujenzi wa Daraja la Nhobola na kilometra kumi za lami ndani ya Mji wa Nzega. Waziri wa TAMISEMI ndani ya Bunge hili mwaka 2016 akijibu swalilangu la msingi alisema Serikali inashughulikia ujenzi wa Daraja la Nhobola katika bajeti ya 2016/2017 na Naibu Waziri Ngonyani katika Bunge lililopita aliahidi daraja hili litajengwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Naibu Waziri anijibu ni lini ahadi ya daraja hili itatimizwa katika Halmashauri ya Mji wa Nzega? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Hussein Bashe na wananchi wa Nzega kwamba ahadi zilizotolewa na viongozi mbalimbali ama ndani ya Bunge kwa kujibu maswali, wakati wa ziara ama wakati wa kampeni kuhusu ujenzi wa hayo maeneo mawili aliyoyasema, ujenzi wa kilometra kumi pamoja na daraja la Nhobola maana yake hii siyo mara kwanza kuliuliza hili suala, nikuahikikishie kama ambavyo tumekuhakikishia siku za nyuma kwamba ahadi hii itatekelezwa katika Serikali hii ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimhakikishia Mheshimiwa Mbunge hilo, na ni kweli tulisema kwamba tungeweka kwenye bajeti ya 2016/2017 na unafahamu kwamba bajeti ni mchakato, kikubwa nachokwambia ni kwamba Serikali itatekeleza ahadi hii ya viongozi mbalimbali pamoja na sisi ambao tumekuwa tukijibu maswali hapa kwa niaba ya Serikali.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, sasa aulize swali lake.

Na. 36

Kuboresha Mafao ya Wastaifu Nchini

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM aliuliza:-

Kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wastaifu ambao wakati wa utumishi wao walilitumikia Taifa hili kwa uaminifu na uadilifu mkubwa lakini kumekuwa na hali ya kucheleweshewa mafao yao ya uezemi yasiyolingana na kupanda kwa gharama za maisha, hali inayosababisha kuwa na maisha magumu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mafao ya uezemi ili kuondoa malalamiko hayo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibuu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mafao ya kustaafu hukokotolewa kwa kutumia muda wa utumishi ambao mtumishi alikuwa katika utumishi na mshahara ambao mtumishi alikuwa analipwa kabla ya tarehe ya kustaafu. Ukokotoaji huo ndiyo unaotoa kiwango cha kiinua mgongo anachostahili kulipwa kwa mkupuo na kiwango cha pensheni atakachoendelea kulipwa kila mwezi. Kwa utaratibu huo, viwango vya pensheni hutofautiana kati ya mstaafu mmoja na mwingine kutegemea muda wake wa utumishi na mshahara kabla ya tarehe kustaafu. Iwapo katika

ukokotoaji, itajitokeza pensheni ya mstaafu kuwa chini ya kima cha chini cha kiwango cha pensheni anacholipwa, mstaafu atalipwa kima cha chini cha pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha viwango vya pensheni ili kukidhi mahitaji muhimu ya kila siku ya wastaifu. Kwa kutambua hivyo, Serikali iliboresha viwango vya pensheni mwezi Julai 2015 ambapo kima cha chini kiliongezwa kutoka shilingi 50,114 hadi shilingi 100,125 kwa mwezi. Hata hivyo, maboresho ya viwango vya pensheni kwa wastaifu yasiyoendana na maboresho ya miundombinu ya kiuchumi na huduma za kijamii hayawezi kuondoa malalamiko ya wastaifu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunatambua kwamba mapato ya Serikali ni madogo ikillinganishwa na mahitaji muhimu ya kitaifa. Kwa kutambua kuwa ni miaka miwili tu tangu tuongeze kima cha chini cha pensheni, Serikali kwa sasa imejielekeza zaidi katika kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji, nishati ya umeme, maji, huduma za afya na elimu. Maeneo haya yana uhitaji mkubwa sana wa rasilimali fedha. Aidha, matokeo mtawanyiko ya maboresho ya maeneo haya yanaleta unafuu mkubwa wa maisha ya wastaifu wetu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inafanya juhudzi za makusudi za kuboresha mifumo ya kukusanya mapato sambamba na kuboresha miundombinu ya kiuchumi na kijamii ili kujenga uwezo wa kuboresha maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza ya pensheni kwa wastaifu, mishahara na maslahi mazuri kwa watumishi wa umma itawezekana tu kama tutafanikisha mikakati na azma ya Serikali ya kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wetu. Hivyo basi, tuendelee kuiunguza mkono Serikali yetu katika juhudzi zake za kujenga uchumi imara, uchumi wa viwanda ambaao ndiyo msingi mkuu wa kuimarisha mapato ya Serikali.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, swali la nyongeza.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kupata nafasi ya kuiliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, imekuwa ni mazoea ripoti kadhaa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) katika miaka mbalimbali zimekuwa zikionyesha kwamba mafao ya wastaifu yanakuwa yakipunjwa kwa makusudi na Serikali imekuwa ikieleza kwamba ni wakati wa kukokotoa ndiyo matatizo hayo yanatokea.

Je, ni kwa nini basi mmekuwa mkiwapunja na kuwanyanya kwa makusudi na hali zao za maisha zimekuwa ni mbaya na tatizo hili limekuwa la muda mrefu, *CAG* analalamika lakini Serikali imekuwa haifuatilii kwa makini, tabia hii mbaya ya Serikali ya kuwapunja/ kuwadhulumu wastaifu mtaacha lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba shilingi 50,000 ambayo ilikuwa miaka iliyopita mkapandisha mpaka shilingi 100,000 ambayo ni wastani wa shilingi 3,300 kwa siku. Katika majibu yako ukasema kwamba sasa mnajielekeza kwenye miundombinu ya usafiri, usafirishaji, nishati na umeme, hivi watu hawa ambao mliwatuma wakiwa wazima wakafanya kazi hii kwa uadilifu na uaminifu mkubwa mnawapatia shilingi 3,300, mtuambie waziwazi mkakati wa Serikali wa ziada wa kuboresha maisha ya wastaifu kwa kuongeza pensheni hii utafanyika lini siyo kubakia na majibu haya tu kwamba mnajielekeza kwenye usafirishaji na usafiri hawa mnawatumwa wakiwa na nguvu sasa mmewaacha mnawatelekeza, tabia hiyo mbaya Serikali mtaacha lini? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Sasa Mheshimiwa Masoud mbona kama umetoa majibu mwenyewe kwa hilo swali? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la kwanza, kusema kwamba Serikali ina tabia mbaya ya kuendelea kuwapunja wastaafu wetu, hii siyo sahihi hata kidogo. Nasema siyo sahihi hata kidogo kwa sababu nimemueleza mafao ya wastaafu hukokotolewa kwa kanuni ambayo imekubalika ndani ya Serikali na wastaafu, kwa hiyo, hakuna sehemu yoyote ambako mstaafu anapunjwa na Serikali yetu, hilo halipo hata kidogo. Kwa hiyo, kanuni iko wazi na inatumika na kila mstaafu anapojiunga na mfuko wowote huiona kanuni hii kabla ya kujinga na mifuko hii.

Kwa hiyo, napenda wananchi wetu waelewe, Serikali yetu ina nia njema na dhamira ya dhati ya kuhakikisha wastaafu wanalipwa katika msingi ambaao ni mzuri kabisa na ndicho ambacho Serikali tumekuwa tukifanya. Ndio maana 2015 tumeongeza kiwango hiki kutoka shilingi 50,000 mpaka shilingi 100,000 kima cha chini. Wapo wanaolipwa vizuri zaidi kwa sababu nimesema *formula* hii inategemea na muda wake wa utumishi pamoja na mshahara wake wa mwisho aliostaafu nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili kwamba Serikali ina mkakati gani, nimemueleza vizuri kabisa kwamba Serikali yetu na sote sisi ni mashahidi tunapambanza kuhakikisha tunaongeza mapato ya Taifa letu, tunaweza kukusanya kodi yetu na sote tunaona.

Pia nimesema wazi, ukiongeza pensheni kwa ajili ya wastaafu tu wakati hakuna dawa, maji na huduma nyingine muhimu za jamii haitoleta maana yoyote kwa Taifa letu. Tunawathamini wastaafu wetu, tunaendelea kufanya nao kazi vizuri na tutaendelea kuwalipa jinsi ambavyo mapato ya Taifa letu yanavyoimarika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ni kweli kabisa kwamba wastaafu

wanateseka sana na wengi wao wanapoteza maisha. Ni katika Bunge hili hili, Mheshimiwa Naibu Waziri aliliahidi Bunge kwamba wastaafu wote wanaodai malimbikizo baada ya marekebisho ya kima cha chini kutoka shilingi 50,000 kwenda shilingi 100,000 watalipwa fedha zao kwa maana *arrears* zote lakini ni takribani miaka miwili sasa wastaafu hawa hawajalipwa fedha zao sana sana ni wale ambao walikuwa kwenye PSPF na PPF.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningetaka kujuu ni kwa nini Serikali haijaweza kuwalipa hawa wastaafu haya malimbikizo kama ambavyo Naibu Waziri uliahidi Bunge hili na je mnavyoenda kuwalipa...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko ni maswali ya nyongeza kwa hiyo unauliza moja tu. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kukanusha kwamba ni miaka miwili wastaafu hawa hawajalipwa ile nyongeza, siyo sahihi hata kidogo. Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii wameanza kulipa kima cha chini kilichoongezwa na Serikali kuanzia mwezi Januari, 2017. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili aliloli-*quote* ye ye kwamba niliahidi hapa, nakumbuka wakati najibu swali hili nillieleza Bunge lako Tukufu kwamba kulingana na Sheria ya SSRA, regulatoranaye-regulate Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii, ni Bodi za Wadhamini za mifuko husika baada ya *actuarial valuation* ndizo zinazoamua sasa kulipa kiwango hiki na ndipo baada ya kufanya *actuarial valuation* Bodi zote zimeidhinisha na tumeanza kulipa kwa kipindi chote kuanzia Januari mpaka leo tunapoongea wote wanalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua yapo malalamiko wanasema kwamba wengine hawaoni hizo *transaction* lakini naomba niwaambie kwamba hasa kwa wastaafu wetu wanaolipwa na PSPF siku za nyuma pensheni zao za kila mwezi zilikuwa zikianza kulipwa kabla ya hii *addition* kwa

hiyo kulikuwa kunaonekana kuna *two transaction* ndani ya mwezi mmoja kwa utofauti wa wiki moja au wiki mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali yetu inalipa nyongeza hii kwa sababu nyongeza hii hasa kwa PSPFhulipwa kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina, tunalipa kwa wakati na wanalipwa siku moja pensheni yao pamoja na ile nyongeza yao. Kwa hiyo, hakuna sehemu yoyote ambapo hawalipwi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hawa Mchafu, swalii la nyongeza.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Waraka wa SSRA Namba 1 wa mwaka 2006 unasema kwamba mstaafu atakayecheleweshewa mafao yake, Mfuko husika wa Hifadhi ya Jamii utatakiwa kumfidia, waraka huo unaonekana kutokuwa na nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nini sasa mkakati kabambe wa Serikali kuhakikisha tabia ya ucheleweshaji wa mafao ya wastaafu inakoma? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha kwa majibu yake mazuri na nampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa waajiri wengi lakini na mifuko kwa maana nyingine wamekuwa wakichelewesha ulipaji wa mafao ya wastaafu wetu kwa namna moja ama nyingine. Kupitia SSRA tumeweka sasa mkakati maalum na kupitia maboresho pia ya Sheria za Kazi ambayo yalifanyika ndani ya Bunge lako hili Tukufu, tumewapa nguvu pia Maafisa Kazi wetu ambao sasa wamepata ya

kukagua, wanapokwenda kukagua masuala ya kazi, wanakwenda pia kukagua *compliance* ya mifuko na waajiri katika kushughulikia pensheni za wastaafu na michango ya waajiri kwenye mifuko ya pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mbunge kwamba Serikali inalismamia hili kupitia *SSRA* lakini pia kupitia ofisi zetu za kazi tutaendelea kuhakikisha kwamba waajiri na mifuko ya pensheni inafanya *compliance* katika sharia zote tulizonazo na wastaafu wetu wapate mafao yao kwa wakati na waajiri wapeleke michango yao kwa wakati.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Taofiq, swali la nyongeza.

MHE. FATMA H. TAOFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naona swali nililotaka kuliuliza ameshaliuliza Mheshimiwa Mchafu, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 37

Tatizo la Tembo katika Mkoa wa Mara

MHE. JOYCE B. SOKOMBI aliuliza:-

Katika Mkoa wa Mara kuna usumbufu mkubwa unaosababishwa na tembo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti tembo hao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na madhara yanayosababishwa na wanyamapori, hususan tembo, Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kunusuru maisha na mali za wananchi waishio kando ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Kwanza, Serikali imeunda timu ya udhibiti wa wanyamapori hatari na waharibifu ambayo inajumuisha watumishi 14 kutoka kikosi dhidi ya ujangili kilichopo Bunda, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Pori la Akiba Ikorongo – Gurumeti, Halmashauri ya Wilaya na *Gurumeti Reserves*. Lengo ni kuhakikisha kwamba tukio lolote la uvamizi wa tembo linashughulikiwa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuweka minara (*observations towers*) ambayo askari wanyamapori wanatumia kufuatilia mwenendo wa tembo ili pale wanapotoka nje ya hifadhi, hatua za kuwadhibiti zichukuliwe na tatu, kuweka mizinga ya nyuki pembezoni mwa mashamba ili tembo wanapoingia katika mashamba wafukuzwe na nyuki.

Nne, kutumia ndege zisizokuwa na rubani (*unmanned aerial vehicles*) kwa ajili ya kufukuza tembo. Mafunzo ya kutumia ndege hizo yametolewa kwa watumishi kwa kushirikiana na Shirika la *World Animal Protection*. Kwa ajili hiyo, Pori la Ikorongo limepeewa ndege moja, Halmashauri ya Serengeti imepewa moja na Kikosi Dhidi ya Ujangili Bunda kimepeewa ndege moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi kwa jamii ili wananchi waepuke kulima katika shoroba za wanyamapori. Sita, kuendelea kufanya utafiti na kushauri wananchi kulima mazao ambayo hayavutii kuliwa na wanyamapori na saba, kuhamasisha Halmashauri ya Wilaya kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na jitihada hizi, matukio ya uvamizi wa tembo yamepungua kutoka 128 mwaka 2015/2016 hadi 105 katika mwaka 2016/2017. Aidha, katika mwaka 2015/2016, tembo waliweza kufanya uharibifu hadi umbali wa kilometra 30 kutoka kwenye hifadhi, lakini kwa mwaka 2016/2017 umbali huo umepungua hadi kilometra 12 tu.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika sana. Majanga ya tembo katika Mkoa wa Mara na Tanzania kwa ujumla ni makubwa sana, lakini majibu ya Waziri yamekuwa ni mepesi sana. Nitanukuu, naambiwa kwamba kuanzia mwaka 2015 mpaka 2016 ni matukio 128 na mwaka 2016 mpaka 2017 wamepunguza hadi 105, kwa maana hiyo matukio waliyoweza kuyapunguza ni 23 tu. Hatuoni kwamba itachukua muda mrefu sana mpaka kuhakikisha kwamba tatizo la tembo hapa Tanzania kwa ujumla litakuwa bado ni tatizo kubwa sana kwa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine, hawa tembo zamani wananchi walikuwa wanajichukulia wenyewe hatua mikononi na tembo hawa walikuwa hawasumbui wananchi. Lakini kwa sababu Serikali imeona kwamba tembo ni wa thamani kuliko binadamu, na ukiua tembo ni shida unafungwa miaka mingi, na tembo akiua binadamu ni halali. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri aje na majibu mazuri kwa wananchi wa Mkoa wa Mara, je, warudi kule kule wajichukulie hatua mkononi? Kwa sababu ile nyama ya tembo inaliwa na wanasema kwamba aidha...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sokombi si umeshauliza maswali mawili tayari? Umeshauliza mawili, labda kama unafuta mojawapo ya hayo mawili ambacho sikushauri, kwa hiyo tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri ajibu hayo maswali mawili.

Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kweli kwamba uvamizi wa tembo katika maeneo ya wananchi ni changamoto kubwa katika maeneo ya Bunda, Tarime na Serengeti. Hata hivyo Serikali inachukua kila aina ya hatua kuhakikisha kwamba inapambana na kuzuia hali hii, na orodha ya hatua ambazo zimechukuliwa nimezitaja. Pamoja na hayo, tunaendelea na utafiti wa kuweza kutambua njia nydingine bora zaidi za kukabiliana na jambo hili. Na Mheshimiwa Mbunge atakuwa ni shahidi kwamba wafanyakazi wetu pamoja na wafanyakazi wa Halmashauri wanafanya juhudhi kubwa sana ya kusaidia wananchi katika jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, si kweli kabisa kwamba tembo ni bora kuliko wananchi. Lakini ni jambo lisilopingika kwamba wanyamapor ni rasilimali kubwa yetu sisi sote kama wananchi wa Tanzania na tunawashukuru sana wananchi wa Mara kwa juhudhi kubwa ambazo wanafanya kusaidia nchi nzima katika kuwahifadhi wanyama hawa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mmesimama wengi, hili tatizo la tembo liko maeneo mengi sana. Sasa inanipa wakati mgumu sana kumchagua nani na nani nimuache, maana mmesimama wengi sana.

Mheshimiwa Willy Qambalo, swali la nyongeza.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, uko utaratibu kama si sheria au kanuni katika nchi hii, kwamba mifugo ya wananchi au wananchi wenyewe wakiingia kwenye hifadhi kuna tozo inawakuta. Je, Mheshimiwa Waziri haoni ili kuondokana na hili tatizo la wanyama kutoka nje umefika wakati sasa wanyama wakitoka nje kwenye maeneo ya wananchi, tozo hiyo hiyo ambayo wananchi wanatozwa wakiingia kwenye hifadhi nayo itozwe? Nakushukuru. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, wanyamapori si binadamu na wanyamaporи hawana akili za kibinadamu, ni wanyama wa porini. Kwa hiyo, tujitahidi sana kuwalinda kwa kuwaeleza askari wanyamaporи pale wanapotokea na mimi nasema kwa kweli ni furaha kubwa kwamba kwa mara ya kwanza sasa tembo wameongezeka kutokana na hali mbaya ya ujangili iliyokuwepo hapa nchini na sasa wanaonekana, wanakuja mpaka kwenye maeneo ya watu. Rai yangu kwa kweli tushirikiane ili tuwataarifu askari wanyamaporи pale wanyama hao wanapotokea na sisi tunachukua hatua haraka iwezekanavyo kila tukio la namna hii linapotokea.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Raphael Chegeni swali la nyongeza.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri katoa majibu mazuri sana, lakini mimi nina *concern* moja kubwa kwamba hawa tembo madhara yao ni makubwa sana katika Wilaya ya Busega ambayo inapakana na Wilaya za Bunda na Serengeti. Maelezo ya Mheshimiwa Waziri katika majibu yake amesema kwamba hawa tembo wanazidi kudhibitiwa, lakini mwishoni amesema kwamba tembo wameongezeka zaidi, sasa sjaaelewa kwamba sasa kwa vile wameongezeka zaidi madhara yatakuwa makubwa kwa wananchi. Serikali sasa kupitia Wizara yake ina mkakati gani kuwaokoa wananchi ambao wanasumbuliwa na tembo kwa kusababishiwa hasara kubwa zaidi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma nchi yetu ilikuwa na tembo wengi sana, wanafika 110,000, hivi sasa hatua tuliyofikia hapa wanyama hawa walipunguzwa sana na ujangili wakafika chini ya 10,000. Sasa hivi ndiyo idadi hiyo inaanza kukua na tunaanza

kuwaona. Katika eneo lile la Serengeti na eneo la Maswa tunafanya utafiti kuangalia kama tunaweza kujenga uzio wa kuwatenganisha watu, mashamba yao na hifadhi. Tunafanya mazungumzo na wawekezaji wakubwa hapa nchini kwetu na mazungumzo yanaelekea vizuri. Sikupenda nifike mahali ninasema jambo hili, lakini Serikali inalichukulia jambo hili kwa uzito mkubwa sana na ndiyo maana tunafanya utafiti wa uwezekano wa kujenga uzio wa kilometra 140 tuone kwamba italeta afueni kiasi gani katika kuwadhibiti wanyama hawa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumalizie swalı letu la mwisho kwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo sasa aulize swalı lake.

Na. 38

Mradi wa Skimu ya Umwagiliaji – Kata ya Ulumi

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE aliuliza:-

Ujenzi wa skimu ya umwagiliaji katika Kijiji cha Ulumi kilichopo Kata ya Ulumi ambao ulianza kujengwa mwaka 2010 haujakamilika mpaka sasa.

(a) Je, ni sababu zipi zimefanya mradi huo kutokamilika mpaka sasa na ni lini utakamilika?

(b) Je, Serikali ilitenga kiasi gani cha fedha katika bajeti ya mwaka 2017/2018 ili kukamilisha mradi huu?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swalı la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Jimbo la Kalambo lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa ujenzi wa Mradi wa Umwagiliaji Ulumi ulianza kujengwa mwaka 2012

kwa kujenga banio lenye gharama ya shilingi milioni 213,279,000 kupitia Mfuko wa Ushirikiano wa Msaada wa Chakula baina ya Serikali ya Tanzania na Japan bila kuhusisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji mashambani ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.3 zinahitajika kukamilisha kazi zote. Aidha, Wizara yangu hivi sasa inafanya mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002 kwa lengo la kuihuisha ili uendane na hali ya sasa. Kazi hii inatarajia kukamilika mwezi Septemba mwaka 2018 na kupitia mpango huu Mradi wa Ulumi ni mionganini mwa miradi iliopewa kipaumbele kwa ajili ya uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji kwa manufaa ya wananchi wa Ulumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa mradi huu kwa wananchi wa Kalambo, Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2018/2019 itaingiza mradi huu katika bajeti kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ili mradi huu uweze kuanza utekelezaji.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali. Kwa kutambua na kukiri umuhimu wa mradi huu, naomba nipiatiwe majibu; lini mradi huu utakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, naomba *commitment*ya Serikali kwamba hiyo 2018/2019 hakika pesa itatengwa kwenye bajeti.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na swali la Mheshimiwa Mbunge kwamba lini utakamilika, mradi huu kujua ni lini utakamilika ni baada ya kukamilisha usanifu na kuingia mikataba ndipo tarehe itapangwa, kulingana na *scope* ya kazi itakayojitokeza ndiyo tutajua ni lini mradi utakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ni *commitment*. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali yetu iko *committed*kuhakikisha kwamba inanyanya na kilimo cha umwagiliaji ili tuweze kuondokana na njaa. Na Mkoa wa Rukwa ni mionganini mwa mikoa mitano ambayo

inazalisha chakula kwa wingi, kwa hiyo kwa mikoa hii Serikali iko *committed* kuhakikisha kwamba tunaendeleza kilimo cha umwagiliaji; tutahakikisha kwamba bajeti hii tunaitenga.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dunstan Kitandula swalii la nyongeza.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niulize swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Skimu ya Umwagiliaji ya Ulumi inafanana sana na Skimu ya Umwagiliaji ya Mwakijembe. Mwaka 2010 Serikali ilitumia shilingi bilioni 1.2 kujenga Skimu ya Umwagiliaji ya Mwakijembe, lakini bahati mbaya sana skimu ile mifereji haikujengewa wala hakuna bwawa liliojengwa kuvuna maji. Matokeo yake, leo hii tunapozungumza *its hardly 10 percent* ya mradi ndiyo imetumika. Nini kauli ya Serikali kuhakikisha skimu ile inafanya kazi?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa, ndiyo maana Serikali kwa kupitia msaada wa Serikali ya Japani sasa hivi mhandisi mshauri anapita nchi nzima ili kubaini matatizo ya miradi ya umwagiliaji ambayo imefanya *efficiency* ya miradi ya umwagiliaji isiwe nzuri. Ni kweli kabisa kwamba miradi mingi imejengewa lakini imekuwa na matatizo kwamba inalimwa mara moja tu, kipindi cha masika, baada ya hapo kilimo hakuna, kunakuwa hakuna maana. Ndiyo maana mpango huu unaoendelea wa mwaka 2002 kupitia miradi yote ya umwagiliaji kubaini shida ni nini ndipo tutagundua kwamba kumbe skimu zilijengwa lakini hazina maji kwa hiyo tuna mpango wa kujenga mabwawa. Lakini tusubiri ripoti ya wahandisi washauri, watakapokuwa wameikamilisha ndipo tutaendelea sasa kurekebisha mapungufu yote ili miradi hii iweze kufanya kwa uwezo mkubwa ule unaotarajiwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mtulia swali la nyongeza.

MHE. MAULID SAID A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokanana taarifa zilizotolewa na *TMA* wameeleza kwamba baadhi ya mikoa yetu katika Tanzania itapata chini ya wastani wa kiwango cha mvua, kwa maana ya Pwani, Tanga, Zanzibar na Morogoro Kaskazini. Je, Serikali ina mpango gani kukabiliana na tatizo litakalotokana na upungufu huo wa mvua?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Serikali yetu kwa kushirikiana na wataalam mbalimbali duniani tunaanza kuandaa miradi ambayo itakuwa na *efficiency* kubwa kwa maana ya kutumia maji kidogo kwenye uzalishaji wa mimea. Teknolojia hiyo tunazidi kuichukua na kuiendeleza ili maji kidogo yanayopatikana yawefe kutumika vizuri na uzalishaji uwe mkubwa. Kwa hiyo, tumejiandaa, taarifa ya *TMA* tunayo na sisi tunaendelea kuifanya kazi ili kuhakikisha kwamba *production* ya mazao hasa ya chakula itaendelea kuwa kama ambavyo matarajio yapo.

NAIBU SPIKA: Swali la mwisho Mheshimiwa Venance Mwamoto.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la maji kwenye Wilaya ya Kilolo ni kubwa na kwa kuwa Wilaya ya Kilolo ina utajiri mkubwa wa mito na vyanzo vya maji; na kwa kuwa tayari kuna utekelezaji mkubwa wa mradi wa maji ambaao uliahidiwa na Mheshimiwa Rais ambaao Wizara hii inafanya; je, kwa maeneo yale mengine ambayo tumekuwa tukipigia kelele kwa mfano Ruaha Mbunyuni, Wambingeto na sehemu nyingine, Waziri anasemaje? Ni pamoja na kuja kutembelea miradi hiyo ambacho ndicho kilio cha muda mrefu cha wananchi; Serikali inasemaje?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa Jimbo lake ni mionganini mwa Majimbo ambayo yaliahidhiwa kupata msaada kutoka Austria. Mpango huo unaendelea lakini kwa kuona kwamba unachelewa, sasa tumeanza utekelezaji kwa kutumia fedha za ndani. Mfano, llula sasa hivi tumepata chanzo cha maji kizuri kutoka Mkombozi na mradi umeanza ambaao unatekelezwa na Mamlaka yetu ya Maji ya Iringa (*IRUWASA*) na pale ni kilometra 14, kilometra mbili zinatikelezwa na tutakuongezea shilingi bilioni tano kuhakikisha kwamba sasa maji yanafika mpaka Mji wa Ilula; na mipango mingine yote uliyoomba Mheshimiwa Mbunge tunaifanyia kazi ikiwemo Ruaha Mbuyuni, lakini pamoja na kuchukua maji Mto Mtitu kupeleka kwenye Makao Makuu ya Wilaya pale Kilolo, tunaendelea kuifanyia kazi.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumeufika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu, tutaendelea na ratiba yetu. Sasa nilete matangazo tuliyonayo asubuhi ya leo.

Tangazo la kwanza ni la wageni. Tunao wageni walioko Jukwaa la Spika na hawa ni wageni watano wa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ambaye ni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na hawa ni viongozi wa Idara na Taasisi za Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Meja Jeneralii Mstaafu Projest Rwegasira, karibuni sana

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Ester Michael Mmasi ambaao wanatoka katika Taasisi binafsi inayojishughulisha na masuala ya TEHAMA vyuo vikuu na hawa ni ndugu Dossi Said Dossi na ndugu John Sarita. Karibuni sana

Tunao pia wageni walotembela Bunge kwa ajili ya mafunzo na kundi la kwanza ni wanafunzi 45 na walimu watano kutoka shule ya sekondari Kihesa iliyo kwa Mkoaa wa Iringa wakiongozwa na Mwalimu Pius Mwachuvaka, karibuni sana.

Tunao pia vijana 60 kutoka Kanisa la *Redeem Assemblies of God Tanzania* la Mkoani Dodoma, karibuni sana wageni wetu. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge tangazo lingine ni kuhusu kukaimu nafasi ya Mkuu wa shughuli za Serikali Bungeni. Mheshimiwa Spika ametaarifiwa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu amesafiri kuelekea Dar es Salaam kwa ajili ya shughuli za kikazi kuanzia jana na kwa hivyo kuanzia leo atakayekuwa anakaimu nafasi hiyo ni Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tunaendelea na ratiba tuliyonayo.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Susan Kiwanga naomba ukae *Chief Whip* wako amesimama, naomba ukae Mheshimiwa Susan Kiwanga. Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naomba kuomba mwongozo chini ya Kanuni ya 68(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu na Kanuni ninayoiombea mwongozo ni kanuni ya 120(1), (2) na (3) na Kanuni ya 122 (1), (2) na (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Kamati mbili Teule za Bunge lako Tukufu zimewasilisha taarifa ya Kamati hizo kwa Waziri Mkuu na tunaambiwa hizo taarifa sasa zinawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Kamati Teule za Bunge hizo mbili zimeundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 120(1), (2) na (3) ya Kanuni za Kudumu na Wajumbe wake waliteuliwa na Mheshimiwa Spika kwa mujibu ya 120(4) ya Kanuni za

Kudumu; na kwa mujibu wa Kanuni ya 122 fasiri ya (1), (2) na (3) ya Kanuni za Kudumu, taarifa ya Kamati Teule za Bunge zilipaswa kuwasilishwa ndani ya ukumbi wa Bunge lako Tukufu na kujadiliwa na Bunge lako Tukufu kwa mujibu wa hiyo Kanuni ya 122(3) ya Kanuni za kudumu za Bunge hili

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mwongozo ninaoumba ni ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, tunaomba useme, uliambie Bunge hili Tukufu ni kwa utaratibu gani wa Kikanuni, taarifa mbili za Kamati Teule za Bunge zimewasilishwa kwa Waziri Mkuu badala ya kuwasilishwa kwa Bunge kama inayotakiwa na Kanuni za Kudumu za Bunge hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tunaomba utuongoze, ni lini sasa kama itawezekana ni lini sasa taarifa hizo mbili zitawasilishwa kwenye ukumbi huu wa Bunge ili zihadiliwe kwa mujibu wa Kanuni za Bunge hili. Nakushukuru. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nimeombwa muongozo na Mheshimiwa Tundu Lissu kwa kutumia kanuni ya 68(7). Katika maelezo yake anaomba mwongozo kuona kama Kanuni ya 120 (1), (2) na (3) na Kanuni ya 122(1), (2) na (3) na ametaja pia Kanuni ya 120(4)

Waheshimiwa Wabunge, katika maelezo yake ameeleza kuhusu tukio lilitokea jana ambapo ameomba mwongozo juu ya mambo mawili kwa yale yaliyotokea jana ambayo sina haja ya kuyaeleza lakini anaomba mwongozo; kwanza kwamba ni utaratibu gani wa kikanuni uliosababisha ama ulioruhusu taarifa za Kamati kupelekwa kwa Mheshimiwa Spika nje ya Bunge hapo na kisha Mheshimiwa Spika kumkabidhi taarifa hizo Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Na jambo la pili aliloliomba ili Bunge hili liweze kuongozwa, ameuliza ni lini taarifa hizo mbili zitaletwa sasa Bungeni ili Bunge liweze kujadili kwa mujibu wa Kanuni tulizonazo.

Waheshimiwa Wabunge, nitaeleza mambo mawili; jambo la kwanza; Kanuni ya 68(7), mwongozo unaombwa kwa jambo lillotokea Bungeni, sasa ili tuende vizuri nitaisoma hiyo fasili:-

"Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatorewa papo hapo au baadaye kadri atakavyoona inafaa."

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, jambo aliloliombea muongozo Mheshimiwa Tundu Lissu kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) halijatokea Bungeni mapema. Nimesema nitazungumza mambo mawili, jambo la pili, kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawa sawa; Waheshimiwa Wabunge, kanuni ya 120(1) inasema hivi:-

"Kamati teule inaweza kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalum, kwa hoja mahususi itakayotolewa na kuafikiwa."

Waheshimiwa Wabunge, masharti mengine ya kuhusu Kamati Teule yako kwenye Kanuni ya 121(1) inasema:-

"Kila Kamati teue itakuwa na Wajumbe wasiozidi watano."

Nimechangua machache ili kupunguza muda wa kuzungumza ili tuwezekuendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Ukisoma Kanuni ya 120 utagundua kwamba, Bunge hili hakuna mahali ambapo hoja ilitolea humu ndani ikaafikiwa kwamba sasa zinaundwa Tume ama inaundwa Kamati Teule ya Bunge. Kwa sababu hiyo ndiyo maana Mheshimiwa Spika yeye amechangua utaratibu alioona bora wa Kamati alizoiunda yeye na si zilizoundwa na Bunge. (Makof)

Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kidogo ili twende pamoja, maana hata waliouliza maswali naona na wenyewe wanazungumza.

Kwa hiyo, ikiwa zile Kamati alizoziuenda Mheshimiwa Spika, tunataka kusema zilikuwa ni Kamati Teule za Bunge hakuna ushahidi uliopo kwenye *Hansard* kuonyesha kwamba Bunge hili liliziunda hizo Kamati. Kamati ziliundwa na Mheshimiwa Spika na akaja kutangaza majina ya wale ambao watakuwepo kwenye hizo Kamati, hilo ni moja. (*Makofii*)

La pili, Waheshimiwa Wabunge ninyi mliwaona wale Waheshimiwa waliokuwa kwenye hizi Kamati mbili. Mheshimiwa Spika asingeweza kuzidisha Wajumbe wa Kamati Teule kwa kiasi kile ambacho tumewaona, kwa hivyo Kanuni ya 121 ingekuwa imevunjwa kitu ambacho hakijafanywa. Kwa hiyo, pamoja na kwamba jambo limetokea jana halitakiwi kutolewa mwongozo ndani ya Bunge hili, nimetoa hayo maelezo kwa sababu kumekuwa na upotoshaji hapa na pale. (*Makofii*)

Sasa kuhusu haya mambo ambayo Mheshimiwa Tundu Lissu ameyaomba, naomba tu Waheshimiwa Wabunge tujue kwamba hata katika mazingira yale ambayo Kamati inazo taarifa ambazo inataka kuishauri Serikali, ukisoma Kanuni ya 117 tuko pamoja naamini; Kanuni ya 117(17) itakupa maelekezo kwamba Mheshimiwa Spika anaweza kuiambia Seriakli juu ya yale mapendekezo ya Kamati mahususi kwahiyio tuelewane hilo na likae vizuri namna hiyo. Kamati zimeundwa na Mheshimiwa Spika, Bunge hili halijawahi kuhojiwa wala hoja haijawahi kuletwa iliofikiwa ili Kamati hizo mbili ziundwe, ni Mheshimiwa Spika aliziuenda. (*Makofii*)

Baada ya Mwongozo huo Waheshimiwa Wabunge sasa tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

NAIBU SPIKA: Naomba ukae Mheshimiwa Mwakajoka. Katibu.

NDG. CHARLES MLOKA-KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Malawi (*The Convention on the Establishment of the Joint Songwe River Basin Commission between the government of united republic of Tanzania and the Government of Republic of Malawi*)

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba kuwasilisha mapendekezo ya Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuanisha Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mta Songwe kati ya Tanzania na Malawi (*Convention on the Establishment of the Joint Songwe River Basin Commission between Tanzania and Malawi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi; Mta Songwe ni rasilimali ya maji shirikishi na unafanya mpaka kati ya Tanzania na Malawi katika ukanda wa chini umbali wa kilometra 200 kutoka mto unapoingia katika Ziwa Nyasa. Bonde la mto huo lina kilometra za mraba 4,243 na wakazi wapatao 341,104. Eneo hilo linajumuisha maeneo ya Wilaya ya Kyela, Ileje, Mbozi, Mbeya Vijiji na Momba nchini Tanzania na Wilaya za Kitipa na Karonga nchini Malawi.

Eneo la uwanda wa chini wa bonde hilo limekuwa likikabiliwa na mafuriko ya mara kwa mara. Mafuriko yamekuwa yakisababisha mkondo wa mto kuhamahama na kusababisha mpaka wa nchi ya Tanzania na Malawi kuhamia kila mafuriko yanapotokea. Kutokana na hali hiyo, wakazi wa eneo hilo hujikuta wapo katika eneo la nchi nyingine kila mkondo wa mto unapohama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubadilika kwa mpaka mara kwa mara kunaweza kusababisha mgogoro wa mpaka katika Tanzania na Malawi kwenye eneo husika na kuathiri muskabali wa usalama katika nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto za mafuriko na kuhama hama kwa mkondo wa mto kuanzia mwaka 1976, Serikali za Tanzania na Malawi zimekuwa zikifanya mazungumzo katika ngazi mbalimbali kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizo. Mwaka 1991 Serikali hizo zilisaini makubaliano ya ushirikiano kwenye masuala mbalimabli (*General Corporation Agreement*) ya kutatua matatizo yanayozikabili nchi zote mbili. Katika kutekeleza makubaliano hayo, mwaka 2001 hado 2003 nchi hizo zilitkeleza mradi wa kudhibiti mkondo wa Mto Songwe (*The Stabilization of the Course of the Songwe River Project*) ambaao ulihusu upembuzi yakini, lengo likiwa ni kubaini njia bora ya kiufundi ya kuimarisha kingo za Mto Songwe na kupata suluhisho la mpaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya upembuzi huo yalibaini kuwa mafuriko yanayosababisha kuhama hama kwa mkondo wa mto Songwe yanaweza kudhibitiwa kwa Kujenga Mabwawa makubwa matatu ya Songwe Chini, Songwe Kati na Songwe Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hiyo pia ingewezesha kutumia rasilimali ya maji kwenye Mabwawa hayo, kuendeleza fursa nyingine zilizopo kwa faida za kijamii na kiuchumi kama vile uzalishaji wa umeme, umwagiliaji, uvuvi, utalii na kadhalika. Kwa hiyo lengo kuu la uimarishaji wa kingo za mto liliirejewa na kujumuisha uboreshaji wa hali ya kijamii na kiuchumi ya wakazi wa bonde hilo kwa kutumia rasilimali zake. Hivyo kuititia upembuzi huo iliamuliwa kuanzishwa kwa programu ya kuendeleza bonde la Mto Songwe (*Songwe River Basin Development Program*).

Mheshimiwa Naibu Spika, program hiyo imegawanywa katika awamu tatu na kutekelezwa kuititia hati ya makubaliano baina ya nchi hizo mbili. Awamu ya

kwanza ilihu upembuzi yakinifu 2001-2003, awamu ya pili ilihu usanifu wa kina na maandalizi ya miradia ya uwekezaji 2012 - 2013.

Awamu ya tatu inahu utekelezaji wa miradi 2016-2026 ambapo utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa Bwawa la Songwe Chini litakalojumuisha miundombinu ya uzalishaji umeme na umwagiliaji, shughuli za uvuvi na utalii pamoja na miradi ya kuboresha huduma za kijamii kama vile maji, shule, hospitali na barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha pande zote mbili zinanufaika na rasilimali za Bonde la Mto Songwe, nchi za Tanzania na Malawi zimeamua kuanzisha Kamisheni ya pamoja ya kuendeleza Bonde la Mto Songwe (*Joint Songwe River Basin Commission*) itakayosimamia na kuendeleza rasilimali za bonde hilo pamoja na kutekeleza miradi iliyoibuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa vyombo mbalimbali vyta ushirikiano katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji shirikishi unatekelezwa kuititia mkataba na itifaki zinazoridhiwa na nchi washirika kama ilivyoelekezwa kuititia Itifaki ya Maji ya Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC Revised Protocol on shared water causes 2000* kifungu cha 53 ambayo ni *shared water cause institutions*.

Mheshimiwa Naibu Spika, itifaki hiyo inaelekeza nchi zinazopaka kwenye bonde moja lenye maji shirikishi kuanzisha taasisi za ushirikiano kama vile Kamisheni za Maji, Mamlaka za Maji na Bodi za Maji kwa lengo la kuendeleza kutumia na kuhifadhi rasilimali za maji katika bonde husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitidha itifaki hiyo ya *SADC* mwezi Agosti, 2003. Vilevile Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 kipengele cha 2.12 na Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 kifungu 9(d) zinaelekeza na kuipa mamlaka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushirikiana

na nchi nyingine katika umiliki, utunzaji na matumizi ya rasilimali ya maji shirkishi kwa manufaa ya nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maadhumuni ya azimio hili ni kuwasilisha Bungeni mapendekezo ya kuridhia mkataba wa kuanzishwa kwa Kamisheni ya Pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Malawi kwa ajili ya kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji katika Bonde la Mto Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipengele muhimu vya mkataba; mkataba una jumla ya vipengele 20. Baadhi ya vifungu ni pamoja na vifuatavyo. Kifungu cha tatu; madhumuni na msingi ya kamisheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni; kwanza itauwa kutoa ushauri kwa pande zote mbili kuhusu usimamizi, uhifadhi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali za maji kwenye bonde.

Pili, kuainisha maeneo ya ushirikiano katika usimamizi na uendelezaji wa pamoja wa rasilimali za maji (*intergrated water resources management and development*) na kuyajumuisha kwenye Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa na Wilaya inayohusu bonde.

Tatu; kuratibu na kutekeleza mipango ya maendeleo iliyochini ya Programu ya Kuendeleza Bonde la Mto Songwe, usimamizi wa miundombinu ikijumuisha mabwawa, mitambo ya kuzalisha umeme, mifumo ya umwagiliaji na miundombinu ya kutoa huduma za kijamii kwa nchi zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Misingi ya Kamisheni. Kwanza ni ushirikiano unaozingatia uhuru, usawa na heshima kwa nchi husika na mipaka yake.

Pili, maendeleo endelevu, usawa na matumizi sahihi ya rasilimali za maji za pamoja kwenye bonde hususan Mto Songwe na vijito vingine vinavyoingiza maji kwenye mto huo.

Tatu, kuchukua tahadhari na kuzuia madhara yanayoweza kujitokeza na usawa wa uwiano katika masuala yote yanayohusu ushirikiano katika bonde la Mto Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha tano; Mamlaka na Majukumu ya Kamisheni; kwanza itakuwa kusaidia kukusanya na kuchakata taarifa muhimu zinazohitajika kuhusu bonde kwa ajili ya kutoa ushauri kwa pande zote na kutekeleza jukumu lolote litakalotekelawa na nchi zote mbili au kufanya maamuzi yanayohusu suala husika endapo itakuwa imeridhiwa, kutoa ushauri na mapendekezo kwa pande zote kuhusu suala lenye maslahi ya pamoja, tatu, kuunda Kamati mbalimbali na vikosi kazi vitakavyopewa majukumu ya kusimamia rasilimali za maji na rasilimali nyingine za bonde kulingana na mahitaji ya kamisheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne; kuajiri wataalam washauri, wakandarasi na watoa huduma kulingana na mahitaji na tano, kuandaa kanuni na taratibu za kamisheni kulingana na madhumuni na misingi ya mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 12 ni masuala ya fedha; Kamisheni itagharamia ushiriki wa wajumbe kutoka pande zote kwenye mikutano inayohusu shughuli za kamisheni kwa fedha zinazotokana na michango ya nchi washirika au mapato kutoka kwa vyanzo vya kamisheni. Aidha, kamisheni itagharamia ushiriki wa wajumbe wengine watakaoalikwa katika vikao vya kamisheni kwa ajili ya kutoa ushauri wa kitaalam kama itakavyokubalika na pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia gharama nyingine na madeni yatokanayo na utekelezaji wa majukumu ya kamisheni yatalipwa kwa usawa na pande zote isipokuwa kama itakubalika kulipa kuitia michango ya nchi washirika na mapato ya kamisheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 13 ni usuluhishi wa migogoro. Kwanza mgogoro wowote utakaojitekeza kati ya pande hizo mbili kuhusiana na tafsiri au utekelezaji

wa mkataba utatatuliwa kwa njia ya maelewano ya amani. Pili, endapo nchi zitashindwa kutatua mgogoro ndani ya siku 90, upande wowote ustaomba msaada wa usuluhishi kutoka kwa taasisi au mtu yejete atakayekubalika na pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, endapo usuluhishi utashindikana pande zote zitawasilisha suala husika kwa maandishi kwenye Baraza la Usuluhishi la SADC au kwa maamuzi (*Adhoc Arbitrator*) kwa makubaliano maalum ya pamoja. Maamuzi ya mwamuzi huyo yatakuwa ya mwisho na pande zote zitawajibika kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya kuridhia mkataba; kuridhiwa kwa mkataba huo kutawezesha kuanzishwa kwa kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe itakayosimamia na kuendeleza rasilimali za maji katika bonde hilo ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

i. Kutekeleza mradi wa ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya kudhibiti mafuriko ambayo huharibu kingo za mto na kusababisha mkondo wa mto kuhama na kuathiri mpaka wa nchi hizo mbili.

ii. Kuanza ujenzi wa mradi wa bwawa Songwe chini litakalotumika kuzalisha umeme megawati 180.2, kutoa huduma za maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, viwandani, kilimo cha umwagiliaji, uvuvi, hifadhi ya mazingira na utalii na hivyo kuongeza fursa za kiuchumi na kuboresha hali ya maisha ya wakazi wa eneo la bonde.

iii. Kuwa na chombo madhubuti kitakachowea, pamoja na kazi nyingine, kutafuta rasilimali fedha kwa niaba ya nchi husika kwa ajili ya kutekeleza miradi itakayokusudiwa katika bonde.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuridhiwa kwa mkataba huu kutakuwa na faida mbalimbali kwenye sekta nyingine kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kisiasa; ulinzi na usalama, wananchi wa eneo husika watakuwa na makazi ya kudumu katika nchi zao na kuepuka kuhamahama nchi nyingine bila hiari yao. Vile vile ulinzi na usalama mpakani utaimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiuchumi; fursa za kiuchumi zitapatikana kutokana na upatikanaji wa umeme utakaowezesha uanzishwaji wa viwanda vyta kusindika mazao ya kilimo na uvuvi. Vilevile ujenzi wa mabwawa na hifadhi ya mazingira utaongezeka, vivutio kwa utalii na kuboresha kilimo na hivyo kuongeza mapato kwa wakazi wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiteknolojia; upatikanaji wa umeme utachochea matumizi ya teknolojia mbalimbali za uzalishaji viwandani na kilimo cha umwagiliaji pamoja na kuimarika kwa huduma za mawasilliano kama vile simu na *computer*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne ni kimazingira; ujenzi wa mabwawa utazuia mafuriko ambayo huharibu mazingira vile vile miradi ya kuhifadhi mazingira kwenye bonde itasaidia kurudisha uoto wa asili, kuzuia mmomonyoko wa udongo na kuhifadhi rasilimali za maji kwa matumizi endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano ni huduma za kijamii; uboreshaji wa huduma za jamii hususan maji, afya na umeme utawapunguzia wanawake muda wanaotumia kutafuta huduma hizo na kutumia muda huo katika shughuli nyingine za uzalishaji na hivyo kuongeza kipato cha familia. Vilevile uboreshaji wa huduma hizo utaongeza mahudhurio ya wanafunzi mashulenii. Kiutamaduni, wakazi wa bonde wataishi bila wasiwasi wa kuathiriwa na mafuriko na hivyo kuendelea kuenzi tamaduni, mila na desturi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuridhia; kifungu cha 15 cha mkataba kinaelekeza kwamba mkataba huo utakuwa na nguvu za kisheria baada ya nchi zote wanachama kuridhia kwa mujibu wa taratibu za Katiba za nchi zao hivyo Tanzania inahitaji kuridhia mkataba huo kama

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inavyoelekeza katika Ibara ya 63(3)(e).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu gharama za kuridhia; katika utekelezaji wa awamu ya tatu ya programu ni ya miaka kumi inayotarajiwa kugharimu jumla ya dola za Marekani milioni mia nane ishirini na tisa ambazo zitatumika kutekeleza miradi iliyosanifiwa katika awamu ya pili. Fedha hizo zinatarajiwa kupatikana kuititia vyanzo vifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, michango kutoka nchi wanachama, mikopo ya masharti nafuu na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo na taasisi za fedha na za kimataifa na uwekezaji wa hisa kutoka Sekta Binafsi.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ya Maji na Umwagiliaji imetenga kiasi cha shilingi milioni mia saba na nane kwa ajili ya kulipa madeni, kuratibu maandalizi ya miradi ya kijamii na mazingira na kuendesha Sekretarieti ya Pamoja ya Mpito ya Kamisheni ya Bonde la mto Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kongamano la wawekezaji la kujadili upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi ilifanyika mwezi Mei, 2017 nchini Malawi, wengi wa wawekezaji hao walionesha nia ya kushiriki kwenye utekelezaji wa miradi inayotarajiwa kutekelezwa katika awamu ya tatu na wanasubiri mtaalam maalum (*transaction advisor*) aa jiriwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuundwa kwa kamisheni gharama za kuchangia kwa kila nchi husika zitabainishwa. Gharama hizo zitahusu kwanza, mchango wa kila mwaka utakaotolewa na kila nchi kwa ajili ya uendeshaji wa kamisheni, pili, mahitaji ya fedha kwa ajili ya miradi itakayotekelawa na tatu gharama nyingine kama zitakavyoridhiwa na pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikishwaji wa Wadau. Katika kuandaa azimio hili la Bunge Wizara imeshirikisha wadau wafuatao:-

Kamati za Kudumu za Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Nishati na Madini; Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; Sheria na Mambo ya Katiba; Fedha na Mipango; Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Maliasili na Utalii; Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi; Elimu, Sayansi na Teknolojia; Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Watoto; Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Mambo ya Ndani ya Nchi na Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Nailbu Spika, taasisi zinazoshirikishwa ni pamoja na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira; Tume ya Taifa ya Umwagiliaji; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Taasisi Zisizokuwa za Serikali ambazo n *Tanzania Country Water Partnership* na *TAWASANET*. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mikoa ya Mbeya na Songwe pamoja na Halmashauri za Kyela, Mbeya Vijijini, Ileje, Mbozi na Momba zimeshirikishwa kwa kutoa maoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ratiba ya utekelezaji; kifungu cha 15 cha mkataba kinaelekeza kwamba mkataba utakuwa na nguvu ya kisheria siku 30 baada ya nchi zote mbili kuridhia na kupeana taarifa kwa maandishi kuhusu hatua hiyo, hivyo utekelezaji wa mkataba utaanza baada ya pande zote mbili kuridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba sasa niwasilishe Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Maji ya Pamoja ya Bonde la Mtou Songwe kati ya Tanzania na Malawi kama ifuatavyo:-

Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Malawi

KWA KUWA Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*);

NA KWA KUWA Tanzania ni moja ya nchi zilizoridhia mkataba wa *SADC* na Itifaki ya Maji za Nchi za *SADC* inayoelekeza uanzishwaji wa vyombo vyaa ushirikiano katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji;

NA KWA KUWA, Tanzania na Malawi zilishiriki katika majadiliano ya pamoja yaliyofanyika mwaka 1976 kuhusu namna ya kutatua changamoto zinazosababishwa na mto Songwe kwa madhumuni ya kutafuta ufumbuzi wa kudumu;

NA KWA KUWA tarehe 20 Februari, 2004 Tanzania na Malawi zili-sign hati ya makubaliano (*MoU*) ambayo pamoja na mambo mengine ilitoa mamlaka kwa pande zote mbili kuanzisha kamisheni mbalimbali za pamoja ikijumuisha Kamisheni ya Pamoja na Bonde la Mto Songwe;

NA KWA KUWA Tanzania ilishiriki kikamilifu katika majadiliano yaliyowezesha kusainiwa kwa Mkataba wa Kimatalifa wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe na hatimaye kusaini mkataba huo katika Mji wa Lilongwe, nchini Malawi tarehe 18 Mei, 2017;

NA KWA KUWA Bonde la Mto Songwe ndilo linalofanya mpaka kati ya nchi ya Tanzania na Malawi na ambapo Wilaya za Kyela, Ileje, Mbozi, Mbeya Vijijini na momba nchini Tanzania zimo katika bonde hilo;

NA KWA KUWA Mto Songwe umekuwa ukifurika mara kwa mara na kusababisha uharibifu wa miundombinu, mali na mashamba na hivyo kuleta madhara, hasara na usumbufu mkubwa kwa wakazi wa bonde hilo;

NA KWA KUWA mafuriko ya Mto Songwe yamekuwa yakisababisha kuhamahama kwa mkondo wa mto na hivyo kusababisha kuhamahama kwa mpaka baina ya nchi ya Tanzania na Malawi na kusababisha wasiwasi wa kiusalama juu ya uwezekano wa kutokea mgogoro wa mipaka baina ya nchi hizi mbili;

NA KWA KUWA Tanzania na Malawi zinatekeleza mradi wa kudhibiti mkondo wa Mto Songwe ambao unapendekeza kujengwa kwa mabwawa makubwa matatu ambayo ni Songwe Chini, Songwe Kati na Songwe Juu kwa madhumuni ya kudhibiti mafuriko;

NA KWA KUWA Ibara ya 2.12 ya Sera ya Taifa ya Maji na kifungu cha 98 cha Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Sura 331 kwa pamoja zinaipa mamlaka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushirikiana na nchi nyingine katika umiliki, utunzaji na utumiaji wa pamoja wa rasilimali za maji kwa manufaa ya nchi;

NA KWA KUWA mkataba huu unalenga kuimarisha usimamizi, uhifadhi, uendelezaji, matumizi endelevu ya rasilimali ya maji ya Mto Songwe;

NA KWA KUWA Ibara ya 15 ya mkataba huu inaeleza kuwa mkataba huu pamoja na masharti mengine utaanza kutumika kwa kuzingatia matakwa ya kisheria ya kila nchi ambapo kwa nchi yetu ili mkataba wa Kimataifa uweze kutumika, pamoja na mambo mengine ni budi uridhiwe na Bunge;

NA KWA KUWA Tanzania kuweka saini ya kuridhia mkataba huu pamoja na kutekeleza itanufaika kisiasa, kiuchumi na kijamii ikijumuisha kutekeleza mradi wa ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya kudhibiti mafuriko ambayo yanakuwa yakiharibu kingo za mto na kusababisha mto kuhama hama na kuathiri mipaka ya nchi hizi mbili;

(b) Bwawa la Songwe Chini ambalo litajengwa baada ya kusainiwa mkataba huu litatumika kuzalisha

umeme wa megawati 180.2, kutoa huduma za maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, viwandani, kilimo cha umwagilajji, uvuvi, hifadhi ya mazingira na utalii na hivyo kuongeza fursa za kiuchumi na kuboresha hali ya maisha ya wakazi wa eneo la Bonde la Mto Songwe;

Na (c) ni kuhifadhi mazingira kurudisha uoto wa asili, kuzuia mmomonyoko wa udongo na kuhifadhi rasilimali za maji kwa matumizi endelevu.

HIVYO BASI kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na mkataba huu kwa Tanzania na umuhimu wa kuridhia mkataba huu, Bunge hili katika Mkutano wa Nane kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 linaazimia kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe (*Joint Songwe River Basin Commision*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(*Makofii*)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono, tutaendelea na utaratibu mwingine. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA - MAKAMU
MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**
Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Azimio la Bunge kuridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Tanzania na Malawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu

ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Tanzania na Malawi (*Convention on the Establishment of a Joint Songwe River Basin Commission between Tanzania and Malawi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyongeza ya Nane kifungu cha 7(1)(b) ya Kanuni za kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016 inazipa Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kilimo, Mifugo jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria, Maazimio na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazosimamia. Jukumu hili pia ni jukumu la Kikatiba chini ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane kifungu cha 6(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji inasimamia Wizara mbili ambazo zinashughulikia sekta za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Kanuni tajwa hapo juu, tarehe 31 Agosti, 2017 uliiletea Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kazi ya kuchambua mapendekezo ya Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Tanzania na Malawi kama yalivyowasilishwa na Serikali ili Kamati iweze kutoa maoni na ushauri kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe Kati ya Tanzania na Malawi liliwasilishwa mbele ya Kamati siku ya Jumatatu tarehe 4 Septemba, 2017 na Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa *Engineer Gerson Lwenge* (Mbunge).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 82(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016

inazitaka Kamati za Bunge zinapokuwa zinashughulikia Miswada ya Sheria, Maazimio na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ialike wadau ili kwa kutumia utaalamu wao waisaidie Kamati kuchambua na kuboresha maudhui yanayopendekezwa. Kufuatia ufinyu wa muda uliotolewa kushughulikia azimio husika, Kamati haikuweza kupata wadau wowote na hivyo kushindwa kutekeleza Kanuni hiyo ya Bunge. Hata hivyo, Kamati iliweza kutekeleza jukumu iliyopewa kwa niaba ya Bunge ilipitia na kuchambua azimio tajwa na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko, madhumuni na faida ya Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia fupi ya kuanza kwa Mkataba wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe; mchakato wa kuanzisha Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mta Songwe ulianza mwaka 1976 ambapo mwaka 2004 Tanzania na Malawi zilisaini Hati ya Makubaliano ambayo pamoja na mambo mengine hati hiyo ya makubaliano inazipa mamlaka nchi ya Tanzania na Malawi kuanzisha Kamisheni mbalimbali za pamoja, ikijumuisha Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mta Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia hati hiyo ya makubaliano, Tanzania ilishiriki kikamilifu katika majadiliano yaliyowezesha kusainiwa kwa Mkataba wa Kimataifa wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya Pamoja na Bonde la Mta Songwe na hatimae kusaini Mkataba huo katika Mji wa Lilongwe nchini Malawi tarehe 18 Mei, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Mkataba wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mta Songwe; dhumuni la msingi la kuanzishwa kwa Mkataba wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mta Songwe ni kuimarisha usimamizi, uhifadhi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali ya maji ya Mta Songwe. Kuanzishwa kwa mkataba huu ni muhimu kufuatia faida zitakazopatikana kwa nchi wanachama, kwani unalenga kuwezesha:-

(i) Kutekeleza mradi wa ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya kudhibiti mafuriko ambayo huaribu kingo za mto na kusababisha mkondo wa mto kuhama na kuathiri mpaka wa nchi hizi mbili.

(ii) Kuanza ujenzi wa mradi wa Bwawa la Songwe Chini litakalotumika kuzalisha wa umeme megawati 180.2, kutoa huduma ya maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, viwandani, kilimo cha umwagiliaji, uvuvi, hifadhi ya mazingira na utalii na hivyo kuongeza fursa za kiuchumi na kuboresha hali ya maisha ya wakazi wa eneo la Bonde.

(iii) Kuwa na chombo madhubuti kitakachowenza, pamoja na kazi zingine kutafuta rasilimali fedha kwa niaba ya nchi wanachama kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyokusudiwa katika Bonde la Mto Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na faida hizo za kiujumla, kuridhiwa kwa Mkataba huu kutakuwa na faida mbalimbali kwenye sekta nyingine kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kisiasa, ulinzi na usalama; eneo la uwanda wa chini wa Bonde la Mto Songwe limekuwa likikabiliwa na mafuriko ya mara kwa mara ambayo yamekuwa yakisababisha mkondo wa mto kuhamahama na kusababisha mpaka wa nchi za Tanzania na Malawi kuhama kila mafuriko yanapotokea. Hivyo kuridhiwa kwa Mkataba huu pamoja na mambo mengine kutasaidia kupata suluhisho la mpaka na kuwawezesha Wananchi wa eneo la mpakani kati ya Tanzania na Malawi kupata makazi ya kudumu katika nchi zao na kuepuka kuhamia nchi nyingine bila hiari yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiuchumi; kuridhiwa kwa mkataba huu kutawezesha ujenzi wa bwawa la Songwe Chini, ambalo mara baada ya kukamilika kwake litatumika kuzailisha umeme megawati 180.2 ambapo fursa za kiuchumi zitapatikana kutokana na umeme utakaowezesha uanzishwaji wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na uvuvi. Aidha, ujenzi wa mabwawa na hifadhi ya mazingira

utaongeza vivutio vya utalii na kuboresha kilimo na hivyo kuongeza kipato kwa wakazi wa eneo la Bonde na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za kijamii; ujenzi wa mabwawa na uzalishaji wa umeme utaboresha pia huduma za jamii kama vile upatika wa maji ya uhakika ambayo ni safi na salama, upatikanaji wa umeme wa uhakika na afya za jamii. Kuboreka kwa huduma hizi kutawasaidia wanawake kupunguza muda mrefu wanaotumia kutafuta huduma hizo na kuwawezesha kutumia muda huo kufanya shughuli zingine za uzalishaji na hivyo kuongeza kipato cha familia.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe. Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe una jumla ya vifungu 20.

Kamati ilipitia vifungu vyote, hata hivyo taarifa ya Kamati ninayoiwasilisha inataja kwa kifupi vifungu muhimu vilivyoko kwenye mkataba huu. Vifungu hivyo ni pamoja na:-

(i) Kifungu cha 3 kinahusu madhumuni na misingi ya Kamisheni.

(ii) Kifungu cha 5 kinafafanua kuhusu mamlaka na majukumu ya Kamisheni.

(iii) Kifungu cha 11 kinataja majukumu, wajibu na haki za msingi za kila nchi katika kutekeleza mkataba.

(iv) Kifungu cha 12 kinaelezea upatikanaji wa rasilimali fedha za kuendesha Kamisheni.

(v) Kifungu cha 13 kinafafanua jinsi ya kushughulikia utatuzi wa migogoro endapo itatokea.

(vi) Kifungu cha 16 kinahusu utaratibu wa nchi kujiondoa katika Mkataba.

(vii) Kifungu cha 17 kinahusu utaratibu utakaozingati na nchi katika kufanya marekebisho katika vifungu vya mkataba.

(viii) Kifungu cha 19 kinahusu sharti la kuzingatia usiri katika utekelezaji wa Mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati kufanya uchambuzi kwenye vifungu hivyo muhimu, Kamati ilitaka kujiridhisha kwenye maeneo ya msingi na hivyo kuhitaji ufanuzi kwenye maeneo hayo ambayo ni pamoja na:-

(i) Hatua iliyofikiwa kati ya Tanzania na Malawi katika kushuhulikia mgogoro wa mpaka wa Ziwa Nyasa ili kujiridhisha kuwa mgogoro uliokuwepo hauwezi kuathiri utekelezaji wa mkataba. Mantiki ya hoja hii nikutokana na ukweli kuwa uhai wa Ziwa Nyasa ni Mto Songwe, na ukweli kwamba Ziwa Nyasa lina umuhimu mkubwa kwenye uchumi wa Tanzania.

(ii) Ufanuzi kuhusu namna nchi itakavyonufaika na Ziwa Nyasa na Mto Songwe, na ni kwa kiasi gani utekelezaji wa Mkataba huu hautaathiri manufaa yaliyokuwa yakipatikana awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kiliarifu Bunge lako kuwa Kamati imeridhishwa na maelezo yaliyoko kwenye Mkataba huu pamoja na ufanuzi uliotolewa na Serikali kuhusu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati; baada ya kufanya uchambuzi wa Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Kwa kuwa uhai wa Ziwa Nyasa ni Mto Songwe, na kwa kuwa mkataba huu unahuisha nchi za Tanzania na Malawi ambazo zimekuwa na mgogoro wa mara kwa mara kuhusu mpaka wa Ziwa Nyasa, Kamati inaishauri Serikali kuchukua tahadhari na kuhakikisha utekelezaji wa

mkataba huu hautaathiri faida ambazo nchi imekuwa ikipata kutoka Ziwa Nyasa na Mto Songwe.

(ii) Kwa kuwa nchi ya Tanzania na Malawi zimekuwa na mgogoro wa mpaka wa Ziwa Nyasa kwa muda mrefu, na kwa kuwa uhai wa Ziwa Nyasa ni Mto Songwe; pamoja na kwamba mkataba huu unahu Mto Songwe, Kamati inaishauri Serikali kupitia fursa ya mkataba huu kufanya utambuzi wa mipaka ya Ziwa Nyasa hatua ambayo inaweza kumaliza kabisa tatizo la mgogoro wa mpaka wa Ziwa Nyasa.

(iii) Kwa kuwa Mkataba huu unahu isisha nchi mbili ni vyema baada ya kuridhiwa na Bunge, Serikali iharakishe utungwaji wa Sheria na Kanuni zake ili wananchi wa Tanzania waanze kunufaika na faida zilizoainishwa kwenye mkataba huu.

(iv) Baada ya nchi wanachama kuridhia utekelezaji wa Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe, elimu ya kutosha itolewe hususan kwa wananchi waishio maeneo yampaka wa Tanzania na Malawi kuhusu utunzaji wa mazingira kwenye eneo la Mto Songwe pamoja na kutumia vizuri faida zitakaopatikana kutokana na mkataba huu pamoja na kutoa elimu kuhusu mipaka ya nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Aidha, sina budi kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge kwa weledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii pia kumshukuru Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa *Engineer Gerson H. Lwenge* (Mbunge), pamoja na Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mheshimiwa *Engineer Isack A. Kamwelwe* (Mbunge), Katibu Mkuu Profesa Kitila Mkumbo na watendaji wa Wizara kwa ushirikiano walιoutoa wakati Kamati ilipokuwa inachambua na kujadili mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri ya kuupitia, kuuchambua na hatimaye kutoa maoni na ushauri wa Mkataba husika, naomba majina ya Wajumbe yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama yalivyoandikwa kwenye taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashillah, Katibu wa Bunge, kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati Ndugu Rachel Nyega, Ndugu Martha Chassama na Ndugu Virgil Mtui wakisaidiwa na Msaidizi wa Kamati Ndugu Mwimbe John kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsanteni kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO
MIFUGO NA MAJI KUHUSU AZIMIO LA BUNGE KURIDHIA
MKATABA WA KUANZISHA KAMISHENI YA PAMOJA YA
BONDE LA MTO SONGWE KATI YA TANZANIA NA MALAWI
(CONVENTION ON THE ESTABLISHMENT OF A JOINT SONGWE
RIVER BASIN COMMISSION BETWEEN TANZANIA AND
MALAWI) – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge kuridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe Kati ya Tanzania na Malawi (*Convention on The Establishment*

of a Joint Songwe River Basin Commission Between Tanzania and Malawi)

Mheshimiwa Spika, Nyongeza ya Nane Kifungu cha 7(1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, inazipa Kamati za kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge Kilimo, Mifugo na Maji, jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria, Maazimio na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia. Jukumu hili pia ni jukumu la Kikatiba chini ya Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane Kifungu cha 6 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji inasimamia Wizara mbili ambazo zinashughulikia sekta za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni tajwa hapo juu, tarehe 31 Agosti, 2017 uliiletea Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kazi ya kuchambua mapendekezo ya Azimio la Bunge kuridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Tanzania na Malawi (*Convention on The Establishment of a Joint Songwe River Basin Commission Between Tanzania and Malawi*), kama yalivyowasilishwa na Serikali ili Kamati iweze kutoa maoni na ushauri kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Azimio la Bunge kuridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe Kati ya Tanzania na Malawi (*Convention on The Establishment of a Joint Songwe River Basin Commission Between Tanzania and Malawi*), liliwasilishwa mbele ya Kamati siku ya Jumatatu tarehe 4 Septemba, 2017 na Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mhe. Eng. Gerson H. Lwenge, Mb.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 82(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inazitaka Kamati za Bunge zinapokuwa zinashughulikia Miswada ya Sheria, Maazimio na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na

Bunge ialike wadau ili kwa kutumia utaalamu wao waisaidie Kamati kuchambua na kuboresha maudhui yanayopendekezwa. Kufuatia ufinyu wa muda uliotolewa kushughulikia Azimio husika, Kamati haikuweza kupata wadau wowote na hivyo kushindwa kutekeleza kanuni hiyo ya Bunge. Hata hivyo, Kamati iliweza kutekeleza jukumu iliyopewa kwa niaba ya Bunge ilipitia na kuchambua Azimio tajwa na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

- 2.0 **CHIMBUKO, MADHUMUNI NA FAIDA YA MKATABA WA KUANZISHA KAMISHENI YA PAMOJA YA BONDE LA MTO SONGWE**
- 2.1 **Historia fupi ya kuanza kwa Mkataba wa Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe**

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuanzisha Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe ulianza Mwaka 1976, ambapo Mwaka 2004 Tanzania na Malawi zilisaini Hati ya Makubaliano ambayo pamoja na mambo mengine Hati hiyo ya Makubaliano inazipa mamlaka nchi ya Tanzania na Malawi kuanzisha Kamisheni mbalimbali za pamoja, ikijumuisha Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe.

Mheshimiwa Spika, kufuatia Hati hiyo ya Makubaliano, Tanzania ilishiriki kikamilifu katika majadiliano yaliyowezesha kusainiwa kwa Mkataba wa Kimataifa wa uanzishwaji wa Kamisheni ya pamoja na Bonde la Mta Songwe na hatimae kusaini Mkataba huo katika Mji wa Lilongwe nchini Malawi tarehe 18 Mei, 2017.

- 2.2 **Madhumuni ya Mkataba wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mta Songwe**

Mheshimiwa Spika, dhumuni la msingi la kuanzishwa kwa Mkataba wa Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mta Songwe ni kuimarisha usimamizi, uhifadhi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali ya maji ya Mta Songwe.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Mkataba huu ni muhimu kufuatia faida zitakazopatikana kwa nchi wananchama, kwani unalenga kuwezesha :-:

- i) Kutekeleza mradi wa ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya kudhibiti mafuriko ambayo huaribu kingo za mto na kusababisha mkondo wa mto kuhama na kuathiri mpaka wa nchi hizi mbili;
- ii) Kuanza ujenzi wa mradi wa Bwawa la Songwe Chini litakalotumika kuzalisha umeme (Megawati 180.2), k u t o a huduma ya maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, viwandani, kilimo cha umwagiliaji, uvuvi, hifadhi ya mazingira na utalii na hivyo kuongeza fursa za kiuchumi na kuboresha hali ya maisha ya wakazi wa eneo la Bonde; na
- iii) Kuwa na chombo madhubuti kitakachoweza, pamoja na kazi zingine, kutafuta rasilimali fedha kwa niaba ya nchi wanachama kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyokusudiwa katika Bonde la Mto Songwe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na faida hizo za kiujumla, kuridhiwa kwa Mkataba huu kutakuwa na faida mbalimbali kwenye sekta nyingine kama ifuatavyo:-

KISIASA, ULINZI NA USALAMA

Mheshimiwa Spika, eneo la uwanda wa chini wa Bonde la Mto Songwe limekuwa likikabiliwa na mafuriko ya mara kwa mara ambayo yamekuwa yakisababisha mkondo wa mto kuhamahama na kusababisha mpaka wa nchi za Tanzania na Malawi kuhama kila mafuriko yanapotokea. Hivyo kuridhiwa kwa Mkataba huu pamoja na mambo mengine kutasaidia kupata suluhisho la mpaka na kuwawezesha Wananchi wa eneo la mpakani kati ya Tanzania na Malawi kupata makazi ya kudumu katika nchi zao na kuepuka kuhamia nchi nyingine bila hiari yao.

KIUCHUMI

Mheshimiwa Spika, kuridhiwa kwa Mkataba huu kutawezesha ujenzi wa bwawa la Songwe Chini, ambalo mara baada ya kukamilika kwake litatumika kuzailisha umeme Megawati 180.2 ambapo fursa za kiuchumi zitapatikana kutohana na umeme utakaowezesha uanzishwaji wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na uvuvi. Aidha, ujenzi wa mabwawa na hifadhi ya mazingira utaongeza vivutio vya utalii na kuboresha kilimo na hivyo kuongeza kipato kwa wakazi wa eneo la Bonde na Taifa kwa ujumla.

HUDUMA ZA KIJAMII

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mabwawa na uzalishaji wa umeme utaboresha pia huduma za Jamii kama vile upatika wa maji ya uhakika ambayo ni safi na salama, upatikanaji wa umeme wa uhakika na afya za jamii. Kuboreka kwa huduma hizi kutawasaidia wanawake kupunguza muda mrefu wanaotumia kutafuta huduma hizo na kuwawezesha kutumia muda huo kufanya shughuli zingine za uzalishaji na hivyo kuongeza kipato cha familia.

3.0 UCHAMBUZI WA MKATABA WA KUANZISHA KAMISHENI YA PAMOJA YA BONDE LA MTO SONGWE

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe una jumla ya vifungu 20. Kamati ilipitia vifungu vyote, hata hivyo taarifa ya Kamati ninayoiwasilisha inataja kwa kifupi vifungu muhimu vilivyoko kwenye Mkataba huu. Vifungu hivyo ni pamoja na:-

- i) Kifungu cha 3; kinahusu Madhumuni na Msingi ya Kamisheni;
- ii) Kifungu cha 5; kinafafanua kuhusu Mamlaka na Majukumu ya Kamisheni;
- iii) Kifungu cha 11; kinataja majukumu, wajibu na haki za Msingi za kila nchi katika kutekeleza Mkataba;

- iv) Kifungu cha 12; kinaelezea upatikanaji wa rasilimali fedha za kuendesha Kamisheni;
- v) Kifungu cha 13; kinafafanua jinsi ya kushughulikia utatuzi wa migogoro endapo itatokea;
- vi) Kifungu cha 16; kinahusu utaratibu wa nchi kujiondoa katika Mkataba;
- vii) Kifungu cha 17; kinahusu utaratibu utakaozingatiwa na nchi katika kufanya marekebisho katika vifungu vya mkataba; na
- viii) Kifungu cha 19; kinahusu sharti la kuzingatia usiri katika utekelezaji wa Mkataba

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kufanya uchambuzi kwenye vifungu hivyo muhimu, Kamati ilitaka kujiridhisha kwenye maeneo ya msingi na hivyo kuhitaji ufanuzi kwenye maeneo hayo ambayo ni pamoja na:-

- i) Hatua iliyofikiwa kati ya Tanzaia na Malawi katika kushuhulikia mgogoro wa mpaka wa Ziwa Nyasa ili kujiridhisha kuwa mgogoro uliokuwepo hauwezi kuathiri utekelezaji wa Mkataba. Mantiki ya hoja hii ni kutokana na ukweli kuwa uhai wa Ziwa Nyasa ni Mto Songwe, na ukweli kwamba Ziwa Nyasa lina umuhimu mkubwa kwenye uchumi wa Tanzania.
- ii) Ufanuzi kuhusu namna nchi itakavyonufaika na Ziwa Nyasa na Mto Songwe, na ni kwa kiasi gani utekelezaji wa Mkataba huu hautaathiri manufaa yaliyokuwa yakipatikana awali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako kuwa Kamati imeridhishwa na maelezo yaliyoko kwenye Mkataba huu pamoja na ufanuzi uliotolewa na Serikali kuhusu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe.

4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya uchambuzi wa Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

- (i) Kwa kuwa uhai wa Ziwa Nyasa ni Mto Songwe,na kwa kuwa mkataba huu unahusisha nchi za Tanzania na Malawi ambazo zimekuwa na mgogoro wa mara kwa mara kuhusu mpaka wa Ziwa Nyasa, Kamati inaishauri Serikali kuchukuwa taadhari na kuhakikisha utekelezaji wa mkataba huu hautaathiri faida ambazo nchi imekuwa ikipata kutoka Ziwa Nyasa na Mto Songwe.
- (ii) Kwa kuwa nchi ya Tanzania na Malawi zimekuwa na mgogoro wa mpaka wa Ziwa Nyasa kwa muda mrefu, na kwa kuwa uhai wa Ziwa Nyasa ni Mto Songwe, pamoja na kwamba mkataba huu unahusu Mto Songwe, Kamati inaishauri Serikali kupitia fursa ya Mkataba huu kufanya utambuzi wa Mipaka ya Ziwa Nyasa hatua ambayo inaweza kumaliza kabisa tatizo la mgogoro wa mpaka wa Ziwa Nyasa.
- (iii) Kwa kuwa Mkataba huu unahusisha nchi mbili ni vyema baada ya kuridhiwa na Bunge, Serikali iharakishe utungwaji wa Sheria na Kanuni zake ili wananchi wa Tanzania waanze kunufaika na faida zilizoainishwa kwenye mkataba huu.
- (iv) Baada ya nchi wanachama kuridhia utekelezaji wa Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe, elimu ya kutosha itolewe hususan kwa wananchi waishio maeneo ya mpaka wa Tanzania na Malawi kuhusu utunzaji wa mazingira kwenye eneo la Mto Songwe pamoja na kutumia vizuri faida zitakaopatikana kutohana na mkataba huu pamoja na kutoa elimu kuhusu mipaka ya nchi hizo.

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati.

Aidha, sina budi kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge kwa weledi.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii pia kumshukuru Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Eng. Gerson H. Lwenge, Mb pamoja na Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mhe. Eng. Isack A. Kamwele, Mb, Katibu Mkuu Dkt. Kitila Mkumbo na Watendaji wa Wizara kwa ushirikiano alioutoa wakati Kamati ilipokuwa inachambua na kujadili Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri ya kuupitia, kuuchambua na hatimaye kutoa maoni na ushauri wa Mkataba husika, naomba majina ya Wajumbe yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama yalivyoorodheshwa hapa chini.

1. Mhe. Dkt. Michael M. Nagu, Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma, Mb M/Mwenyekiti
3. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb Mjumbe
4. Mhe. Mahmoud H. Mgimwa, Mb "
5. Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb "
6. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb "
7. Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb "
8. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb "
9. Mhe. Mattar Ali Salum, Mb "
10. Mhe. John John Mnyika, Mb "
11. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb "
12. Mhe. James Kinyasi Millya, Mb "
13. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb "
14. Mhe. Pascal Yohana Haonga, Mb "
15. Mhe. Salim Mbaraku Bawazir Mb "
16. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb "
17. Mhe. Abdallah Hamis Ulega, Mb "
18. Mhe. Haji Ameir Haji, Mb "
19. Mhe. Daniel N. Nsanzugwanko, Mb "
20. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb "
21. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb "
22. Mhe. Emmanuel Papian John, Mb "

- | | | |
|-----|-------------------------------|---|
| 23. | Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb | " |
| 24. | Mhe. Oliver Daniel Semuguruka | " |

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashillah - Katibu wa Bunge, kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati Ndg. Rachel Nyega, Ndg. Martha Chassama na Ndg. Virgil Mtui wakisaidiwa na Msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati .

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Hoja.

Dkt. Christine Ishengoma, Mb
M/MWENYEKITI,
KAMATI YA KUDUMU YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI
7 SEPTEMBER, 2017

NAIBU SPIKA: Sasa tutamsikia msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, kwenye Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

MHE. HAMIDU H. BOBALI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha kwa ufupi sana maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, Kuhusu Azimio Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Sonngwe kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Malawi (*The Convention on the Establishment of a Joint Songwe River Basin Commission Between the Government of The United Republic of Tanzania And The Government of The Republic of Malawi*) yanayotolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na

afya nzuri inayoniwezesha kusimama mbele ya ukumbi huu na kuweza kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusiana na azimio hili. Aidha, nitoe shukrani kwa wananchi na wanachama wote wa Chama cha Wananchi (CUF) kwa imani yao kwangu na kwa chama chetu katika kuhakikisha kuwa tunapambana kwa nguvu zote ili kushinda nguvu za aina yoyote kutoka nje ya chama chetu zinazokusudia kukidhuru na kukihujumu chama chetu kilichobeba matumaini ya Watanzania wapenda mabadiliko na demokrasia ndani ya ushirikiano madhubuti ujulikanao kama UKAWA. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa si mwangi wa fadhila kama sita mshukuru Naibu wangu, Mheshimiwa Peter Ambrose Lijualikali kwa msaada wake katika maandalizi ya maoni haya. Sambamba na hili niwashukuru waheshimiwa wajumbe wenzangu wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo, Maji na Uvuvi kwa ushirikiano mkubwa tulionao ndani ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa utangulizi huo, naomba kuelezea baadhi ya mambo ambayo kwa mtazamo wetu tumeona yanahitaji kupatiwa maelezo ya kina na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Azimio la Bunge linavyosema kwamba Bonde la Mto Songwe ndilo linalofanya mpaka kati ya Tanzania na nchi ya Malawi na Wilaya za Kyela, Ilaje, Mbozi Mbeya Vijiji na Momba zimo ndani ya Bonde hilo. Kutokana na ukweli kwamba mto huo umekuwa ukihama hama na hivyo kusababisha mpaka baina ya nchi hizi nao kuhama hama jambo ambalo linaweza kusababisha mtafaruku na jirani zetu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Mheshimiwa Waziri aliyoleta kwenye kamati inaonesha kuwa Tanzania na Malawi zinatekeleza Mradi wa Kudhibiti Mkondo wa Mto Songwe (*Stabilization of the Course of Songwe River Project*) kwa kujenga Bwawa la Songwe Chini ambalo litajengwa baada ya kusainiwa Mkataba huu na bwawa hilo litatumika kuzalisha umeme wa Megawati 180.2, kutoa huduma ya maji

kwa ajili ya matumizi ya majumbani, viwandani, kilimo cha umwagiliaji, uvuvi, hifadhi ya mazingira na utalii na hivyo kuongeza fursa za kiuchumi na kuboresha hali za maisha ya wakazi wa eneo la Bonde la Mto Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo hayo niliyosoma yameelezwa kwenye Ibara ya 8 ya mkataba kuwa ni baadhi ya kazi za Kamati ambayo inaundwa chini ya Ibara ya Nne ya Mkataba. Kazi hizo za Kamati kama ilivyoundwa chini ya ibara tajwa zitatekelezwa na kusi mamiwa na sekretarieti inayoanzishwa na Ibara ya nne. Ibara ya Tisa inaainisha majukumu ya Sekretariat, pamoja na majukumu mengine Ibara ya 9(6)(g) kinasema kwamba:-

"Manage on daily basis the construction, operation and maintenance of all infrastructure under Songwe River Basin Development Programme, including flood warning, hydropower, irrigation systems and operation of the dam; social infrastructure and regularly obtain, update and exchange information and data as necessary, including the development and use of decision support system."

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hicho kinaonesha kuwa kazi hizo zote zinatakiwa zifanywe na sekretarieti, lakini tukumbuke kwamba ustawi wa wananchi katika wilaya husika utakuwepo kama wananchi mmoja mmoja au kwa vikundi vyao au kampuni zao (*local content*) watanufalka kwa kuwa wamiliki katika miradi itakayoanzishwa na Kamisheni hiyo. Sambamba na hilo ni kwamba, ushiriki huo wa wananchi utawezekana kwa sheria yetu ya PPP kati ya Kamisheni na wananchi (sekta binafsi).

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa Ibara ya 18 inaongelea mawanda ya mkataba ni kwamba washirika wa mkataba wanaweza kuingia mkataba baina au ya kimataifa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi au programu zitakazotakiwa kutekelezwa na Kamisheni. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema bado Ibara hiyo haijatoa uhakika wa ushiriki wa wanufaikaji katika kumiliki na kutekeleza miradi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kwamba, miradi mingi ambayo ilianzishwa na Serikali kwa ufadhili kwa ajili ya wananchi imekufa kutokana na kutokuwepo kwa dhana ya umiliki kutoka upande wa wanufaikaji, wananchi. Tukumbuke kwamba, watangulizi wa Serikali hii ya Awamu ya Tano waliliona hilo na ndio sababu ya ubinafsishaji japokuwa kutokfanya vizuri kwa ubinafsishaji haikuwa ni dhana hiyo, bali utekelezaji wake. Kushindwa kwake kulitokana na ulegele na kutowajibika ipasavyo kwa wahusika walikuwa wasimamizi wa zoezi hilo la ubinafsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kwamba, kwa kuwa, moja ya lengo la uundwaji wa Kamisheni hii ni utumiaji endelevu (*sustainable*) wa rasilimali ya maji kwa wananchi wa Wilaya tajwa hapo awali, hivyo basi ni lazima ushiriki wa wananchi uonekane wazi kwenye mkataba huu ili sheria zetu za utekelezaji zitakapotungwa *domestication*, vipengele vya uhusishwaji wa wananchi kwenye maeneo tajwa uakisiwe kwenye sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinyume cha hapo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba, Kamisheni hii na malengo yake hayatakuwa na manufaa kwa maendeleo ya wananchi hasa wa maeneo husika, bali itakuwa kama mamlaka ya uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji ambalo badala ya kuwa mkombozi au mleta kicheko kwa wananchi wa maeneo husika imekuwa ndio mleta kilio kwa wananchi na hivyo, Taifa kuendelea kubaki kuwa mtazamaji tu wa rasilimali hiyo adhimu, bila kunufaika nayo. Serikali kuacha kulifanya kazi stahiki Bonde la Mto Rufiji ni muendelezo wa kutotumia vizuri rasilimali zetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kabisa kuwa hii Kamisheni sio kama itajikita kwenye maji tu, bali ni kweli ardhi ambayo wakulima wengi wanaendesha shughuli za maisha yao ya kila siku. Kwa maana hiyo, basi ni muhimu Mheshimiwa Waziri akaweka wazi kuhusiana na mfumo mzima wa vibali vya matumizi ya ardhi hiyo ambayo imo ndani ya himaya ya Kamisheni. Kwa maana nyingine ni kwamba, maisha ya wananchi wa Wilaya husika yataathirika kwa kiwango

kikubwa sana. Jambo hilo pia, lifanywe kwa kuzingatia suala zima la usalama wa Taifa letu. Kamisheni ni vema pia, ikahusisha Idara zetu zinazohusika na ulinzi na usalama wa Taifa kwani isije ikatumika kama ndio ufunguaji wa mipaka yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya mafupi, Kambi Rasmi ya Upinzani haioni sababu ya kutokuridhia Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa kwa Kamisheni hii ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.
(Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU AZIMIO LA KURIDHIA MKATABA WA UANZISHWAJI WA KAMISHENI YA PAMOJA YA BONDE LA MTO SONGWE KATI YA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NA SERIKALI YA JAMHURI YA MALAWI (*CONVENTION ON THE ESTABLISHMENT OF A JOINT SONGWE RIVER BASIN COMMISSION BETWEEN THE GOVERNMENT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA AND THE GOVERNMENT OF THE REPUBLIC OF MALAWI*) –
KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

“Yanatolewa kwa Mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016”

Mheshimiwa Spika,

Kwa heshima kubwa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na afya nzuri inayoniwezesha kusimama mbele ya ukumbi huu na kuweza kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusiana na azimio hili. Aidha, nitoe shukrani kwa wananchi na wanachama wote wa chama cha wananchi-CUF kwa imani yao kwangu na kwa chama chetu katika kuhakikisha kuwa tunapambana kwa nguvu zote ili kushinda nguvu za aina yoyote kutoka nje ya chama chetu zinazokusudia kukidhuru na kukihujumu chama chetu

kilichobeba matumaini ya watanzania wapenda mabadiliko na demokrasia ndani ya ushirikiano madhubuti ujulikanao kama UKAWA.

Mheshimiwa Spika,

Nitakuwa si mwangi wa fadhila kama sita mshukuru Naibu wangu, Mheshimiwa Peter Lijualikali kwa msaada wake katika maandalizi ya maoni haya, sambamba na hili niwashukuru waheshimiwa wajumbe wenzangu wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo, Maji na Uvuvi kwa ushirikiano mkubwa tulionao ndani ya kamati.

Mheshimiwa Spika,

Baada ya kutoa utangulizi huo, naomba kueleza baadhi ya mambo ambayo kwa mtazamo wetu tumeona yanahitaji kupatiwa maelezo ya kina na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika,

Kama azimio la Bunge linavyosema kwamba Bonde la Mto Songwe ndilo linalofanya mpaka kati ya Tanzania na Nchi ya Malawi na wilaya za Kyela, Ileje, Mbozi Mbeya Vijiji na Mombasa zimo ndani ya Bonde hilo. Kutokana na ukweli kwamba mto huo umekuwa ukihama hama na hivyo kusababisha mpaka baina ya nchi hizi nao kuhama hama, jambo ambalo linaweza kusababisha mtafaruku na jirani zetu hao.

Mheshimiwa Spika,

Taarifa ya Mheshimiwa Waziri aliyoleta kwenye kamati inaonesha kuwa Tanzania na Malawi zinatekeleza Mradi wa kudhibiti Mkondo wa Mto Songwe (Stabilization of the Course of Songwe River Project) kwa kujenga Bwawa la Songwe Chini ambalo litajengwa baada ya kusainiwa Mkataba huu na bwawa hilo litatumika kuzalisha umeme wa Megawati 180.2, kutoa huduma ya maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, viwandani, kilimo cha umwagiliaji, uvuvi, hifadhi ya mazingira na utalii na hivyo kuongeza fursa za kiuchumi na kuboresha hali za maisha ya wakazi wa eneo la Bonde la mto Songwe.

Mheshimiwa Spika,

Maelezo hayo niliyosoma yameelezwa kwenye Ibara ya 8 ya mkataba kuwa ni baadhi ya kazi za Kamati ambayo inaundwa chini ya Ibara ya 4 ya Mkataba.

Mheshimiwa Spika,

Kazi hizo za Kamati kama ilivyoundwa chini ya ibara tajwa yanatekelezwa na kusimamiwa na Secretariat inayoanzishwa na Ibara ya 4, Ibara ya 9 inaainisha majukumu ya Sekretariat, pamoja na majukumu mengine Ibara ya 9, kifungu cha 6(g) kinasema kwamba:

" Manage on daily basis the construction, operation and maintenance of all infrastructure under Songwe River Basin Development Programme, including flood warning, hydropower, irrigation systems and operation of the dam; social infrastructure and regularly obtain, update and exchange information and data as necessary, including the development and use of decision support system;"

Mheshimiwa Spika,

Kifungu hicho kinaonesha kuwa kazi hizo zote zinatakiwa zifanywe na Secretariat, lakini tukumbuke kwamba ustawi wa wananchi katika wilaya husika utakuwepo kama wananchi mmoja mmoja au kwa vikundi vyao au Kampuni zao (Local Content) wapanufaika kwa kuwa wamiliki katika miradi itakayoanzishwa na Kamisheni hiyo. Sambamba na hilo ni kwamba ushiriki huo wa wananchi utawezekana kwa sheria yetu ya PPP kati ya Kamisheni na wananchi (Sekta binafsi).

Mheshimiwa Spika,

Japokuwa Ibara ya 18 inaongelea mawanda ya Mkataba ni kwamba washirika wa mkataba wanaweza kuingia mkataba baina au ya kimataifa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi au programe zitakazotakiwa kutekelezwa na Kamisheni. Kambi Rasmii ya Upinzani inasema bado Ibara hiyo hajatoa uhakika wa ushiriki wa wanufaikaji katika kumiliki na kutekeleza miradi husika.

Mheshimiwa Spika,

Ni ukweli uliowazi kwamba miradi mingi ambayo ilianzishwa na Serikali kwa ufadhili kwa ajili ya wananchi imekufa kutokana na kutokuwepo kwa dhana ya umiliki kutoka upande wa wanufaikaji(wananchi), na tukumbuke kwamba watangulizi wa Serikali hii ya tano waliliona hilo na ndio sababu ya ubinafsishaji japokuwa kutokufanya vizuri kwa ubinafsishaji hakukuwa ni dhana hiyo bali utekelezaji wake. Kushindwa kwake kulitokana na ulegelege na kutowajibika ipasavyo kwa wahusika waliokuwa wasimamizi wa zoezi hilo la ubinafsishaji

Mheshimiwa Spika,

Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kwamba kwa kuwa moja ya lengo la uundwaji wa Kamisheni hii ni utumiaji endelevu(sustainable) wa rasimali ya maji kwa wananchi wa wilaya tajwa hapo awali, hivyo basi ni lazima ushiriki wa wananchi uonekane wazi kwenye Mkataba huu ili sheria zetu za utekelezaji zitakapotungwa(domestication), vipengele vya uhusishwaji wa wananchi kwenye maeneo tajwa uakisiwe kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika,

Kinyume cha hapo Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba Kamisheni hii na malengo yake hayatakuwa na manufaa kwa maendeleo ya wananchi hasa wa maeneo husika, bali itakuwa kama mamlaka ya uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji ambayo badala ya kuwa mkombozi au mleta kicheko kwa wananchi wa maeneo husika imekuwa ndio mleta kilio kwa wananchi na hivyo Taifa kuendelea kubaki kuwa watazamaji tu wa rasimali hiyo adhimu bila kunufaika nayo. Serikali kuacha kulifanyia kazi stahiki Bonde la Mto Rufiji ni muendelezo wa kutotumia vizuri rasilimali zetu.

Mheshimiwa Spika,

Ni ukweli kabisa kuwa hii kamisheni sio kama inajikita kwenye maji tu, bali ni kweli ardhi ambayo wakulima wengi wanaendesha shughuli za maisha yao ya kila siku. Kwa maana hiyo basi ni muhimu Mheshimiwa Waziri akaweka wazi kuhusiana na mfumo mzima wa vibali vya matumizi ya ardhi

hiyo ambayo imo ndani ya himaya ya kamisheni. Kwa maana nyingine ni kwamba maisha ya wananchi wa wilaya husika yataathirika kwa kiwango kikubwa sana. Jambo hilo pia lifanywe kwa kuzingatia pia suala zima la usalama wa taifa letu. Kamisheni ni vyema pia idara zetu zinazohusika na ulinzi na usalama wa Taifa kwani isije ikatumika kama ndio ufunguaji wa mipaka yetu.

Mheshimiwa Spika,

Baada ya kusema hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani haina sababu ya kutokuridhia azimio la kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa kwa Kamisheni hii ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

.....
Hamidu H.Bobali (Mb)

**Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-Wizara ya
Maji na Umwagiliaji.**

7/9/2017

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea.
Katibu.

NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:

AZIMIO LA BUNGE

**Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama
wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African
Community Protocol on Peace and Security*)**

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani
ya Nchi, Mheshimiwa Mwigulu Nchomba.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba maelezo yote niliyoyleta kwa ajili ya Azimio hili yaingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa hii ili jiweze kuwasilisha mapendeleko ya kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Community Protocol on Peace and Security*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na mkataba wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 1999 pamoja na marekebisho yake, hatua nne za mtangamano ambazo ni kuwepo kwa umoja wa forodha, ikifuatiwa na soko la pamoja, kisha umoja wa fedha na hatimaye shirkisho la kisiasa, vilipangiliwa. Aidha, Ibara ya 124 ya mkataba huo inaelezea kuwa nchi wanachama zimekubaliana kuwa amani na usalama ndio nguzo kuu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Jumuiya ya Afrika Mashariki

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Ibara ya 151 ya mkataba huo inatoa mamlaka kwa nchi wanachama kuandaa na kuridhia itifaki katika maeneo mbalimbali ya ushirikiano. Ili kuweza kutekelezwa kwa itifaki iliyoidhinishwa ni lazima nchi zote wanachama kuridhia, kulingana na taratibu za ndani ya nchi husika na kisha kuwasilisha hati za kuridhia kwa itifaki hizo kwa Katibu Mkuu wa Jumuya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Protocol on Peace and Security*) iliyodhinishwa kwa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mukutano uliofanyika Novemba mwaka 2012 na kisha kusainiwa na Mawaziri wa nchi tano wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, tarehe 15 mwezi wa Februari, 2013. Mpaka sasa nchi tatu ambazo ni Kenya, Rwanda na Uganda zimeridhia itifaki hiyo kulingana na matakwa ya mkataba, Ibara ya 152 niliyoitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipengele muhimu nya ushirikiano vimeainishwa kwenye Ibara ya Pili Na. (2), (3) ni pamoja na kuzuia na kutatua migogoro ya ndani ya nchi na nje ya nchi wanachama ambapo nchi wanachama zimekubaliana kutatua migogoro itakayojitokeza na miongoni mwao ni pamoja na kushughulikia matatizo yanayojitokeza na kuleta mauaji ya kimbari, kupambana na ugaidi, kupambana na uharamia, kushiriki katika operesheni za kulinda amani, kukabiliana na kupunguza madhara yanayotokana na majanga ambapo nchi wanachama zimekubaliana kuanzisha mifumo ya kupashana taarifa za majanga ili kupunguza au kukabiliana nayo kabla hayajajitokeza ili kutoleta madhara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kusimamia masuala ya wakimbizi kwa nchi wanachama, kuhuisha sera, sheria na mikakati na programu zinazosimamia masuala ya wakimbizi kulingana na makubaliano ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Wakimbizi wa Mwaka 1951 na Mkataba wa Umoja wa Nchi za Afrika wa Mwaka 1969 unaohusu matatizo ya wakimbizi Barani Afrika. Aidha, kuoanisha taratibu juu ya kutafuta na kuhifadhi wahusika wanaoshughulikia upashanaji wa habari katika masuala ya mitandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine muhimu ya itifaki hii ni kudhibiti uzagaaji wa silaha haramu ndogondogo na nyepesi, kukabiliana na uhalifu wa Kimataifa na uhalifu unaovuka mipaka pamoja na kuzuia na kupambana na wizi wa mifugo na utoaji wa huduma Magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuridhia itifaki hii kutarahisisha uainishaji wa sera, sheria, programu za ndani ya Jumuiya zenye uwiano katika masuala ya amani na usalama. Kuwepo kwa mazingira mazuri ya amani na usalama hivyo, kuwezesha wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi na za kijamii bila kuwa na hofu. Kingine ni kujenga mazingira ya ujirani mwema kwa jamii za wafugaji wa ndani ya nchi pamoja na jamii zao ambazo wanafanya

shughuli zinazowiana ikiwemo pia na kuimarisha ushirikiano katika kupambana na kuondoa wizi wa mifugo unaojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuimarisha na kuimarika kwa uzoefu na pia, nchi zitawezwa kuwa na mpango wa kubadilishana wafungwa; nchi zitawezwa kutunga sheria na kuweka mikakati ya pamoja ya kuimarisha amani na usalama wa nchi wanachama na makosa yanayovuka mipaka yatadhilitiwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya maelezo ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha Azimio lenyewe kwa Bunge ili liweze kuridhiwa, kama ifuatavyo:-

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa mujibu wa Ibara ya 3(1) cha Mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao ulisainiwa na Wakuu wa nchi wanachama uliofanyika Mjini Arusha tarehe 30 Novemba,1999;

NA KWA KUWA, Ibara ya 151 ya Mkataba huo wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unatoa mamlaka kwa Nchi Wanachama kuandaa na kuridhia itifaki katika maeneo mbalimbali ya ushirikiano ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Jumuiya;

NA KWA KUWA, mkataba huo unaelekeza kwamba kila itifaki itakayoandalishiwa itaidhinishwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na itakuwa wazi kwa ajili ya kusainiwa na hatimaye kuridhiwa na nchi wanachama kwa mujibu wa taratibu zao;

NA KWA KUWA, Itifaki ya Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliidhinishwa na Mkutano Mkuu wa 14 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 30 Novemba, 2012 Mjini Nairobi, Kenya na kusainiwa na Mawaziri kutoka katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, tarehe 15

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Februari, 2013 ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mojawapo ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyosaini Itifaki hii;

NA KWA KUWA, lengo la Itifaki hii ni kuimarisha amani na usalama na utulivu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kukuza ujirani mwema kwa nchi wanachama.

NA KWA KUWA, kwa kujunga kwa Itifahi hii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania itaimarisha ushirikiano wake na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kutatua migogoro mbalimbali katika Jumuiya ya Afrika Mashariki hivyo, kuimarisha ujirani mwema, kuwepo kwa amani na usalama kutokana na kubadilishana taarifa za uhalifu na uhalifu unaovuka mipaka, kupata taarifa za kuibuka kwa makosa mapya, kuimarisha mapambano dhidi ya ugaidi, dawa za kulevyta, biashara haramu za binadamu, kuenea kwa silaha haramu ndogondogo na nyepesi, wizi wa mitandaoni na vilevile kusaidia katika kubadilishana ujuzi na uzoefu katika kubadilishana wahalifu.

HIVYO BASI, kwa kuzingatia manufaa yatakayotokana na itifaki hii kwa Tanzania na pia, umuhimu wa kuridhia itifaki hii, Bunge hili katika Mkutano wake wa Nane kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kuridhia Itifaki hii iitwayo Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Community Protocol on Peace and Security*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono.

**MAELEZO YA UTANGULIZI YA KURIDHIA ITIFAKI YA AMANI
NA USALAMA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAST
AFRICAN COMMUNITY PROTOCOL ON PEACE AND SECURITY)
KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii niweze kuwasilisha mapendekezo ya ya kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani *East African Community Protocol on Peace and Security*.

Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Kulingana na Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999 pamoja na marekebisho yake umeainisha hatua nne za Mtangamano ambazo ni kuwepo kwa Umoja wa Forodha ikifuatiwa na Soko la Pamoja kisha Umoja wa Fedha na hatimaye Shirikisho la Kislasa. Aidha, Ibara ya 124 ya Mkataba huo inaeleza kuwa nchi wanachama zimekubaliana kuwa Amani na Usalama ndiyo nguzo kuu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Jumuiya. Kwa msingi huo, nchi wanachama zimekubaliana kujenga na kuimarisha mazingira mazuri ya amani na usalama kwa kushirikiana katika nyanja hiyo kwa lengo la kuzuia uhalifu na kutatua migogoro itakayojitokeza kwa njia ya amani, kuimarisha ujirani mwema, kuandaa mfumo wa pamoja wa menejimenti ya wakimbizi na kuimarisha mfumo wa kupambana na wahalifu wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Ibara ya 151 ya Mkataba inatoa mamlaka kwa nchi wanachama kuandaa na kuridhia Itifaki katika maeneo mbalimbali ya ushirikiano. Ili kutekelezwa kwa itifaki iliyoidhinishwa ni lazima nchi zote wanachama kuiridhia kulingana na taratibu za ndani za nchi husika na kisha kuwasilisha Hati ya kuridhia Itifaki hiyo kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani iliyodhinishwa na Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mukutano uliofanyika mwezi Novemba, 2012 na kisha kusainiwa na

mawaziri wa nchi tano wanachama wa Jumuiya kwa wakati huo tarehe 15 Februari, 2013. Mpaka sasa nchi tatu ambazo ni Kenya, Rwanda na Uganda zimeridhia Itifaki hiyo kulingana na matakwa ya Ibara ya 152 ya Mkataba.

Mhesimiwa Spika, Vipengele muhimu vyatayishwa kwenye Ibara ya 2(3) ni pamoja na Kuzuia na kutatua migogoro ndani na nje ya nchi wanachama ambapo nchi Wanachama zimekubaliana kutatua migogoro itakayojitokeza mionganini mwao au na nchi nyiningine kwa njia ya amani. Vile vile, Jumuiya imekubaliana kushirikiana na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (*United Nations Security Council*) na Baraza la Amani na Usalama la Umoja la Afrika (*Peace and Security Council of the African Union*) katika kutatua migogoro ya nchi mwanachama au nchi nyiningine kwa njia ya Amani.

Mhesimiwa Spika, itifaki hii imekusudia kuzuia mauaji ya kimbari, Kupambana na ugaidi, Kupambana na uharamia, Kushiriki katika operesheni za kuliinda amani, Kukabiliana na kupunguza madhara yatokanayo na majanga ambapo nchi wanachama zimekubaliana kuanzisha mifumo ya kupashana taarifa za majanga ili kupunguza au kukabiliana nayo kabla hayajajitokeza na kuleta madhara, Kusimamia masuala ya Wakimbizi kwa nchi wanachama kuhuisha Sera, Sheria, Mikakati na Programu za usimamizi wa masuala ya wakimbizi kulingana na makubaliano ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Wakimbizi wa mwaka (1951) na Mkataba wa Umoja wa nchi za Afrika wa mwaka (1969) unaohusu matatizo ya wakimbizi barani Afrika. Aidha, kuoanisha taratibu juu ya watafuta hifadhi kwa kuwa na mitandao ya kupashana taarifa.

Mhesimiwa Spika, maeneo mengine muhimu ya itifaki hii ni Kudhibiti uzagaaji wa silaha haramu ndogondogo na nyepesi, kukabiliana na uhalifu wa kimataifa na uhalifu unaovuka wa mipaka, Kuzuia na kupambana na wizi wa mifugo na Utoaji wa huduma za Magereza.

Mheshimiwa Spika, kuridhia itifaki hii kutarahisisha uainishaji wa Sera, Sheria na Programu za ndani ya Jumuiya zenyewe uwiano katika masuala ya amani na Usalama, Kuwepo kwa mazingira mazuri ya amani na usalama hivyo kuwawezesha wananchi kufanya shughuli za kiuchumi na kijamii bila hofu, Kujenga mazingira ya ujirani mwema kwa jamii za wafugaji ndani ya Jumuiya, Kuimarisha ushirikiano katika kupambana na kuondoa wizi wa mifugo, kuimarika kwa uzoefu na pia nchi zitaweza kuwa na mpango wa kubadilishana wafungwa, nchi zitatunga sheria na kuweka mikakati ya pamoja ya kuimarisha Amani na Usalama wa nchi wanachama na Makosa yanayovuka mipaka yatadhibitiwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kuwasilsha Azimio la Bunge la kuridhia kama ifuatavyo:-

AZIMIO LA BUNGE NA. LA MWAKA 2017

**AZIMIO LA KURIDHIA ITIFAKI YA AMANI NA USALAMA YA
JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAST AFRICAN
COMMUNITY PROTOCOL ON PEACE AND SECURITY)**

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (The East African Community - EAC) kwa mujibu wa Ibara ya 3(1) ya Mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao ulisainiwa na Wakuu wa Nchi Wanachama wa EAC uliofanyika mjini Arusha, tarehe 30 Novemba, 1999;

NA KWA KUWA, Ibara ya 151 ya Mkataba huo wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999 (The Treaty for the Establishment of the East African Community) inatoa mamlaka kwa nchi wanachama kuandaa na kuridhia Itifaki katika maeneo mbalimbali ya ushirikiano ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Jumuiya;

NA KWA KUWA, Mkataba huo unaelekeza kwamba kila Itifaki itakayoandalishiwa na Mkutano wa Wakuu wa

Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na itakuwa wazi kwa ajili ya kusainiwa na hatimaye kuridhiwa na Nchi Wanachama kwa mujibu wa taratibu zao;

NA KWA KUWA, Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (East African Community Protocol on Peace and Security) iliidhinishwa na Mkutano Wakuu 14 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa EAC uliofanyika tarehe 30 Novemba, 2012 mjini Nairobi Kenya na kusainiwa na Mawaziri kutoka nchi wanachama wa Jumuiya tarehe 15 Februari, 2013 ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mojawapo ya Nchi Wanachama wa EAC iliyosaini Itifaki hii;

NA KWA KUWA, Lengo la Itifaki hii ni kuimarisha amani, usalama na utulivu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kukuza ujirani mwema kwa nchi wanachama;

NA KWA KUWA, Kwa kuijunga na Itifaki hii Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaimarisha ushirikiano wake na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kutatua migogoro mbalimbali katika Jumuiya na hivyo kuimarisha ujirani mwema, kuwepo na amani na usalama kutohakana kubadilishana taarifa za uhalifu na uhalifu unaovuka mipaka, kupata taarifa za kuibuka kwa makosa mapya, kuimarisha mapambano dhidi ya ugaidi, dawa za kulevyta, biashara haramu ya binadamu, kuenea kwa silaha haramu ndogo ndogo na nyepesi, wizi wa mtandaoni na vilevile kusaidia katika kubadilishana ujuzi na uzoefu katika kukabiliana na uhalifu;

HIVYO BASI, Kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Itifaki hii kwa Tanzania na pia umuhimu wa kuridhia Itifaki hii, Bunge hili katika Mkutano wa nane na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka, 1977 linaazimia kuridhia Itifaki hii iitwayo **ITIFAKI YA AMANI NA USALAMA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAST AFRICAN COMMUNITY PROTOCOL ON PEACE AND SECURITY)**

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

NAIBU SPIKA: Tutaendelea na utaratibu wetu. Sasa tutamsikia Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

MHE. STEPHEN J. MASELE (K.n.y. MHE. BAL. ADADI M. RAJABU - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuuya ya Afrika Mashariki (*The East African Community Protocol on Peace and Security*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6),(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Itifaki ya Amani na Usalama wa Jumuuya ya Afrika Mashariki (*The East African Community Protocol on Peace and Security*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyongeza ya Nane ya Kifungu cha 7(1)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inazipa Kamati za kisekta ikiwemo Kamati hii jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa, kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sambamba na hilo, jukumu hili pia ni jukumu la Kikatiba chini ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 6(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama inasimamia Wizara tatu ambazo ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, masuala yaliyomo katika itifaki hii yanazigusa moja kwa moja Wizara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo 5 Septemba, 2017, Kamati yangu ilikutana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba na kupokea maelezo ya Serikali kuhusu chimbuko, vipengele vya muhimu na faida ya kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Baada ya maelezo hayo, Kamati ilipata fursa ya kutafakari na kujadili kwa kina hoja hiyo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya msingi yaliyozingatiwa na Kamati. Kwa kuzingatia wajibu wa Kamati kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo, Kamati ilizingatia masuala mbalimbali katika kujiridhisha na hoja iliyotolewa na Serikali. Kamati ilifanya mapitio ya mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 1999 ambapo Ibara ya 124 ya mkataba huo inaeleza kuwa nchi wanachama zimekubaliana kuwa amani na usalama wa Kanda ya Afrika Mashariki ndlio nguzo ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Aidha, Kamati ilijiridhisha kuwa Ibara ya 151 ya mkataba huo, inatoa mamlaka kwa nchi wanachama kuandaa, kuridhia itifaki, katika maeneo mbalimbali ya ushirikiano likiwemo suala la amani na usalama. Itifaki iliyordhiwa kwa mujibu wa Ibara ya 124 na Ibara ya 151 ya mkataba huo inakuwa ni sehemu ya mkataba na hivyo kuweka misingi ya kisheria na kuilazimisha nchi mwanachama kuitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati ilijiridhisha kuhusu muda kipindi ambacho itifaki hii ilisainiwa na nchi wanachama. Katika kufanya hivyo, Kamati ilibaini kuwa itifaki hii ilisainiwa na Mawaziri wa Nchi zote Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwezi Julai mwaka 2013. mpaka sasa ni nchi tatu tu; Kenya, Rwanda na Uganda zimeridhia itifaki hiyo kwa mujibu wa Ibara ya 152 ya mkataba mama na kuzifanya Tanzania na Burundi kuwa nchi pekee ambazo bado hazijaridhia itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko, malengo na madhumi ya Itifaki hii. Kama ilivyoelezwa katika sehemu ya

kwanza ya taarifa hii, Ibara ya 124 ya mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 1999 inaeleza kuwa nchi wanachama zilikubaliana kuwa amani na usalama ni maeneo muhimu katika ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii ndani ya Jumuiya. Kwa kuzingatia jambo hilo nchi wanachama zinawajibika kusaini na kuridhia itifaki husika ili kufanikisha utekelezaji wenye tija wa mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Itifaki hii ni kuimarisha amani, usalama na utulivu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, pamoja na kukuza ujirani mwema kwa nchi wanachama. Itifaki hii inataja maeneo muhimu ya ushirikiano ambayo yote yanalenga kuimarisha amani, ulinzi na usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Maeneo haya ni pamoja:-

- (i) Kuzuia na kutatua migogoro ndani na nje ya nchi wanachama;
- (ii) Kuzuia mauaji ya kimbari ikiwa ni pamoja na kuzuia vitendo vya kuharibu kwa jumla au sehemu ya Utaifa, uasili, ubaguzi wa rangi ama dini;
- (iii) Kupambana na ugaidi;
- (iv) Kushiriki katika operesheni za kulinda amani;
- (v) Kukabiliana na kupunguza madhara yatokanayo na majanga;
- (vi) Kusimamia masuala ya wakimbizi;
- (vii) Kudhibiti kuzagaa kwa silaha haramu ndogondogo na nyepesi;
- (viii) Kukabiliana na uhalifu wa kimataifa na uhalifu unaovuka mipaka;
- (ix) Kuzuia na kupambana na wizi wa mifugo; na

- (x) Kushirikiana katika utoaji wa huduma za magereza ikiwemo kubadilishana wafungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa maeneo hayo muhimu, nchi wanachama zimekubaliana kuanzisha mifumo, sera na operesheni na mikakati ya pamoja kupambana na uhalifu wa aina zote. Aidha, nchi wanachama zimekubaliana kuhuisha sera, sheria, mikakati na programu za usimamizi wa masuala ya wakimbizi kulingana na makubaliano ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Wakimbizi wa mwaka 1951 na Mkataba wa Umoja wa Nchi za Afrika wa mwaka 1969 unaohusu matatizo ya wakimbizi Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la kushirikiana katika utoaji wa huduma za magereza, nchi wanachama zimekubaliana kushirikiana katika ubadilishanaji wa wafungwa, mahabusu na urekebishwaji wa tabia za wahalifu pamoja na kushirikiana katika kuboresha mifumo ya utawala katika Magereza na huduma za marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida na changamoto za kuridhia Itifaki hii. Zipo faida nyingi ambazo zinapatikana Tanzania kuridhia itifaki hii. Faida hizo ni pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaimarisha ushirikiano wake na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kutatua migogoro mbalimbali na hivyo kuimarisha ujirani mwema, kuwepo kwa amani na usalama katika nchi kutokana na kubadilishana taarifa za uhalifu na uhalifu unaovuka mipaka, kupata taarifa za kuibuka kwa makosa mapya, kuimarisha mapambano dhidi ya ugaidi, dawa za kulevyta, biashara harama za usafirishaji wa binadamu, kuenea kwa silaha haramu na wizi wa mitandaoni. Mwisho kubadilishana ujuzi na uzoefu katika kukabiliana na uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika upande wa Jumuiya ya Afrika kuridhiwa kwa Itifaki hii kunarajiwा kuwa na matokeo yafuatayo:

- (i) Itifaki itarahisisha uainishaji wa sera, sheria za program

za ndani ya Jumuiya zenyе uwiano katika masuala ya amani na usalama.

- (ii) Kuwepo kwa mazingira mazuri ya amani na usalama, kuwawezesha wananchi wa nchi wanachama kufanya shughuli za kiuchumi bila hofu.
- (iii) Kujenga mazingira ya ujirani mwema kwa jamii za wafugaji ndani ya Jumuiya.
- (iv) Kuimarisha ushirikiano katika kupambana na kuondoa uhalifu wa aina zote.
- (v) Kuimarika kwa uzoefu wa kukabiliana na makosa ya jinai na pia nchi wanachama zitaweza kuwa na mipango madhubuti ya kubadilishana wafungwa.

Itifaki hii itahusisha *operations* zote ambazo zitakuwa na viashiria vya uvunjifu wa amani na haki za binadamu.

Changamoto kuridhia Itifaki hii. Zipo changamoto kadhaa zinazoweza kujitekeza kwa Tanzania kuridhia Itifaki hii, changamoto hii ni pamoja na gharama za kuendesha *operations* mbalimbali za pamoja kama vile *operations* za ukamataji wa bidhaa bandia mipakani na kuwa na mafunzo ya pamoja kwa nyakati tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto hizo Kamati yangu imejiridisha kuwa faida zinazopatikana kwa Bunge kuridhia Azimio hili ni nyingi na zenyе manufaa si tu kwa Tanzania pekee bali wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ujumla wake, hususan katika kufanikisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya kujadili kwa kina hoja ya Serikali kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

Kwanza, ucheleweshwaji wa kuridhia Itifaki. Kamati ilipokuwa ikifanya uchambuzi wake ilibaini kuwa Itifaki hii

ilisainiwa na nchi wanachama, husika tarehe 12 Julai, 2013. Itifaki hii imechukua miaka minne kuletwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa licha ya kuonekana kuwa ina manufaa makubwa kwa nchi. Kamati inaishauri Serikali kuwasilisha Itifaki zote zilozosainiwa ambazo zinahitaji kuridhiwa na Bunge kwa kuzingatia matakwa ya sheria.

Pili, masuala ya wizi wa kimtandao kuingizwa katika Itifaki. Ibara ya 12 ya Itifaki hii inaainisha maeneo ambayo nchi wanachama zimekubaliana kuandaa mifumo, sera na mikakati ya pamoja, kuzuia na kukabiliana na aina mbalimbali za uhalifu wa Kimataifa na uhalifu unaovuka mipaka ikiwemo wizi wa magari, biashara haramu ya usafirishajij wa binadamu, mapambano dhidi ya ugaidi na dawa za kulewa.

Mheshimiwa Nailbu Spika, hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa hakukuwa na kipengele mahususi kinachoongelea masuala ya kuweka mikakati madhubuti ya kuzuia wizi wa mitandaoni (*cybercrime*) ambao ukuaji wake ni wa kasi duniani kote. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa Itifaki hii kujumuisha kipengele hicho kwa siku za usoni, hatimaye kuwa na mkakati wa pamoja wa Jumuiya katika kudhibiti tatizo hili.

Tatu, utungaji wa sheria na mikakati ya pamoja. Katika utekelezaji za Itifaki hii nchi wanachama zitatunga sheria na kuweka mikakati ya pamoja, kuimarisha amani na utulivu ndani ya Jumuiya. Pamoja na jambo hili jema Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa sheria zitakazotungwa pamoja na mikakati itakayowekwa ziwe zenye manufaa na tija kwa Taifa letu.

Nne, ubadilishaji wa wafungwa katika Jumuiya. Suala la ubadilishaji wa wafungwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki limekuwa lina ugumu kwa muda mrefu. Kamati inaishauri Serikali kuwa mara Itifaki hii itakaporidhiwa na kuwa tayari kwa utekelezaji wake mikakati ya namna ya kushirkiana katika kubadilishana wafungwa iandaliwe kwa umakini mkubwa ili iweze kuwezesha wafungwa

wanaotumikia vifungo katika nchi ambazo wao siyo raia kurejeshwa na kutumikia vifungo katika nchi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati sasa naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa michango yao mizuri wakati wa kuchambua hoja ya Serikali. Michango yao imewezesha kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo; wakiongozwa na Mheshimiwa Balozi Mohamed Adadi Rajab Mbunge, Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud Ali Khamis Mbunge, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Capt. George Huruma Mkuchika, Mbunge...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Stephen Masele majina huwa hayasomwi Kikanuni. Kwa hiyo, wewe omba tu yaingia kwenye *Hansard*.

MHE. STEPHEN J. MASELE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uendeshaji mzuri wa Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati kumshukuru Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa uwasilishaji na ufanuzi wa kina alioutoa wakati wa Kamati ikichambua Itifaki hii. Aidha, nawashukuru watalaam wa Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambao michango yao imewezesha Kamati kuchambua kujiridhisha kuhusu faida za kuridhia Itifaki hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati hii Ndugu Ramadhani Abdallah,

Ndugu Grace Bidya wakisaidiwa na Ndugu Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati kuhakiki taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Azimio hili na naomba Bunge letu Tukufu liridhie Itifaki hii kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU AZIMIO LA BUNGE
LA KURIDHIA ITIFAKI YA AMANI NA USALAMA YA JUMUIYA
YA AFRIKA MASHARIKI (EAST AFRICAN COMMUNITY
PROTOCOL ON PEACE AND SECURITY) – KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Community Protocol on Peace and Security*).

Mheshimiwa Spika, Nyongeza ya Nane ya Kifungu cha 7(1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, inazipa Kamati za kisekta, ikiwemo Kamati hii, jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia. Sambamba na hilo, Jukumu hili pia ni jukumu la kikatiba chini ya Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama inasimamia Wizara tatu ambazo ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ulinzi na JKT, na Wizara ya Mambo ya Nje na

Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Masuala yaliyomo katika Itifaki hii yanazigusa moja kwa moja Wizara hizi.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 05 Septemba, 2017 Kamati yangu ilikutana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba, Mb, na kupokeo maelezo ya Serikali kuhusu chimbuko, vipegele vya muhimu na faida za kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Baada ya maelezo hayo, Kamati ilipata fursa ya kutafakari na kujadili kwa kina Hoja hiyo ya Serikali.

1.1 Mambo ya Msingi yaliyozingatiwa na Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia wajibu wa Kamati katika kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo, Kamati ilizingatia masuala mbalimbali katika kujiridhisha na Hoja illyotolewa na Serikali. Kamati illifanya Mapitio ya Mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 1999 ambapo Ibara ya 124 ya Mkataba huo inaeleza kuwa nchi wanachama zimekubaliana kuwa Amani na Usalama wa Kanda ya Afrika Mashariki ndio nguzo kuu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Jumuiya hiyo.

Aidha, Kamati ilijiridhisha kuwa Ibara ya 151 ya Mkataba huo inatoa Mamlaka kwa nchi wanachama kuandaa na kuridhia Itifaki katika maeneo mbalimbali ya ushirikiano likiwemo suala la Amani na Usalama. Itifaki inayoridhiwa kwa mujibu wa Ibara ya 124 na 151 ya Mkataba huo, inakuwa sehemu ya Mkataba na hivyo kuweka misingi ya Kisheria na kuilazimisha nchi mwanachama kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kamati ilijiridhisha kuhusu muda/ kipindi ambacho Itifaki hii ilisainiwa na nchi wanachama. Katika kufanya hivyo, Kamati ilibaini kuwa, Itifaki hii ilisainiwa na Mawaziri wa nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Mwezi Julai, 2013. Mpaka sasa, nchi tatu za Kenya, Rwanda na Uganda zimesharidhia Itifaki hiyo kwa mujibu wa Ibara ya 152 ya Mkataba mama, na kuzifanya Tanzania na Burundi kuwa nchi pekee ambazo bado hazijaridhia Itifaki hii.

1.2 Chimbuko, Malengo na Madhumuni ya Itifaki

Mheshimiwa Spika, Kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 1.1 ya taarifa hii, Ibara ya 124 ya Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999, inaeleza kuwa nchi wanachama zilikubaliana kuwa Amani na Usalama ni eneo muhimu katika ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii ndani ya Jumuiya. Kwa kuzingatia jambo hilo, nchi wanachama zinawajibika kusaini na kuridhia itifaki husika ili kufanikisha utekelezaji wenye tija wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Lengo la itifaki hii ni kuimarisha amani, usalama na utulivu katika jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kukuza ujirani mwema kwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, Itifaki hii inataja maeneo muhimu ya Ushirikiano ambayo yote yanalenga kuimarisha **amani, ulinzi na usalama** wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Maeneo haya ni pamoja na:-

- i) Kuzuia na kutatua migogoro ndani na nje ya nchi wanachama.
- ii) Kuzuia mauaji ya Kimbari ikiwa ni pamoja na kuzuia vitendo vya kuharibu kwa jumla au sehemu ya utaifa, uasili, ubaguzi wa rangi au dini.
- iii) Kupambana na ugaidi.
- iv) Kushiriki katika operesheni za kulinda amani.
- v) Kukabiliana na kupunguza madhara yatokanayo na majanga.
- vi) Kusimamia masuala ya wakimbizi.
- vii) Kudhibiti kuzagaa kwa silaha haramu ndogo ndogo na nyepesi.
- viii) Kukabiliana na uhalifu wa kimataifa na uhalifu unaovuka mipaka.
- ix) Kuzuia na kupambana na wizi wa mifugo.
- x) Kushirikiana katika utoaji wa huduma za magereza ikiwemo kubadilishana wafungwa.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa maeneo

hayo muhimu, nchi wanachama zimekubaliana kuanzisha mifumo, sera, operesheni na mikakati ya pamoja katika kupambana na uhalifu wa aina zote. Aidha, nchi wanachama zimekubaliana kuhuisha Sera, Sheria, Mikakati na Programu za usimamizi wa masuala ya wakimbizi kulingana na makubaliano ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Wakimbizi wa Mwaka 1951 na Mkataba wa Umoja wa Nchi za Afrika wa Mwaka 1969 unaohusu matatizo ya wakimbizi Barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, katika suala la kushirikiana katika utoaji wa huduma za Magereza, nchi wanachama zimekubaliana kushirikiana katika ubadilishanaji wa wafungwa, mahabusu na urekebishi waji wa tabia za wahalifu pamoja na kushirikiana katika kuboresha mifumo ya utawala katika magereza na huduma za marekebisho.

2.0 FAIDA NA CHANGAMOTO ZA KURIDHIA ITIFAKI HII

2.1 Faida za Kuridhia Itifaki

Mheshimiwa Spika, zipo faida nyingi ambazo zitapatikana kwa Tanzania kuridhia Itifaki hii. Faida hizo ni pamoja na:-

i) Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaimarisha ushirikiano wake na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kutatua migogoro mbalimbali na hivyo kuimarisha ujirani mwema.

ii) Kuwepo kwa amani na usalama katika nchi kutokana na kubadilishana taarifa za uhalifu na uhalifu unaovuka mipaka.

iii) Kupata taarifa za kuibuka kwa makosa mapya.

iv) Kuimarisha mapambano dhidi ya ugaidi, dawa za kulevyta, biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, kuenea kwa silaha haramu na wizi wa mitandaoni.

v) Kubadilishana ujuzi na uzoefu katika kukabiliana na uhalifu.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuridhia kwa Itifaki hii kunatarajiwa kuwa na matokeo yafuatayo:-

- i) Itifaki itarahisisha uainishaji wa Sera, Sheria na Programu za ndani ya Jumuiya zenyenye uwiano katika masuala ya amani na usalama.
- ii) Kuwepo kwa mazingira mazuri ya amani na usalama kuwawezesha wananchi wa nchi wanachama kufanya shughuli za kiuchumi na kijamii bila hofu.
- iii) Kujenga mazingira ya ujirani mwema kwa jamii za wafugaji ndani ya Jumuiya.
- iv) Kuimarishe ushirikiano katika kupambana na kuondoa uhalfu wa aina zote.

- v) Kuimariika kwa uzoefu wa kukabiliana na makosa ya jinai na pia nchi wanachama zitaweza kuwa na mipango madhubuti ya kubadilishana wafungwa.
- vi) Itifaki hii itahusisha operesheni zote ambazo zitakuwa na viashiria vya uvunjifu wa amani na haki za binadamu.

2.2 Changamoto za Kuridhia Itifaki

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto kadhaa zinazowenza kujitokeza kwa Tanzania kuridhia Itifaki hii. Changamoto hizi ni pamoja na gharama za kuwa na operesheni mbalimbali za pamoja kama vile operesheni za ukamataji wa bidhaa bandia mipakani; na kuwa na mafunzo ya pamoja kwa nyakati tofauti.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Changamoto hizo, Kamati yangu imejiridhisha kuwa faida zitakazopatikana kwa Bunge kulidhia Azimio hili ni nyingi na zenyenye manufaa si tu kwa Tanzania pekee bali kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ujumla wake hususan katika kufanikisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi wanachama.

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kujadili kwa kina Hoja ya Serikali kuhusu Azimio la kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

i) **Uchelewashwaji wa kuridhia Itifaki**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokuwa ikifanya uchambuzi wake, ilibaini kuwa Itifaki hii ilisainiwa na nchi wananchama husika tarehe 12 Julai, 2013. Itifaki hii imechukua miaka minne kuletwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa licha ya kuonekana kuwa ina manufaa makubwa kwa nchi yetu. Kamati inaishauri Serikali kuwasilisha Itifaki zote zilizosainiwa ambazo zinahitaji kuridhiwa na Bunge kwa kuzingatia matakwa ya Sheria.

ii) **Masuala ya Wizi wa Kimtandao kuingizwa katika Itifaki**

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 12 ya Itifaki hii inaanisha maeneo ambayo nchi wananchama zimekubaliana kuandaa mifumo, sera na mikakati ya pamoja ya kuzuia na kukabiliana na aina mbalimbali za uhalifu wa Kimataifa na uhalifu unaovuka mipaka ikiwemo wizi wa magari, biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, mapambano dhidi ya ugaidi, dawa za kulevyo nk.

Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa, hakukuwa na kipengele mahususi kilichoongelea masuala ya kuweka mikakati madhubuti ya kuzuia wizi wa mtandaoni (*cybercrime*) ambao ukuaji wake ni wa kasi duniani kote.

Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa Itifaki hii kujumuisha kipengele hicho kwa siku za usoni na hatimaye kuwa na mikakati ya pamoja ya Jumuiya katika kudhibiti tatizo hili.

iii) Utungaji wa Sheria na Mikakati ya Pamoja

Mheshimiwa Spika, Katika utekelezaji wa Itifaki hii, nchi wanachama zitatunga sheria na kuweka mikakati ya pamoja ya kuimarisha amani na utulivu ndani ya Jumuiya. Pamoja na jambo hili jema, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Sheria zitakazotungwa pamoja na mikakati itakayowekwa ziwe ni zenyе manufaa na tija kwa Taifa letu.

iv) Ubadilishanaji wa wafungwa katika Jumuiya

Mheshimiwa Spika, suala la ubadilishanaji wafungwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki limekuwa lina ugumu kwa muda mrefu. Kamati inaishauri Serikali kuwa, mara Itifaki hii itakaporidhiwa na kuwa tayari kwa utekelezaji wake, Mikakati ya namna ya kushirikiana katika ubadilishanaji wa wafungwa iandaliwe kwa umakini mkubwa. Hii itawezesha wafungwa wanaotumikia vifungo katika nchi ambazo wao si raia kurejeshwa na kutumikia vifungo katika nchi zao.

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati, sasa naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa michango mizuri wakati wa kuchambua Hoja ya Serikali. Michango yao imewezesha kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb, **Mwenyekiti**
2. Mhe. Kanal (Mst) Masoud Ali Khamis, Mb, **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Capt. George Huruma Mkuchika, Mb Mjumbwe
4. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb "
5. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb "
6. Mhe. Prosper J. Mbenza, Mb "
7. Mhe. Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa, Mb "
8. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb "
9. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb "
10. Mhe. Alphaxad Kangi Lugola, Mb "

- | | |
|--|---|
| 11. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb | " |
| 12. Mhe. Cosato David Chumi, Mb | " |
| 13. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb | " |
| 14. Mhe. Bonnah Kaluwa, Mb | " |
| 15. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb | " |
| 16. Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb | " |
| 17. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb | " |
| 18. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb | " |
| 19. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb | " |
| 20. Mhe. Lucy Simon Magereli, Mb | " |
| 21. Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb | " |
| 22. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb | " |
| 23. Mhe. Lazaro S. Nyalandu, Mb | " |
| 24. Mhe. Stephene J. Masele, Mb | " |
| 25. Mhe. Machano Othman Said, Mb | " |
| 26. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb | " |
| 27. Mhe. Khamisi Yahya Machano, Mb | " |
| 28. Mhe. Yahya Omari Masare, Mb | " |

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uendeshaji mzuri wa Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati, namshukuru Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, Mb, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa uwasilishaji na ufanuzi wa kina alioutoa wakati Kamati ikichambua Itifaki hii. Aidha, nawashukuru wataalamu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambao michango yao imeiwezesha Kamati kuchambua na kujiridhisha kuhusu faida za kuridhia Itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi.

Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Azimio hili na naomba Bunge lako Tukufu liridhie Itifaki hii kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mb

MWENYEKITI

KAMATI YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA
7 Septemba, 2017

NAIBU SPIKA: Sasa tutamsikia Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Azimio hili.

MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MSEMADI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Protocol on Peace and Security*).

Mheshimiwa Naibu Spika, amani na usalama ni mahitaji ya msingi kwa ustawi wa Taifa lolote duniani. Ili watu wawze kutulia na kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi, kisiasa na kijamii, wanahitajika kuhakikishiwa usalama ambao msingi wake ni amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba nchi yetu ipo katika historia ya dunia kutohana na kudumisha tunu zake za amani na utulivu, historia hiyo haiondoi ukweli kwamba amani na utulivu katika Mataifa mbalimbali dunia vimeporomoka kwa kiwango kikubwa sana na hivyo kuhatarisha usalama wa watu katika Mataifa hayo. Syo jambo la kubishaniwa kwamba kuongezeka kwa vitendo vyta kigaidi na kiharamia duniani, kuongezeka kwa uhasama kati ya Mataifa, uhasama ambao umesababisha au

matikisiko ya kivita na kuongezeka kwa aina mbalimbali za uhalifu kumefanya hali ya usalama duniani kuwa katika hali tete.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo Mataifa mbalimbali duniani yameanza kubuni mbinu mbalimbali za mashirikiano katika nyanja za ulinzi wa amani na pia namna ya kujilinda na kujihami dhidi ya uvamizi au uhalifu unaoweza kujitokeza katika nchi moja au ukanda ambao uko katika ushirikiano ili kuhakikisha usalama wa wananchi wa nchi washirika unalindwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tanzania imetajwa kuwa ni kisiwa cha amani cha Afrika na kwa kuwa tangu enzi za utawala wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, nchi yetu ilijipambanua kwa kusimamia misingi ya haki, demokrasia na utawala wa sheria, misingi ambayo ndio za amani na utulivu tunaojivunia leo; na kwa kuwa Tanzania ilijitoa mhanga kupigia vita vya kipinga ubaguzi wa aina yoyote, unyonyaji, unyanyasa na dhuluma dhidi ya binadamu mwingine chini ya kauli mbiu ya wakati huo, binadamu wote ni ndugu zangu na Afrika ni moja kwa lengo la kuhakikisha kwamba amani na usalama kwa Waafrika wote vinalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa kuwa nchi yetu iliandika historia wakati wa Serikali ya Awamu ya Kwanza kwa kudiriki kuzitenga hata baadhi ya Serikali za nchi za Kiafrika zilizokuwa hazihestimu utawala wa kisheria, demokrasia na haki za binadamu; hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haipingi wazo au nia ya kuanzisha itifaki hii ya Jumuuya ya Afrika Mashariki kuhusu ushirikiano katika masuala ya amani na usalama kwa kuwa ushirikiano huo utasaidia kuhuisha misingi ya kidemokrasia, utawala wa sheria na haki za binadamu ambayo kwa pamoja huzaa amani, amani ambayo hatimaye huzaa usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu amani na usalama katika ukanda wa Afrika Mashariki viko katika hatari ya kuporomoka kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya baadhi ya Viongozi kutokuheshimu misingi ya

demokrasia, utawala wa sheria na haki za binadamu. Tumeshuhudia baadhi ya nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki wakibadili na wengine wanaendelea kushawishi kubadili Katiba zao za nchi ili waendelee kutawala kwa awamu nyingine kinyume kabisa na Katiba hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha viongozi wengine wamediriki kudhoofisha Upinzani katika nchi zao, Upinzani ambao uko Kikatiba kwa kuwazuia kufanya mikutano ya kisiasa, kuwakamata, kuwashtaki kwa kesi za uchochezi na kuwafunga gerezani baadhi ya viongozi wa Upinzani ili watawale bila kupingwa au kukosolewa na wengine wamediriki kukandamiza uhuru wa habari kwa kuweka Sheria ngumu za Vyombo vyta Habari ili visiweze kukosoa maovu yanayofanywa na baadhi ya Viongozi wa Serikali wa nchi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo niliyoyataja pamoja na mengine ya namna hii huzua chuki kati ya Serikali na makundi mbalimbali ya jamii yanayoona kwamba yanaonewa na matokeo yake ni kuzuka kwa vikundi vyta waasi na hatimaye vita vyta wenyewe kwa wenyewe na katika hatua hiyo amani na usalama vinakuwa vimetoweka kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mambo haya yasiendelee kutokea katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki, Kambi Rasmi ya Upinzani Bunge ina mtazamo kwamba itifaki hii imekuja wakati muafaka na kwamba Bunge liliridhie Itifaki hii. Sababu za kuunga mkono Itifaki hii ni kutokana na umuhimu wa masuala yanayopendekezwa katika Itafiki hii kwa mstakabali mwema wa nchi washirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala hayo ni pamoja na ushirikiano katika usuluhisho wa migogoro baina ya nchi wanachama wa Afrika Mashariki au Mataifa mengine, kudhibiti na kukomesha mauaji ya kimbari, kukomesha ugaidi, kukomesha na kutokomeza uharamia, operesheni za kulinda amani, kukabiliana na majanga, uhifadhi wa wakimbizi, udhibiti wa uingizaji haramu wa silaha, udhibiti

wa uhalifu wa Kimataifa kama vile wizi wa magari, usafirishaji wa magendo uhamiaji haramu, biashara haramu ya binadamu na kadhalika, pia kudhibiti uswagaji wa mifugo kuvuka mipaka na kuingia nchi nytingine na pia kubadilishana mahabusu na wafungwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatoa tahadhari wakati wa utekelezaji wa Itifaki hii kama ifuatavyo:-

Kwamba pamoja na masuala hayo ambayo tunapendekeza Bunge hili liliqidhie, lakini tunatoa wito kwa Bunge na Serikali pia kuchukua tahadhari katika masuala kadhaa kabla ya kuridhia na wakati wa utekelezaji wa itifaki hii inayopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri Bunge hili na Serikali kutoitetea au kuilinda Serikali yoyote ya nchi zinazoridhia Itifaki hii ambayo itakataliwa na wananchi wake kwa kisingizio cha ushirika kupitia Itifaki hii. Azimio hili lisiwe kinga kwa Serikali ambazo zitakuwa zimekataliwa na wananchi wake, kwa maneno mengine hatutarajii kuona Serikali ya nchi moja ikisaidia Serikali ya nchi zingine ndani ya Jumuiya kubaki madarakani kimabavu au kuingia madarakani kwa njia za udanganyifu kwa kisingizio kwamba zipo katika ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendo vyote visivyo vya kidemokrasia vinavyotendwa na Serikali yoyote katika Jumuiya ya Afrika Mashariki lazima vikemewe na vilaaniwe na Jumuiya nzima ya Afrika Mashariki ili kusudio la kuwa na itifaki hii ya Amani ya Kudumu ya Usalama liweze kufikiwa. Hii ni kwa sababu kukirokea vitendo vya baadhi ya Serikali kusaidia au kubebana katika uovu machafu ya kisia ya yatatokea, amani itapotea na hatutakuwa na usalama tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri nchi zitakazoridhia itifaki hii kutokushiriki katika ukandamizaji wa raia wa nchi zao na kusababisha ukosefu wa amani na usalama katika nchi zao, halafu

zikategemea kupata ushirikiano wa ulinzi wa amani kutokana na itifaki hii. Kwa kuwa, itifaki hii inahusu masuala ya amani na usalama basi nchi wanachama ziwe mfano wa kuigwa kwa kudumisha amani na usalama ndani mwao kwanza badala ya kuwa chanzo cha machafuko zenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ili itifaki hii ifikie malengo yaliyokusudiwa na iwe na manufaa ya kudumu katika nchi zitakazoiridhia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba nchi washiriki wa Itifaki hii ziweke kipaumbele zaidi katika mazungumzo ya kidiplomasia katika maeneo yenye migogoro kuliko kutumia nguvu nyingi za kijeshi kulinda amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazishauri nchi zitakazoridhia itifaki hii kupitia mara kwa mara taarifa za makubaliano ya azimio hili na utekelezaji wake ili kuhakikisha hakuna mabadiliko hasi ya Azimio kulingana na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tano, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kuwa, Serikali yetu ihakikishe kuwa inaendeleza na kuziimarisha sababu zinazofanya nchi washirika kukubali kuwa na Azimio hilo ikiwa ni sababu za kisiasa, kiuchumi na kiusalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuweka bayana kwamba mbalimbali na tofauti ndani za kisiasa na baada ya kutoa maangalizo au tahadhari za kuchukua wakati wa kuridhia na kutekeleza Itifaki hii sasa tunakwenda pamoja kama Taifa katika kusaidia utekelezaji bora wa Azimio hili. Ikumbukwe kwamba amani na utilivu tulionao ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kwa hiyo, hatuna budi kuilinda si kwa mitutu ya bunduki bali kwa kutenda haki kwani amani ni tunda la haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia kwa kusema kwamba, kama kweli tunaipenda amani tuliyonayo na kama kweli tunakuwa mfano wa kuigwa na Mataifa

mengine kwa kudumisha amani na utulivu, basi Viongozi wetu waliopewa dhamana ya kuongoza Taifa hili hawana budi kuongoza wa kuzingatia misingi ya demokrasia, utawala wa sheria na kuheshimu haki za binadamu, kutokuoneana haya kwa Viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na wengineo wanaovunja misingi hiyo kwa uchu wa madaraka. Aidha, vitendo vyote vya kibaguzi na vya unyanyapaa wa itikadi tofauti za kisiasa, havina budi kukomeshwa kwa nguvu zote kwani hiyo ndio huzaa chuki na machafuko na hatimaye amani na usalama kutoweka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazihakikishia nchi wanachama ushirikiano katika utekelezaji wa Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, KUHUSU
AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA ITIFAKI YA AMANI NA
USALAMA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (*THE EAST
AFRICAN COMMUNITY PROTOCOL ON PEACE AND
SECURITY*) KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Protocol on Peace and Security*).

Mheshimiwa Spika, amani na usalama ni mahitaji ya msingi kabisa kwa ustawi wa taifa lolote duniani. Ili watu waweze kutulia na kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi, kisiasa na kijamii wanahitaji kuhakikishiwa usalama ambao msingi wake ni amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba nchi yetu ipo katika historia ya dunia kutokana na kudumisha tunu zake za amani na utulivu; historia hiyo haiondoi ukweli kwamba amani na utulivu katika mataifa mbalimbali duniani vimeporomoka kwa kiwango kikubwa sana, na hivyo kuhatarisha usalama wa watu katika mataifa hayo. Si jambo la kubishaniwa kwamba; kuongezeka kwa vitendo vya kigaidi na kiharamia duniani; kuongezeka uhasama kati ya mataifa, - uhasama ambao umesababisha vita au matishio ya kivita na kuongezeka kwa aina mbalimbali za uhalifu kumefanya hali ya usalama duniani kuwa katika hali tete.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo; mataifa mbalimbali duniani yameanza kubuni mbinu mbalimbali za mashirikiano katika nyanja za ulinzi wa amani na pia namna ya kujilinda na kujihami dhidi ya uvamizi au uhalifu unaoweza kujitokeza katika nchi moja au ukanda ambao uko katika ushirikano, ili kuhakikisha usalama wa wananchi wa nchi washirika unalindwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tanzania imetajwa kuwa ni kisiwa cha amani cha Afrika, na kwa kuwa tangu enzi za utawala wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, nchi yetu ilijipambanua kwa kusimamia misingi ya haki, demokrasia na utawala wa sheria – misingi ambayo ndiyo nguzo za amani na utulivu tunaojivunia leo; na kwa kuwa Tanzania ilijitoa mhanga kupigana vita vya kupinga ubaguzi wa aina yoyote; unyonyaji, unyanyasaji na dhuulma dhidi ya binadamu mwingine chini ya Kauli mbiu ya wakati huo ***“Binadamu wote ni ndugu zangu na Afrika ni Moja”*** kwa lengo la kuhakikisha kwamba amani na usalama kwa waafrika wote vinalindwa; na kwa kuwa nchi yetu ililandika historia wakati wa Serikali ya awamu ya kwanza kwa kudiriki kuzitenga hata baadhi ya Serikali za nchi za kiafrika zilizokuwa hazihestimu utawala wa sheria, demokrasia na haki za binadamu; Hivyo, basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haipingi wazo au nia ya kuanzisha itifaki hii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu ushirikiano katika masuala ya amani na usalama; kwa kuwa ushiriakiano huo utasaidia kuhuisha misingi ya demokrasia,

utawala wa sheria na haki za binadamu ambayo kwa pamoja huzaa amani; - amani mbayo hatimaye huzaa usalama.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu, amani na usalama katika ukanda wa Afrika Mashariki viko katika hatari ya kuporomoka kutokana na kuongezeka kwa vitendo nya baadhi ya viongozi kutoheshimu misingi ya demokrasia, utawala wa sheria na haki za binadamu. Tumeshuhudia baadhi ya nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki wakibadili na wengine wanaendelea kushawishi kubadili katiba za nchi zao ili waendelee kutawala kwa awamu nyiningine kinyume na katiba hizo. Aidha, viongozi wengine wamediriki kudhoofisha upinzani katika chi zao; - upinzani ambao uko kikatiba, kwa kuwazuia wapinzani kufanya mikutano ya kisiasa; kuwakamatama, kuwashtaki kwa kesi za uchochezi na kuwafunga gerezani baadhi ya viongozi wa upinanzi ili watawale bila kipingwa au kukosolewa; na wengine wamediriki kukandamiza uhuru wa habari kwa kuweka sheria ngumu za vyombo nya habari ili visiweze kukosoa maovu yanayofanywa na baadhi ya viongozi wa Serikali wa nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, hayo niliyoyataja pamoja na mengine ya namna hiyo, huzua chuki kati ya Serikali na makundi mbalimbali ya jamii yanayoona kwamba yanaonewa na matokeo yake ni kuzuka kwa vikundi nya waasi na hatimaye vita wa wenyewe kwa wenyewe; - na katika hatua hiyo, amani na usalama vinakuwa vimetoweka kabisa.

Mheshimiwa Spika, ili mambo hayo yasiendelee kutokea katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba Itifki hii imekuja wakati mufaka na kwamba Bunge liridhie itifaki hii. Sababu za kuunga mkono itifaki hii ni kutokana na umuhimu wa masuala yanayopendekezwa katika ifaki hii kwa mustakabali mwema wa nchi washirika. Masuala hayo ni pamoja na ushirikiano katika:-

- i. Usuluhihi wa migogoro baina ya nchi wanachama wa Afrika Mashariki na au mataifa mengine.
- ii. Kudhibiti na kukomesha mauaji ya kimbari (Genocide)
- iii. Kukomesha ugaidi
- iv. Kukomesha na kutokomeza uharamia
- v. Operesheni za kulinda amani
- vi. Kukabiliana na majanga
- vii. Uhifadhi wa Wakimbizi
- viii. Udhibiti wa uingizaji haramu wa Silaha
- ix. Udhibiti wa uhalifu wa kimataifa kama vile wizi wa magari, usafirishaji wa magendo, uhamiaji haramu, biashara haramu ya binadamu nk.
- x. Kudhibiti uswagaji wa mifugo kuvuka mipaka na kuingia nchi nyingine
- xi. Kubadilishana mahabusu na wafungwa nk

2. TAHADHARI WAKATI WA UTEKELEZAJI WA ITIFAKI

Mheshimiwa Spika, pamoja na masuala hayo ambayo tunapendekeza Bunge hili liridhie, lakini tunatoa wito kwa Bunge na Serikali pia kuchukua tahadhari katika masuala kadhaa kabla ya kuridhia na wakati wa utekelezaji wa itifaki hii inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza: Kambi Rasmi ya Upinzani inalishauri Bunge hili na Serikali kutoitetea au kuilinda Serikali yoyote ya nchi zilizoridhia itifaki hii ambayo itakataliwa na wananchi wake kwa kisingizio cha ushirikiano kupitia itifaki hii. Azimio hili lisiwe kinga kwa Serikali ambazo zitakuwa zimekataliwa na wananchi wake. Kwa maneno mengine, hatutarajii kuona Serikali ya nchi moja ikiisaidia Serikali ya nchi nyingine ndani ya Jumuiya, kubaki madarakani kimabavu au kuingia madarakani kwa njia za udanganyifu kwa kisingizio kwamba zipo katika ushirikiano. Vitendo vyote visivyo vyta kidemokrasia vinavyotendwa na Serikali yeoyote katika Jumuiya ya Afrika Mashariki lazima vikemewe na vilaaniwe na Jumuiya nzima ya Afrika Mashariki ili kusudio la kuwa na amani ya kudumu na usalama liweze kufikiwa. Hii ni kwa sababu kukitokea vitendo vyta baadhi ya Serikali

kusaidiana au kubebana katika uovu – machafuko ya kisiasa yatatokea, amani itapotea na hakutakuwa na usalama tena.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Kambi Rasmi ya Upinzani inazishauri nchi zitakazoridhia itifaki hii kutoshiriki katika ukandamizaji wa wa Raia wa nchi zao na kusababisha ukosefu wa amani na usalama katika nchi zao halafu zikategemea kupata ushirikiano wa wa ulinzi wa amani kutokana na itifaki hii. Kwa kuwa Itifaki hii inahusu masuala ya amani na usalama; basi nchi wanachama ziwe mfano wa kuigwa wa kudumisha amani na usalama ndani mwao kwanza badala ya kuwa chanzo cha machafuko zenyewe.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu; ili itifaki hii ifikie malengo yaliyokusudiwa na iwe na manufaa ya kudumu katika nchi zitakazoridhia, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba nchi washirika wa itifaki hii ziweke kipaumbele zaidi katika mazungumzo ya kidiplomasia katika maeneo yenye migogoro kuliko kutumia nguvu za kijeshi kulinda amani.

Mheshimiwa Spika, jambo la nne, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazishauri nchi zitakazoridhia itifaki hii kupitia mara kwa mara taarifa za makubaliano ya Azimio hili na utekelezaji wake ili kuhakikisha hakuna mabadiliko hasi ya Azimio kulingana na wakati.

Mheshimiwa Spika, jambo la tano, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa Serikali yetu ihakikishe kuwa inaziendeleza na kuziimarisha sababu zilizofanya nchi washirika kukubali kuwa na azimio hili, ikiwa ni sababu za kisiasa, kiuchumi na kiusalama.

3. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuweka bayana kwamba; mbali na tofauti zetu za ndani za kisiasa; na baada ya kutoa maanganlizo au tahadhari za kuchukua wakati wa kuridhia na kutekeleza

itifaki hii; sasa tunakwenda pamoja kama taifa katika kusaidia utekelezaji bora wa azimio hili. Ikumbukwe kwamba amani na utulivu tulio nao, ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kwa hiyo hatuna budi kuilinda si kwa mitutu ya bunduki bali kwa kutenda haki kwani amani ni tunda la haki.

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kwa kusema kwamba kama kweli tunaipenda amani tuliyonayo, na kama kweli tunataka kuwa mfano wa kuigwa na mataifa mengine kwa kudumisha amani na utulivu basi viongozi waliopewa dhamana ya kuongoza taifa hili hawana budi kuongoza kwa kuzingatia misingi ya demokrasia, utawala wa sheria na kuheshimu haki za binadamu, na kutowaonea haya viongozi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na nyaginezo, wanaovunja misingi hiyo kwa uchu wa madaraka. Aidha, vitendo vyote vya kibaguzi na vya unyanyapaa wa itikadi tofauti za kisiasa havina budi kukomeshwa kwa nguvu zote kwani hivyo ndiyo huzaa chuki na machafuko na hatimaye amani na usalama kutoweka. Mwisho kabisa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazihakikishia nchi wanachama ushirikiano katika utekelezaji wa itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha.

Cecilia Daniel Paresso (Mb)

**Kny. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI KATIKA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
7 Septemba, 2017

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumemaliza mawasilisho sasa tutaanza na wachangiaji. Kwa orodha iliyonifikia hapa mezani Vyama vyote vinavyowakilishwa Bungeni vimelela majina. Kwa hiyo, ninao Wabunge wa CCM, CHADEMA na *CUF*. Tutaanza na Mheshimiwa Tundu Lissu ambaye atachangia kwa dakika 15. Atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Janet Mbene ajiandae ikiwa muda wetu utakuwa umetosha.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia. Naomba niseme kwamba nitachangia hoja ya Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Tume ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe, kati ya Tanzania na Malawi. Kwa sababu ya muda naomba nijielekeze kwenye suala moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba kati ya Tanzania na Malawi juu ya Bonde la Mta Songwe ni Mkataba wa Kimataifa, *it is an International Treaty*, tuanzie hapo. Ni mkataba wa Kimataifa kati ya nchi mbili. Pili, kwa vile ni mkataba wa Kimataifa, mkataba wa Kimataifa huu kama kuna sheria nyingine yoyote ya Tanzania inayokwenda kinyume na matakwa ya mkataba huu wa Kimataifa, mkataba wa Kimataifa unasimama sheria ya nchi inatanguka, *basic International Law 101. (Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kitu ambacho ni muhimu sana na ambacho tunahitaji majibu ya Serikali kuhusiana na mkataba huu wa Kimataifa ni ule unaohusu utaratibu wa utatuaji wa mgogoro chini ya mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 13(3) ya mkataba huu, *The Songwe River Basin Convention*, endapo kutakuwa na mgogoro kati ya Tanzania na Malawi ambao ndiyo wahusika wa mkataba huu, endapo kutakuwa na mgogoro kuhusiana na masuala mbalimbali yanayohusiana na mkataba huu wa Kimataifa, Ibara ya 13(3) inasema mgogoro huo utapelekwa kwenye Mahakama ya SADC; *the parties shall refer the matter to the SADC Tribunal or shall appoint an adhoc arbitrator through mutual agreement which shall be in writing. The arbitrator's decision shall be final and binding on the parties.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikipelekwa kwenye Mahakama ya SADC au ikapelekwa kwa msuluhishi wa Kimataifa, uamuzi wa Mahakama ya SADC au uamuzi wa huyu msuluhishi wa Kimataifa utakuwa ni wa mwisho na utatufunga sisi pamoja na Malawi, sasa shida iko hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa Bonde la Mto Songwe unahusu rasilimali ya maji, unahusu *acquatic resources*, unahusu *water resources*, unahusu *lakes*, unahusu *rivers*. Haya yote niliyoyataja yanajulikana katika sheria, ile sheria ilipitishwa kwa shamrashamra sana humu ndani, ile sheria ya kutangaza mamlaka ya kudumu ya utajiri wa nchi; *The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty Act* iliyopitishwa hapa mwezi Julai. Sheria ile imesema, hizo nilizozisema, rasilimali za maji, vile vitu vilivyoko kwenye maji, samaki *and so on and so fourth, lakes, rivers, everything*, kifungu cha 11 cha sheria ile kimesema kwamba ni marufuku kwa rasilimali hizi zilizotajwa kuamuliwa nje ya Mahakama za Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na Waheshimiwa Wajumbe wajiridhishe wakaangalie kifungu cha tatu cha sheria ile, waangalie na kifungu cha 11(1), (2) na (3) cha sheria ile ili wajiridhishe juu ya hiki ninachokisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo letu la miaka yote na tatizo letu hasa la Bunge hili ni ushabiki usiokuwa na maana yoyote. Tumeruhusu Bunge linapitisha sheria za mambo makubwa bila kuzitafakari, matokeo yake ndiyo haya. Sasa tuna mkataba wa Kimataifa unaosema rasilimali zetu za maji, maziwa, mito, kuhusiana na Bonde la Mto Songwe zitaamuliwa kama kutakuwa na mgogoro katika Mahakama ya *SADC*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wale walioenda *knegotiate* huu mkataba na umesainiwa tarehe 18 ya Mei, hakukuwa na watu wa *Attorney General's Office*, hakukuwa na watu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali? Hakukuwa na watu wa Wizara ya Katiba na Sheria na tuna maprofesa pale! Niliposema *professorial rubbish, this is what I meant*, hawakuwepo? Hawa ambao walileta baadaye hii Sheria ya *Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty)* hawakujua kwamba kuna mkataba umekuwa *negotiated, ume...* (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tundu Lissu, kuna Mheshimiwa Mbunge amesimama. Mheshimiwa Janet Mbene.

T A R I F A

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Mheshimiwa Tundu Lissu anaweza akatoa maoni yake bila kutumia maneno ya karaha. Hana haja ya kutukana, hana haja ya kusema maneno ya hovyo, yeye aeleze kilichocharibika kinachowenza kutengenezwa na nini ambacho kimekosewa ili kifanyiwe kazi. Sidhani kama kuna haja ya kutumia maneno ya kuwaambia wenzake *rubbish* wala chochote.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, / *will not...*

NAIBU SPIKA: Kaa kidogo Mheshimiwa Tundu Lissu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu tunaendelea na huu mjadala na ili tuweze kwenda wote sawasawa, tukumbushane zile Kanuni zinazohusu majadiliano, lakini hata zile zinazohitaji kupata fursa ya kuzungumza ikiwa Mbunge mwagine anazungumza. Kwa hiyo, twende vizuri kwa sababu huu mjadala tunaendelea nao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Maneno ya Mheshimiwa Mbene wala hayahitaji heshima ya kujibiwa, naomba niendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hivi, nimeuliza swali la msingi hapa, huu mkataba umesainiwa tarehe 18, Mei 2017. Je, Mheshimiwa Waziri wa Maji Gerson Lwenge alienda peke yake? Yeye *Engineermambo* ya sheria anaweza asiyafahamu, alikuwa peke yake? Hakupata ushauri wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali? Hakupata ushauri wa Waziri

wa Sheria? Wale walioleta Sheria hii ya *Permanent Sovereignty over Natural Wealth* hawakujua matakwa ya mkataba huu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, matokeo yake nimezungumza na nitaendelea kuzungumza tena, matokeo yake ni aibu hizi! Mmetunga sheria miezi miwili iliyopita, leo mnaleta mkataba mnatunga sheria nyingine ya kuitengua na mtaitengua. Waheshimiwa Wabunge, nawaomba sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili la mgongano kati ya sheria inayosema maliasili na utajiri wa nchi yetu ushughulikiwe na Mahakama zetu uko vilevile kwenye Mkataba amba unakuja kesho wa Bomba la Mafuta, kaangalieni. Mkataba wa Bomba la Mafuta unasema tukigombana Uganda na Tanzania kwa sababu ya bomba la mafuta mgogoro ule unaenda kuamuliwa London na hawa amba wanajifanya ndio watetezi wa rasilimali za nchi hii, hatuoni! (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, nawaombeni, mimi nina maneno makali sana, lakini nani aniambie kama haya ambayo tumeyapitisha yako sahihi. Aniambie haya ninayoyasema ni ya uwongo, kwamba hatujaleta mkanganyiko wa kisheria hapa, kama tumeleta mkanganyiko wa kisheria tunatunga mkataba wa Kimatalifa, tunapindua kile tulichokipitisha hapa kwa majidai mengi. Tunakitengua miezi miwili baadaye, sisi ni watu wa aina gani? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, hasa Waheshimiwa Wabunge mlion wengi, narudia tena wito wangu, haraka haraka haina baraka, maangamizi ya Taifa hili na maanguko ya Bunge hili ni hicho kinacholetwa kila leo kwa hati ya dharura. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim atafuatiwa na Mheshimiwa Janet Mbene.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Tunagawana muda na Mheshimiwa Hamidu Bobali, nusu kwa nusu, sijui dakika ngapi, sijaelewa ni 10 au 15.

NAIBU SPIKA: Kama mnagawana maana yake wewe ni saba na nusu na yeye saba na nusu. Ama wewe saba mpe yeye nane, ama wewe nane yeye saba. Kwa hiyo, kubalianeneni kwanza useme hapo ili Katibu aweke vizuri.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongea dakika nane na Mheshimiwa Bobali ataongea dakika saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nami nitajielekeza kwenye Azimio moja tu ambalo ni Azimio la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuia ya Afrika Mashariki (*East African Community Protocol on Peace and Security*). Katika muktadha wa shughuli nzima za ulinzi na usalama na jinsi ambavyo *articles zilivyokuja*, naomba nianze na Article 12 ambayo inasema *combating trans-national and cross border crimes*. Katika mambo ambayo yameelezwa, sitaki nisome sentensi zote lakini nataka niende kwenye ile (e) *illegal migration* (uhamiaji haramu).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika dhana nzima hii ya uhamiaji haramu, imeonekana kwamba wakati tukiweza kupitia Azimio hili kuridhia Azimio hili, naunga mkono Azimio hili lakini tuangalie ni kwa jinsi gani kwa muda mrefu, pamoja na vipengele vilivymo katika Azimio hili, vyta kuweza kuchukua taratibu, sheria na kanuni, lakini tuangalie ni kwa nini baadhi ya wahamiaji haramu wanaotoka Eritrea, Ethiopia, Somalia wanafika kwetu Tanzania ilhali wanapita katika nchi ya Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo hapa ya kujifunza, tunataka kwenda katika utaratibu ambao tunataka kwenda vizuri na wenzetu kuona kwamba kuna hatua ambazo zitachukuliwa, kuna mikakati ambayo

itafanywa, lakini wasiwasi ambao unakuja hapa sasa ni mahusiano, maelewano ya ziada katika shughuli nzima ya kutoka wahamiaji haramu kutoka Eritrea, Ethiopia, Somalia wanaopita Kenya kuja kwetu. Naomba hilo liwe angalizo kubwa katika mkataba wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda katika *Article 13; preventing and combating cattle rustling*, ule wizi wa mifugo. Katika shughuli nzima hii ya wizi wa mifugo kumekuwa na operesheni nydingi sisi wenyewe kwanza hapa. Tulikuwa na Operesheni Tokomeza ambayo ukiangalia Ukanda ule wa Kigoma kulikuwa na mambo mengi, lakini katika maeneo mengine ambayo viongozi hasa wa mipakani walio katika maeneo yale ya wafugaji, wamekuwa wakipata matatizo sana na malalamiko sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutekeleza itifaki hii na kuiridhia inaonekana viongozi walioko mipakani, Watendaji wa Vijiji, Viongozi wa Chama, sisemi ni chama gani lakini inaonekana wale walio wengi zaidi kwa sababu ndio waliopata ushindi katika maeneo haya wengi wanapata, chama hicho, sitaki kutaja kwa sababu nikitaja itakuwa ni ukakasi, wataanza mambo ya hapa na pale lakini hili ni tatizo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Viongozi hawa wanapokea rushwa, viongozi hawa ndio wanaoingiza mifugo, tumesema mara nydingi lakini bado Serikali imekuwa ikitisimia kwamba itachukua hatua hii, utaratibu unakwenda, tuna mipango kabambe, mikakati hapa na pale, lakini hakuna kitu. Hilo ni tatizo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kuridhia mkataba huu, mimi sina pingamizi nimesema naunga mkono kabisa, lakini tuangalie jambo lingine, tunakwenda kuridhia itifaki hii, lakini tuna tatizo kubwa la urejeshaji wa alama za mipaka (*beacons*). Hili suala ni la ulinzi na usalama, amani na utulivu. Mheshimiwa Shamsi anajua, Mheshimiwa Hussein Mwinyi anajua na wengine wanajua. Tuna tatizo kubwa la urejeshaji wa mipaka katika maeneo mbalimbali,

ripoti kadhaa zimesema kwamba baina ya Tanzania pale Tarime na Migori Kenya *beacons* zimeondolewa kwa muda mrefu, Serikali inasema tuna mkakati, suala hili ni mtambuka, itachukuliwa hatua hapa na pale, hakuna kitu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetaja maeneo, kuna Vijiji vya Panyakoo, Ronche, Ikoma, leo kila wakati unasi kia kwamba *beacons* zimeng'olewa, zimeondolewa, lakini utaratibu maalum haupo. Sasa tunakwenda kwenye Itifaki hii lakini kuna mambo sisi wenyewe kwanza kwa kuwa mambo haya ni mtambuka, Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Mambo ya Ndani, TAMISEMI, Mambo ya Nje, zote tukae kwa pamoja katika nchi hizo husika wakati tunakwenda kuridhia itifaki hii kuweka utaratibu wetu, hili jambo likae vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana inaonekana kama tunasukumwa tu, kwanza tumechelewa. Tangu tarehe 12, Machi iliposainiwa tumekaa miaka minne, tumbakia sisi na Burundi tu, sisi Watanzania ni watu wa mwisho tu, kuna mambo kidogo ya kujifunza hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo haya ambayo tunakwenda nayo, basi napenda kusema kwamba Msemaji wa Kambi ya Upinzani alisema kwamba ni vema nchi zetu za Kiafrika ziendelee kujifunza katika kudumisha amani na utulivu katika mambo ya demokrasia pale ambapo mmoja kashindwa akubali matokeo. Unafuta uchaguzi, kwa nini ufute uchaguzi? Kwa mantiki ipi, kwa dhana ipi? Kwa manufaa ya nani? Umeshindwa kaa pemberi kwa sababu hakuna mwenye hatimiliki ya kuongoza, nchi ni yetu sote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo amesema Msemaji wa Kambi ya Upinzani, namshukuru sana Msemaji, Mheshimiwa Cecilia Paresso, amesema jambo kubwa kweli, jambo zuri, jambo jema, amewaambia kwamba katika kudumisha amani na utulivu katika demokrasia hizi za mfumo wa Vyama vingi pale ambapo mmoja atashindwa basi akae pemberi, ni jambo jema sana, na hili tupate kujifunza katika maeneo mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, bila kupigiwa kengele ile ya mwisho, nashukuru sana na naunga mkono Azimio hili la Amani na Usalama, lakini amani iwe ya kweli, isiwe ile amani ya kuigiza igiza. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masoud, baada yako nilimtaja Mheshimiwa Janet Mbene, lakini Waheshimiwa Wabunge tunapojadili humu ndani lazima tujue pamoja na kwamba huwa tuna masihara ya hapa na pale, lakini tusilet mtafaruku kwenye mambo ambayo nchi husika ndiyo inayopaswa kujua nini cha kufanya. Hili lilitotajwa la mfano, Katiba yao ndivyo inavyosema. Kwa hiyo, tuwaache wamalize mambo yao salama, wao wenyewe waliamua hivyo na ndivyo inavyofanywa huko kwao, tuwaachie. Lakini nje tukitoka hapo tunaweza kujadili ila humu ndani hayo tuyaache yasije yakatuma ujumbe ambao uko tofauti kidogo huko nje.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea. Mheshimiwa Masoud anajaribu kusema amemkumbuka sana Jecha.

Mheshimiwa Janet Mbene, kama muda utakuwa bado upo atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Mbogo. Hakuna aliyerukwa, kila mtu atachangia, kwa sababu hata CHADEMA kuna ambao wamegawana dakika saba na nusu na sijawaita, kwa hiyo msitie shaka muda wako uko palepale.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami napenda kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Kwanza naipongeza Serikali kwa kuleta hili Azimio hapa Bungeni kwa sababu hili suala la mradi wa Bonde la Mto Songwe ni la muda mrefu lakini sasa naona linafikia tamati na inasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kupongeza Serikali kuwa sasa hivi pia imeongeza wigo wa zile Wilaya ambazo zitaguswa na mradi huu au programu hii kutoka zile mbili za mwanzo iliyokuwa lleje na Kyela, sasa

mpaka Momba, Mbozi na Mbeya Vijijini, kwa hiyo hii vilevile italeta manufaa zaidi kwa wananchi wa sehemu hizo za Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vilevile kuzungumzia kuwa kwa kweli hii programu imekuja wakati mzuri, kwa sababu kwa muda mrefu sana Mto Songwe umekuwa ukisumbua sana pale ambapo kunakuwa na mafuriko ambayo yanaletea kingo zake kuleta madhara mengi sana ya kimazingira pia kuharibu miundombinu ya eneo husika na kwa kudhibiti sasa hivi itatusaidia sana kuhakikisha kuwa Mto Songwe unadhibitiwa lakini vilevile unatumika vizuri zaidi kiuchumi kulinda mazingira, vilevile kuboresha maisha ya wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na maendeleo hayo inaonekana kuwa programu hii pia itasababisha ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya barabara, vituo vy'a afya, elimu na masuala ya utalii. Napenda kutoa rai kwa Serikali kuwa wakati wanapofikiria kufanya miradi hii basi wazingatie miradi au mipango ya miradi iliyoko pale kwenye eneo hilo ili tusiwe tuna miradi ambayo inakwenda sambamba wakati kuna haja ya kumalizia ile iliyopo ili tusiletie ile *duplication* au kuzidisha ukiritimba kwenye shughuli za maendeleo za eneo husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda sana kutoa rai kwa Serikali juu ya kuhusisha wadau muhimu. Kwa sababu hata hapo nyuma ambapo mradi ulikuwa umefikiriwa kufanya, kuna wananchi mpaka leo walikuwa wameambiwa kuwa maeneo yao wasiyatumie kwa sababu mradi utapita, kama mnavyojua ni miaka mingi tangu wazo liwekwe na wamekuwa kwenye hali ya sintofahamu wakisubiri nini kinaendelea. Kwa hiyo, safari hii tutakapomaliza kuridhia na itakapoanza kufanya hii programu basi wananchi wafahamishwe, Halmashauri husika zihusishwe moja kwa moja ili sasa wananchi watambue ni nini kitakuja kuendelea katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia

masuala ya kujifunza kutoka kwenye matokeo ya miradi mingine ya haya mabonde, tumesikia hapa kuwa kulikuwa kuna mabonde kama tisa nchini ambayo yamekuwa na miradi lakini yamekuwa na ufanisi ambao wakati mwingine sio mzuri sana. Sasa hii ingekuwa ni fursa nzuri kwa mradi huu na wenyewe kuangalia jinsi gani watajifunza tusiingie tena katika matatizo yale ambayo yaliingiwa katika miradi ya huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Ruaha tunajua jinsi ambavyo shughuli za kibinadamu zimeathiri sana mto ule na mpaka sasa hivi unaathirika hata kina chake na kwa hiyo inaleta shida. Sasa na huu mradi nao ukaangaliwe katika mtazamo huo na zile Wizara zote ambazo zinahusika katika mradi huu basi ziwe na ushirikiano wa karibu ili kila mmoja asimame katika nafasi yake kuhakikisha kuwa mradi huu unakuwa wa manufaa kuliko kuwa wa hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala amelizungumzia Mheshimiwa Lissu pale ningependa kusema pamoja na kuwa amelizungumza kwa njia ambayo haikufurahisha basi likaangaliwe, ingawa mimi kwa uelewa wangu mdogo ingawa siyo Mwanasheria, huu ni mradi ambao unahusisha rasilimali zinazogusa nchi mbili. Kwa hiyo, naamini kutakuwa na makubaliano mazuri ya jinsi gani ya kusuluhisha usimamizi wake na sikuona kama kulikuwa kuna sababu ya kutoa maneno makali ambayo kwa kweli hayajengi.

Mwisho kabisa nataka kupongeza sana na kuomba Waheshimiwa Wabunge turidhie Azimio hili kwa sababu linakwenda kujenga na kuboresha miundombinu na rasilimali hii nzuri itatumika vizuri zaidi kuliko jinsi ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Janet Mbene. Mheshimiwa Richard Mbogo nilikuwa nimekutaja, kama muda utakuwa umebaki atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Kakoso.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa hii nafasi. Kwanza nitoe tu hoja kwamba Wabunge na Bunge zima tuunge mkono hizi hoja mbili ambazo zimewasilishwa ya kuhusu Bonde na hili la Amani na Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na hili Azimio la Bonde la Songwe, napendekeza kwamba kwa ujumla wetu tuangalie umuhimu wa haya mabonde. Sehemu kubwa, watu bado hawajatambua kwamba umuhimu wa bonde uko kwa kiasi gani katika nchi, tunaangalia kuyalinda mabonde kwa kwanza kuangalia vyanzo vyetu nya haya mabonde ne mito yote. Tumekuwa na sehemeu kubwa sna ya uharibifu wa mazingira ambapo imepelekea mtu wa chini hafaidiki tofauti na mtu wa juu, kwa lugha nyepesi ya kigeni wanaita *upstream* na *downstream users*. Sasa kwa kuweka huu mkataba kati ya nchi mbili tunaona kwamba kutakuwa na usawa katika utumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la Bonde hili pia linakwenda kutujengea ushirikiano mzuri kati ya nchi hizi mbili, kati ya Malawi na Tanzania, kwa hapo nyuma kuna maneno yalishapita ya mtaani ambayo yalikuwa siyo mazuri lakini tunatumaini sasa kwa Mkataba huu ambao umesainiwa na matumizi haya ya bonde na faida zake zote ambazo zimeelezwa na Waziri mwenye dhamana, tunatumaini kwamba tutafaidika kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida ya kwanza ambayo nimeiona kwanza ni ushirikiano ambapo tutakuwa kwa pamoja na ukiangalia katika mipaka yetu watu wanafanana tamaduni na lugha, kwa hiyo ushirikiano utaendelea kuimarika.

Lingine ambalo naona litakuwepo ni suala zima la kiusalama. Nchi mbili mnapokuwa mmeshirikiana katika shughuli za kiuchumi kama hili ambalo tumesaini maana yake tutakuwa na uelewa wa pamoja, tutakuwa na usalama kati ya nchi na nchi, kwa hiyo, tunapongeza sana Serikali kwa kufanya hii jitihada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho ningesema ni kwamba tuhusishe pia Wizara yenyeye dhamana upande wa Mazingira, iendelee kuititia Sheria zake za Mazingira kuendelea kulinda vyanzo vyote ambavyo vinakwenda kwenye hili bonde, tumeona kwamba nchi sasa hivi imezungukwa sana na shughuli za kiuchumi ambazo hazizingatii sana Sheria ya Mazingira, ile mita 60 kutoka kwenye kingo za mito, mita 500 kutoka kwenye vyanzo vyta maji na Serikali imekuwa inahimiza sana. Kwa hiyo, naomba sana Wizara inayohusika na mazingira waendelee kulinda haya mabonde yote katika nchi yetu ili vizazi na vizazi ambavyo vinafaudia viweze kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hii nita-*comment* kidogo kwenye *Commission*, tuombe Wizara inayohusika iangalie *Commission* ambayo imeundwa, waangalie matatizo ambayo yamewahikutokea, kwa mfano TAZARA ambapo kwenye upande wa reli kati ya Tanzania na Zambia, waangalie changamoto zilizopo upande wa TAZARA na upande wa huku sasa hii *Commission* ambayo imeundwa zisiweze kujirudia na utendaji wake uwe wenyet tija na ufanisi. Kwa hiyo, tunaomba sana na hata *staffing* yenyewe izingatie kama mkataba vile ulivyo na namna bora ambayo wataona ni ya kuboresha na itapendeza zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeelezwa faida nyingi na mimi napendezwa sana kuona kwamba litajengwa bwawa na tutaweza ku-*control* mafuriko ambayo huwa yanatokea na tutaweza kupata umeme, shughuli za kiuchumi zitawezza kufanyika. Naunga mkono na naomba Wabunge wote tuunge mkono Azimio hili ambalo ni muhimu sana kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia Azimio hili la bonde la Mto Songwe, naomba nigosie pia na kuhusiana na kuridhia Itifaki, Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kiujumla Tanzania ni nchi ambayo ilijengwa kwa misingi mizuri na hasa Rais wetu wa kwanza, Hayati Julius Kambarage Nyerere alitengeneza amani kubwa sana katika nchi yetu ya Tanzania na vitu vingi aliweza

kuviondoa. Kwa mfano; aliondoa utawala wa Kichifu ikapelekea nchi inakuwa inatawalika vizuri, ukabila vyote hivyo vimeduwa vimesaidia sana Tanzania tumekuwa na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nchi yetu Tanzania ilipokea sana Wakimbizi kutoka nchi za jirani ambazo ni Congo, Burundi, Rwanda yote yalitokea kwa sababu wenzetu hawakuwa na amani. Sasa kwa misingi ya maazimio haya ambayo yanaletwa na tayari tuko kwenye Umoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki maana yake tutajikita kwenye haya maazimio ambayo yatakuwa yamesainiwa kwa ajili ya amani na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wanapokuwa hawana amani matatizo yale yanaleta migogoro katika nchi yetu ikiwa ni pamoja na kuja kwa wakimbizi, imetokea matukio wamekamatwa na silaha katika Kambi za Wakimbizi na wengine matukio ya kiujambazi, sasa kwa minajili hiyo kwa kulinda amani itatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ya nchi za jirani kuna Tume zimewahi kuundwa, kuna mojawapo Rais Mstaafu Benjamin Mkapa amekuwa Mwenyekiti, Hayati Nelson Mandela amewahi kuwa Mwenyekiti, marehemu Hayati Mwalimu Nyerere amewahi kuwa Mwenyekiti katika kusuluuhisha nchi za jirani kwa kutokuwa na amani. Nchi nydingi duniani zinasumbuliwa na masuala ya ugaidi, kwa hiyo tunavyokuwa na umoa kama Jumuiya ya Afrika Mashariki, tutaweka msimamo wa kulinda amani na wananchi wake wote watakuwa kwenye hali ya utulivu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja zote hizi mbili na nawashawishi Wabunge wote tuziunge mkono. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso kama na yeche atakuwa amechangia muda mfupi basi tutamaliza na Mheshimiwa Pascal Haonga

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kunipa nafasi hii kuchangia maazimio ambayo yamewasilishwa kwenye Bunge hili. Kwanza ninapongeze kwa uwasilishaji ambao wawasilishaji wote wameyaelezea kwa ufasaha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la amani suala la msingi sana katika nchi yetu. Ili nchi iweze kufanya kazi vizuri ni sharti tuwe na amani ya kutosha, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri alipokuwa anawasilisha ni vema sasa kama Bunge tuli-*support* Azimio hili kwa ajili ya kulinda amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sisi tunaoishi mipakani bado kuna shida kubwa sana ya Watanzania ambao wengine wanaishi bila kuwa na uhakika mzuri wa maisha yao, tunaiomba sana Serikali iimarishe suala zima la ulinzi na usalama hasa maeneo ya mipakani. Mimi natoka Mkoa wa Katavi ambao tumepakana na Ziwa Tanganyika pia nchi ya Congo tumepakana nayo. Wapo Watanzania ambao wanaishi mazingira ambayo siyo sahihi. Naomba sana Serikali iweze kuangalia mazingira hasa nchi zile zinazopakana na Maziwa kama ilivyo Mkoa wa Katavi, Rukwa na Kigoma maeneo haya tunahitaji sana kuweka ulinzi shirkishi katika nchi zote tunazopakana nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania ni watu wakarimu, tumeweza kuwapokea wananchi wa Mataifa mbalimbali kama Congo, Burundi lakini mazingira tunayoishi kule ni mazingira ambayo Serikali inahitaji kuweka ulinzi shirkishi ili kupunguza haya matatizo ambayo yanaweza yakajiteza. Naipongeza Serikali kwa Azimio lilioletwa, naamini litakuwa suluhisho kwa nchi zote za Afrika Mashariki na zile ambazo ziko nje ya Afrika Mashariki kama DRC-Congo tuweze kuazimia yale ambayo yamewekwa ili yawe na tija kwa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni juu ya Bonde la Mto Songwe. Bonde la Mto Songwe, Azimio lilioletwa ni muafaka lakini lina mazingira ambayo yanafanana na maeneo mengine. Nizungumzie maeneo ya Mkoa wa Katavi.

Tunayo mabonde ambayo yametoka, tuna mito ambayo imetoka maeneo ya kwetu na imeenda mpaka nchi ya DRC-Congo, tuna Mto Lwegere ambaao umevuka Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna madhara ya suala zima la mazingira. Upande wa Congo, Ziwa Tanganyika linapeleka maji ambayo yanaleta athari kwa nchi yetu, sasa ni vema tunapoweka mikataba hii tuangalie na maeneo mengine ambayo kimsingi yanaweza yakachangia suala zima la maendeleo na suala zima la mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nje ya hapo tuna Mto Nile ambaao unatoka Ziwa Victoria. Ni vema sasa tuangalie mazingira ambayo yatakuwa ni mazuri kwa nchi yetu, kuwatengenezea mazingira mazuri hasa Watanzania. Mfano, Mto Nile ni mto ambaao unatoka kwenye maeneo yetu lakini Wamiliki wakubwa wa Mto Nile ni wenzetu watu wa Misri, ni vizuri tukaangalia maeneo haya, tukayapitia upya ili yawe na manufaa kwa Watanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mazingira ni suala ambalo linahitaji sasa liwekewe kipaumbele na Wizara husika ili tuweze kulinda Mabonde na mito ambayo kimsingi inahama. Bonde la Mto Songwe linahama na ndiyo maana limeletwa hapa kwa sababu mipaka huwa inahama kutoka sehemu moja hadi sehemu nyingine, lakini bado kwenye maeneo yetu ya ndani, leo hii tunapozungumzia mabonde haya ambayo chanzo ni uharibifu wa mazingira, tuna Mto Katuma ambaao unapeleka maji kwenye hifadhi ya Katavi na unapeleka maji mpaka kwenye Ziwa Rukwa, leo hii Ziwa Rukwa linapoteza thamani yake na upo uwezekano wa kutoweka kabisa, ni kwa sababu hakuna ulinzi mzuri wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Waziri mwenye dhamana aendelee na jitihada ambazo zitatengeneza mazingira mazuri ili kujenga mikakati ya kulinda suala zima la mazingira, lakini cha kufurahisha kwenye Azimio hili ni juu ya mpango wa uwezeshwaji wa kiuchumi

kwenye maeneo yote. Tuwaombe sasa Wataalam waweze kushughulikia uhalisia wa kutengeneza mazingira ambayo yatalinda hadhi ya Watanzania waweze kuwezeshwa kiuchumi ili waweze kuendana na uhalisia wa mabonde haya ambayo wamezungukwa nayo kwenye maeneo ya mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuwaombe sana wataalam wetu watengeneze mazingira ya kisheria yatakayolinda nchi yetu ili Watanzania na wale ambao wanazunguka katika maeneo hayo wawe na faida na haya Maazimio tunayoyakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Pascal Haonga ambaye ana dakika saba na nusu na nadhani hizo zinakamilika pale. Mheshimiwa Haonga.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, hayupo.

NAIBU SPIKA: Hayupo eehh?

MBUNGE FULANI: Ndiyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ryoba Chacha dakika Saba na nusu.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nami niweze kuchangia Itifaki hii naomba nianze na hii Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kuipitia vizuri na nimeilewa ni nzuri. Sisi kama nchi tunapaswa kuiridhia lakini kuna mambo machache ningetaka niseme, kwamba kuna nchi zimejingga na zingine hazijajunga na kwa kuwa Itifaki hii lengo lake ni kutatua migogoro ndani na nje ya nchi wanachama, kuzuia mauaji ya kimbari, kupambana na

ugaidi, kupambana na uharamia na kadhalika ni jambo zuri sana. Hata hivyo, nchi hizi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaongozwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi zao na Katiba hizi zimetoa haki kadha wa kadha, lakini unakuta katika nchi hizi, viongozi ambao wako madarakani wanaamua kukanyaga Katiba ya nchi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba imetoea fursa ya demokrasia, Katiba imetoea fursa ya uhuru wa mawazo, Katiba imetoea fursa ya uhuru wa kujieleza, Vyama vyta Siasa na kadhalika, anatokea mtu anakwenda kinyume na Katiba, huyu mtu siyo gaidi? Kwa hiyo, gaidi siyo wale wa kuvamia peke yake ni pamoja na viongozi wanaokwenda kinyume na Katiba ya nchi, wanaokwenda kinyume na sheria ya nchi. Kwa hiyo, nimefurahi kuona hii Itifaki kwamba pamoja na wale wanaozuia vyama vyta siasa visifanye mikutano kwa mujibu wa sheria itawashughulikia, nimefurahi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni vizuri mfahamu kwamba, amani siku zote ni tunda la haki. Kama viongozi wa nchi hizi ambao wako madarakani hawataki kutenda haki, hakutakuwepo na amani, ni vizuri tufahamu Muasisi wa amani ni Mungu mwenyewe. Kama viongozi wa nchi hizi ambao wako madarakani wanawaona wananchi wenzao hawana haki ambayo haki imetolewa kwa mujibu wa Katiba, Mungu atawahukumu siku moja na namshukuru Mungu ameanza kuwahukumu wengine leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi kama Mheshimiwa Ryoba ninaikubali hii Itifaki iko sawa sawa, Bunge liridhie ili wale viongozi wanaokwenda kinyume na Katiba ya nchi, kuzuia vyama vyta siasa visifanye mikutano kwa mujibu wa sheria waweze kushughulikiwa na umoja huu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. (*Makof!*)

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lucy taarifa.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, tunachochangia hapa kilichopo mbele yetu ni kitu kingine, lakini Mheshimiwa Mbunge anazungumza jambo lingine kabisa ambalo haliko mbele yetu. Naomba ajikite kwenye mada kwa sababu hicho anachokiongea hapa siyo mahali pake na wala hayo anayoyaongea siyo ya kweli. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ryoba Chacha unapokea taarifa hiyo?

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mtu hata hajasoma Kanuni, kwanza hajui Kanuni, lakini la pili hii Itifaki inaongelea amani na ukisoma ndani yake kuna kuzuia ugaidi, mauaji ya kimbari, nini *source* ya mauaji ya Kimbari? Ni Viongozi walio madarakani kutokutenda haki. Fuatilia kule Rwanda na Burundi nini kilitokea? Viongozi wallikuwa madarakani hawakutenda haki. Msipotenda haki kunaweza kukatokea mauaji ya kimbari, kwa hiyo ni vizuri haki itendeke ili watu wote wawe na amani. Msipofanya hivyo haina maana, ndiyo maana nikasema hii ni nzuri sana, kwa sababu itawazuia wale viongozi ambao hawatendi haki kwa wenzao. (*Makofi*)

Jambo lingine nilitaka niongelee hii *Commission* ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe. Pamoja na Mbunge wa Singida Mashariki Mheshimiwa Tundu Lissu ametoa tahadhari hapa kwa sheria iliyopitishwa. Pia niungane naye kwamba ni vizuri jambo hili liangaliwe vizuri ingawa maudhui ya Itifaki hii ni mazuri sana kwa sababu jambo hili kimsingi lilitakiwa lifanyike muda mrefu sana kwa ajili ya kutoa manufaa kwa wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo pia mabonde mengi sana, kuna Bonde la Mto Rufiji, kuna Bonde la Mto Mara na Mabonde mengine ambayo kama mabwawa yangetengenezwa, kilimo cha umwagiliaji kikafanyika, wananchi wa maeneo husika wangepata faida kubwa sana. Kwa hiyo, pamoja na *weakness* za kisheria ambazo zimeonekana, ambazo naamini kupitia Bunge hili mtazipitia mkaangalia nini kinaweza kufanyika ili *Commission* hii iweze

kutekelezwa, lakini kimsingi maudhui yake ni mazuri lakini angalizo kubwa ni mgogoro wa mpaka.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha Bunge cha Asubuhi. Kabla sijasitisha shughuli za Bunge, niwakumbushe tena kuhusu michango hasa ile inayozungumzia nchi nytingine. Mheshimiwa Ryoba mambo uliyokuwa unayasema sijajua wewe umesoma historia kiasi gani kuhusu nchi hizo, lakini ni mambo mazito kwenye nchi hizo balaa! Sasa sisi hapa tunazungumza kana kwamba ni mchango wa kuufanyia mfano kirahisi namna hiyo, haya mambo hata kwao yametungiwa sheria namna ya kuyazungumza. Kwa hiyo, tusiyachukulie kirahisi sana tukaonekana Bunge la nchi hii kuna namna labda inayajadili mambo yale kinyume na Katiba zao lakini na taarifa zile ambazo wao wanazo kule kwao.

Waheshimiwa Wabunge, ningewaomba sana tujikite kwenye yale ya kwetu sisi, kama tunatumia mfano wa nje tutumie kwenye yale wanayofanya vizuri kwa sababu kila mtu atataka kusikia anavyofanya vizuri, lakini kwenye yale ambayo hayajakaa vizuri huko kwao tuwachie wao kama wanavyotuachia ya kwetu. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo, niwataje Waheshimiwa Wabunge watakaopata fursa ya kuchangia mchana; Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, Mheshimiwa Pascal Haonga na Mheshimiwa Hamidu Bobali.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni leo.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilsitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Kabla hatujaendelea, baadhi yenu mnaweza kuwa mmeputa taarifa kuhusu Mheshimiwa Tundu Lissu kushambuliwa kwa risasi mchana huu. Mpaka sasa kama Bunge, Mheshimiwa Spika yuko hospitali na vyombo vyaa usalama pia vinafanya kazi yake. Kwa hiyo, naomba kwa wakati huu tumwombee mwenzetu, Madaktari wanapoendelea kufanya kazi yao naye apate ahueni.

Nadhani Mheshimiwa Spika atakapomaliza huko tutapata taarifa, aidha mchana huu ama kesho asubuhi. Tuendelee kuwa watulivu kwa hili liliolmpata mwenzetu, kama nilivyosema tuendelee kumwombea ili afya yake irejee. Yoko hospitali, Madaktari wanaendelea kumshughulikia, vyombo vyaa ulinzi na usalama vinafanya kazi yake nasi Waheshimiwa Wabunge tuendelee kumwombea mwenzetu.

Baada ya kusema hayo, tutaendelea na kilichopo mbele yetu. Kama kuna jambo litakaloifikia meza, basi mtataarifiwa.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimetaja majina kadhaa ya watu watakaochangia mchana huu. Kwa hiyo, nitaanza kuita kwa kadri ninavyoona watu walioko humu ndani kwa sasa. Mheshimiwa Rashid Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Njeza halafu Mheshimiwa Esther Michael Mmasi ajiandae.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami nachukua nafasi hii niungane na Waheshimiwa Wabunge pamoja na Mheshimiwa Spika, kutoa pole kwa mwenzetu kwa jambo ambalo limempata na tunamuomba Mwenyezi Mungu amjaalie ili afya yake iweze kurejea katika hali ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami nitoe mchango mbele ya Bunge lako Tukufu juu ya Azimio la Bunge kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa Kamisheni ya pamoja ya

Bonde la Mto Songwe sambamba na kuridhia Azimio la Itifaki ya Amani na Usalama kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya hivi karibuni suala la maji limekuwa ni suala ambalo linaleezwa kuweza kusababisha Vita Kuu ya Tatu ya Dunia. Maji yamekuwa ni tatizo, lakini chanzo kikubwa cha ukosefu wa maji ni uharibifu wa mazingira. Pamoja na mabadiliko ya tabia nchi ambayo kimsingi yanashahibiana moja kwa moja na mabadiliko ya tabia za binadamu hasa pale ambapo tunaharibu mazingira, basi maazimio kama haya yakija kwenye Bunge letu Tukufu, hakuna namna zaidi ya kuridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai tu kwamba pamoja na nia nzuri ya Serikali kuridhia hili, lakini sasa iwe ni mwanzo wa changamoto pia kuhifadhi mabonde mbalimbali yaliyoko katika Taifa letu. Kwa mfano, tumeona hivi karibuni kulikuwa na wadau wa Bonde la Mto Ruaha Mkuu lakini pia kule Mkoani Rukwa na Katavi kuna bonde pia, nimeona Mheshimiwa Waziri anayehusika na mazingira walikuwa wanafuatilia pia uhifadhi wa lile bonde; na kuna mabonde mengine kama Malagarasi, bonde la Mto Pangani nayo pia bado hayako katika hatua nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitoe rai kwamba tunapokwenda kuridhia mikataba hii ya Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe kwa maana kwa nchi ya Tanzania na Malawi, basi pia tuone umuhimu wa kuangalia kwa mapana haya mabonde mengine ambayo yanazunguka katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai, kama ambavyo kwenye Kamati wameshauri kwamba nchi yetu haikuwa na mahusiano mazuri sana na Malawi hasa katika eneo hili la ziwa, lakini nadhani kwamba itifaki hii iende pia kuamsha ari mpya katika kutengeneza mahusiano, siyo tu ya kidiplomasia lakini ya kiuchumi, ya kijamii na ya kimazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba mkataba huu ukiridhiwa utoe tija ambayo inategemewa kwa

wananchi wa pande zote mbili. Pia ni kipaumbele kwamba kwa kuwa hata Mkoa huu wa Songwe ni mkoa mpya, tunaamini kwamba fursa mbalimbali zitakazopatikana kuititia uanzishwaji wa hii Kamisheni utasaidia hata kusukuma maendeleo mengineyo hasa katika Sekta za Kilimo na uzalishaji wa umeme; tumeona hapa takriban *megawatt* 180 zinaweza zikazalishwa kuititia bonde la Mto Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ambayo naiona ni suala zima tu la eneo kwa wananchi juu ya utunzaji wa jumla wa mazingira hasa tunavyoona kwamba mto huu unatirisha maji kuelekea katika Ziwa Nyasa na mara nyingi shughuli za kilimo wakati mwagine zinachangia kusababisha uharibifu na kusababisha vina vya maziwa kupanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hilo, nitoe rai kwamba pia wananchi waelimishwe ili wale ambao wanalima pembezoni mwa mabonde haya, wawe waangalifu kiasi kwamba tuweze kulinda siyo bonde peke yake, lakini pia hata mtiririko wa maji kuelekea katika Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili nizungumzie kuhusu kuridhia kwa Itifaki hii ya Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Napenda kupongeza kwa hatua hii. Pia natoa rai kwamba naunga mkono moja kwa moja Azimio hili, kwa sababu tumeona kwamba sasa hivi nchi hizi za Afrika Mashariki tuna tatizo la ugaidi. Tumeona mara nyingi kule upande wa Kenya hasa eneo la Garissa na Mombasa mara kwa mara wamekuwa wakishambuliwa na magaidi hasa hawa wanaotokana na wenzetu wale wa kutoka Somalia, Al-Shabaab.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni, mwaka mmoja uliopita, hata katika Mkoa wa Tanga katika maeneo ya Mapango ya Amboni kulipatikana vikundi ambavyo vilikuwa na dalili zote kwamba ni vikundi vya kigaidi na hata hali inayotokea pale katika eneo la Kibiti, Mkuranga ni viashiria ambavyo siyo vizuri sana kwa ustawi wa amani na usalama katika nchi zetu za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme wazi kwamba *protocol* hii itatusaidia ili tuwe na ulinzi wa pamoja kama ambavyo tunafanya na hata juzi hapa, tuliona kule Tanga kulikuwa na zoezi la pamoja kwa nchi za *SADC*. Kwa hiyo, tutafarijika sana kwamba zoezi hili sasa nje ya *SADC* lifanyike pia kwa nchi hizi za Afrika Mashariki hasa kwa kuzingatia kwamba sisi mipaka yetu hii karibu nchi zote tano ukiondoa Sudan Kusini ambayo ni mwanachama mpya, lakini nyininge zote tunapakana nazo kila mahali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hii itasaidia kama hapa ambapo wamezungumza pia kwamba wakati mwiningine kuna minada ya mifugo inafanyika katika hizi nchi, hata mimi katika Jimbo langu la Mlalo pia ni mwathirika wa hii minada. Ni kwamba katika Bonde la Mkomazi ambako kuna wafugaji ambaao wanapatikana katika Wilaya za Same, Lushoto Mkinga na Korogwe, mara nyengi kule hatuna minada katika haya maeneo kwa upande wa Tanzania. Kwa hiyo, hawa wafugaji huwa wanapeleka kuuza mifugo katika upande wa Kenya. Kwa hiyo, kwa kupitia itifaki hii, naamini kwamba suala hili litaimarisha mahusiano haya na tunaweza hata tukawa na masoko mazuri yenye amani na usalama na kusaidia biashara hizi ziweze kufanyika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, nitoe rai kwamba ipo mipaka katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo siyo mipaka rasmi, lakini kwa Serikali hizi kwa kushindwa kuirasimisha, inachochea sasa hata vitendo vya uhalifu kufanyika na biashara za magendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na kwenda kusaini Azimio hili la Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini pia Serikali sasa ione pia chachu na ione pia mwanya wa kwenda kurasimisha ile mipaka, hata isiwe katika ngazi za Kimataifa lakini angalau katika ngazi zile zile za ujirani mwema kwamba tuwe tunaweza kubadilishana mazao ambayo yanapatikana katika nchi hizi tunazopakana. Tofauti na hivyo, bado unabaki mwanya kwa wananchi wa kawaida kuitumia kuvusha kwa njia za magendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitoe rai kwamba tunapokuwa na maazimio mazuri kama haya ni vizuri pia tukayatumia haya haya kuongeza tija nyinezo za kiuzalishaji, isibaki tu kwa ulinzi na usalama, lakini pia za uzalishaji na kuinua uchumi wa wananchi katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono Maazimio yote mawili. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Oran Njeza, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Michael Mmasi.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Nami kwanza niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumwombea mwenzetu uponyaji wa haraka kwa haya yaliyompata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili la leo ni muhimu sana kwa nchi yetu, hata kwa nchi zinazotuzunguka. Labda ningezanzia pale kwenye Azimio, nafikiri kunahitaji masahihisho kidogo ya jina la Wilaya. Kuna Wilaya pale imetajwa, Mbeya Vijijiini. Hatuna Wilaya ya Mbeya Vijijiini, ila tuna Wilaya ya Mbeya. Kwa hiyo, labda kwa ajili ya kumbukumbu sahihi za Bunge, ingebadilishwa na kusahihishwa kuwa Wilaya ya Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, niende zaidi kwenye maoni. Niungane kwanza na maoni ya Kamati, walivyosilitiza kuwa katika mkataba huu labda ndiyo wakati muafaka wa Serikali kuangalia ni namna gani huu mkataba vile vile unaweza kutusaidia katika kutatua tatizo la mgogoro wa mpaka ulioko katika Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hiki kinaweza kuwa ni chanzo kizuri sana na Ziwa Nyasa linatokana na Mto songwe na Mto Songwe kwa kiasi kikubwa unatoka kwetu, kwa hiyo, nafikiri hiyo inaweza kuwa ni chanzo kizuri ni namna gani tukaondoa hili tatizo la mgogoro wa Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili katika maoni ya Kamati, vile vile waligusia elimu kwa wananchi. Nafikiri hili ni jambo muhimu sana kuangalia ni namna gani wananchi wakashirikishwa kikamilifu na kuwapa elimu ya namna ya kuhifadhi haya mabonde yetu na hivi vyanzo vya mito.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia tunapozungumzia bonde la Mto Songwe, kuna Mto Songwe ambao unakwenda Ziwa Nyasa na kwa kweli kilichonifurahisha hapa ni namna gani yatajengwa yale mabwawa matatu na faida za yale mabwawa matatu ambayo yatazalisha umeme takriban *Megawatt* 182.2. Pamoja na hilo, hayo maji yatatumika kwa ajili ya umwagiliaji na vile vile kwa ajili ya matumizi ya majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia yale maeneo ya kwetu hasa katika Wilaya yangu, pamoja na kuwa na mito mingi ambayo ndiyo vyanzo vya mito hii inayokwenda Songwe na ile Songwe inayokwenda Rukwa, vile vile ndiyo chanzo cha Mto Ruaha, lakini yale maji kwa kiasi kukubwa wananchi hawayafaidi. Kwa hiyo, kwa mtazamo huu uliopo kwenye mkataba huu nina imani ya kwamba Serikali itaangalia ni namna gani wananchi nao wafaidike na haya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoliangalia bonde la Mto Songwe ambao unaelekeza maji yake kwenye Ziwa Nyasa, napendekeza kuwa Serikali vile vile iangalie bonde la Rukwa ambalo nalo lina Mto Songwe ambao unaopeleka maji Ziwa Rukwa. Hili ni bonde muhimu sana na kwa kiasi kikubwa Ziwa Rukwa karibu linaanza kupotea kwa ajili ya udongo na mmomonyoko ambao unasongwa na mto Songwe kupelekwa Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika huu mtazamo ambao tunauona hapa leo, nafikiri itakuwa ni jambo jema sana, tuanze sasa hivi kuangalia kuchukua hatua za haraka, ili haya yanayofanyika kwenye Bonde la Mto Songwe unaopeleka maji Ziwa Nyasa, vile vile iende na kwenye Mto Songwe unaopeleka maji Ziwa Rukwa. Tufanye hivyo hivyo,

kwa vyanzo vingine vya mito vilivyoko kwenye milima ya Uporoto na Kitulo amba maji yake ndiyo chanzo cha Mto Kiwira amba unapeleka maji vile vile Ziwa Nyasa na vile vile ndiyo chanzo cha Mto Ruaha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hivi vyanzo vyote ni muhimu sana. Kwa hiyo, elimu itakuwa muhimu sana kwa wananchi, lakini tufanye mikakati ya makusudi, ni namna gani tuwasaidie hawa wananchi ili waone manufaa vile vile, nao wahusike katika kuhifadhi hivi vyanzo vya hii mito.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, atafuatiwa na Mheshimiwa Rehani.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Naibu Spika, nina heshima ya pekee kusimama kwenye Bunge lako Tukufu nami kuweza kuchangia kwa kifupi sana kuhusiana na *documents* hizi tatu ambazo tumeletewa, tuweze kuzipitia kwa minajili ya kuweza kulinda na kuhifadhi maliasili ya Tanzania, kuweza kulinda amani na usalama wa nchi yetu na kuinua uchumi wa Tanzania kupitia mradi wa Hoima - Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza tu kwenye Azimio hili moja la mkataba kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe, kwa sababu kimsingi sikuweza kupitia *documents* zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza kabisa na kurasa ya saba Article No. 7, uundwaji wa hii *Council*, tukisoma pale Section (1) tunasema kwamba *Board Members* watakaoiunda hii *Council*, tume-mention kwamba hatutakuwa na zaidi ya watu sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika watu sita, tuka-mention *relevant Ministries* ambazo tunafikiri zitatengeneza hii *Board Composition* kwenye kusimamia hii *Council*. Pia tuka-

mention Wizara ya Maji, Ardhi, *Energy, Irrigation, Agriculture and Local Government*. Katika hawa watu sita, ukiangalia hizi Wizara hapa, tunapata watu watano, lakini hii nafasi moja tumeacha kwenye *discretion power* ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri pengine ni vizuri Wizara ikajaribu kuangalia au ku-*consider technical personell ambaye ana specified background ya finance au accounting management*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu ukiangalia kwenye majukumu haya ya hii Bodii, utaona pale kwenye *page eight Section (c)*, tunasema kwamba pamoja na majukumu mengine hii *Council* itakuwa na majukumu ya: "*to establish guidelines for financial and technical assistance and development of projects and programs.*" Pia ukienda (d) tunasema kwamba, pamoja na majukumu mengine, hii *Council* itakuwa na majukumu ya ku-*approve the budget of the Commission by the joint Steering Committee and such blah blah blahs.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *concern* yangu, nafikiri ni vyema kwa kuwa tume- *consider Deputy Ministers* ndio ambao watatengeneza hii *Council*, kwenye nafasi za watu sita tume *consider Deputy Minister's* watano. Ni *concern* yangu kwamba pengine *either* *consider* *Deputy Minister from the Ministry of Finance* ama tuwe *specified* *tuseme kabisa* tutahitaji kuwa na *technical personnel* mwenye *specified background in financing or accounting. (Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo, nikija *page nine*, kwenye *the Committee*; uundwaji wa hiyo *committee*, ukisoma pale *Section One* inasema kwamba hiyo *Committee* itaundwa na Wajumbe watano, lakini hatujaona *background of the relevant Ministries* ambao wataunda hii *Committee* kama ambavyo ilikuwa kwenye *Council*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni ushauri wangu pia tuseme hawa *members* wana *background* gani; au

watatoka kwenye Bodi gani; au ni *Ministries* gani? Tusiache tu hivyo ina-*hang*. Kismsingi naona kama vile tunahitaji kuongeza kitu hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukija pale *the Chairmanship of the Committee*, tumesema kwamba huyu *Chairman* atakuwa anaishi kwenye nafasi yake kwa muda wa mwaka mmoja na itakuwa ina-*rotate*, lakini pia nikawa nahoji ni vyema basi tungeona *the life span* au *project duration* kwa maana kwamba mimi ningeweza kusema mbona *one year* haitoshi? Sasa napata shida kwa sababu hata sijui *life span* ya hii *project*, yaani *the Shared Watercourse Projects*. Kwa hiyo, ni vyema basi tukaona kabisa hii *project* ni ya muda gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kismsingi naona hivyo, kwa sababu naweza nikasema kwamba mwaka mmoja hautoshi au nikashindwa kupata *relevance* ya mwaka mmoja kwa sababu kismsingi sijui hata *life span* ya hii *project*. Kwa hiyo, *concernyangu* kwenye *section* hiyo ilikuwa ni hiyo niliyoi-mention.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikienda *section 12* kwenye Sekretariet, tunasema pamoja na Bodi itakayoteuliwa; *appointing authority of course* imekuwa *mentioned*, lakini pia tukasema itakuwa *headed* na *Executive Secretary* pia itakuwa *assisted* na *Deputy Executive Secretary* lakini *who are the body?* Hatujaona bado hii bodi ni akina nani? Wako wangapi? Wanatoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukiangalia *functions*, it means zinatakiwa ziwe *performed* na a certain number of people, lakini siyo tu *Executive Secretary* au *Deputy Secretary*. Kwa hiyo, kismsingi naona tuna haja kabisa ya kusema idadi ya *Board Members*, ikibidi pia na *background* zao, lakini siyo tu kusema kwamba itakuwa *headed* na nani kwa sababu tayari tuna *duties and responsibilities* to be performed by a certain number of people.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kwenda kwa haraka haraka *page number* 15, kuhusu *dispute resolution*. Ukiangalia kwenye hii *dispute resolution, the way imekuwa drawn, hutaona who is the specified body to deal with the disputes or misunderstandings*. Nadhani ingekuwa ni muhimu kabisa na itakuwa na tija kama tutaweka *the governing board ya ku-overseas disputes au misunderstandings*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka mpaka Ziwa Malawi, ile *misunderstanding* ambayo tuliyokuwa nayo, nafikiri ni fundisho tosha. Kwa hiyo, Kimsingi napenda kabla ya ku-*question* kwa nini *SADC Tribunal* iwe ndiyo *Appellate Board* lakini pia ni muhimu tukaona kwamba kunakuwa na *governing board ya ku-overseas any dispute that may arise during the execution of this project*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukisoma hii *document* inakwambia *host country* ni Tanzania na Makao Makuu yatakuwa Mbeya kule Songwe. Sasa kama *host country* ni Tanzania, kwa nini *Appellate Board* inabaki kuwa *SADC Tribunal?* Kimsingi niki-refer hata kuna Mjumbe mmoja ameongea humu ndani, lakini siangalii kwake, naangalia kama nilivyoelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipitisha hapa juzi Miswada ya kuweza ku-*govern our natural resources*, ile *Permanent Sovereignty Act* ambayo tulijikita na tukasema kabisa kwamba *any dispute or misunderstandings* zitakuwa *dealt within the country*. Kimsingi ukiangalia hii *document* na ukiangalia vitu ambavyo tumepitisha Miswada na Sheria ambazo tumepitisha nadhani hapa kunaleta ukakasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba naunga mkono hoja asilimia mia, mawasilisho yaliyoletwa na Wizara husika katika muktadha mzima wa kujengwa Tanzania yenye uchumi wa katika, lakini pia ni *subject to minor corrections where necessary*. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Rehani atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa upande wa

Wabunge, utafuata upande wa Serikali. Mheshimiwa Rehani atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Olensha halafu atafuatia Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi kupata fursa hii adhimu. Kwanza niunge mkono hoja hii ya kuanzisha *Commission* hii ya Bonde la Mto Songwe ambayo kimsingi, *the highly potential area* kwa nchi yetu, kwa uchumi wa nchi hii, lakini vilevile kwa mustakabali wa wananchi wale wa Wilaya zile tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba mimi kwa bahati nzuri nimeusoma huu mkataba vizuri na nimeuelewa madhumuni yake. Ikiwa dhumuni kubwa ni kuhifadhi, kuendeleza na kuondoa athari za maji ambayo yanasababisha mto ule uweze kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyngine na tishio la athari ya wananchi amba wanakaa pembezoni mwa mto ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, fursa hasa za kuangalia kitu gani ambacho kitaweza kutusaidia kama nchi, eneo lile la Mto Songwe kwa Tanzania ni *belt* ya uzalishaji wa mazao mbalimbali. Kinachotakiwa baada ya kuridhiwa Kamisheni hii; Kamisheni itengeneze mpango mkakati ambao utaweza kuridhiwa na pande zote mbili kwa sababu yale yote yaliyoainishwa katika Kamisheni hii, kila mmoja yanamgusa hasa kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango mkubwa pale wa kuanzisha mabwawa matatu yale ya Songwe Juu, Songwe Kati na Songwe Chini, kwa kweli kwa Tanzania ni fursa kubwa kwanza kwa upatikanaji wa maji hasa ya mvua. Ile dhana ya *rainfall harvesting* pale ndipo itakapotimia. Tutakapoweza kuyavuna yale maji, tutaweza kuu-*shape* ule mto uweze kwenda kwa mujibu wa mwelekeo tunaoutaka sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mto ule unafungua uwanja mpana wa kuanzisha maeneo ya umwagilaji maji kwa eneo lile la Kyela. Tutaweza kuzalisha mpunga kwa kutumia yale mabwawa kama wanavyozalisha Moshi Chini

na Moshi Juu. Tufanye uwekezaji wa maana ili nchi ione kane kwamba kuanzisha ile Kamisheni imeleta manufaa na isiwe Kamisheni tu kama nyingine ambazo baada ya miaka mitano, kumi tukija kutathmini, hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Mawaziri watakoasimamia, pawe na uwekezaji ambao utaleta fursa kwa kila sekta. Tukizungumza Sekta ya Kilimo, zaidi ya hekta 15,000 pale tunaweza kuzifanya zote kuwa za umwagiliaji maji na zikaweza kutuzalishia zaidi ya tani laki tatu za mchele. Hilo linawezekana, suala ni kujipanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika eneo lile kuna mazao ya biashara, kuna ndizi ambalo ni zao kubwa katika maeneo yale ya Tukuyu na Kyela. Fursa ya uzalishaji kwa kutumia *irrigation* ipo, kutumia mabwawa yatakayoanzishwa kule. Tuhamasishe wananchi wajipange kwenye uzalishaji wa tija kuliko uzalishaji wa kutegemea mvua ambao hauna uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo yale, bado unaweza kuzalisha mahindi kwa mpango maalum na nchi ikaweza kunufaika na kuondokana na tishio la njaa linalotokana na ukosefu wa maji wa kila siku. Isitoshe, kazi kubwa inayotaka kufanya pale ni kuhifadhi mazingira ya vyanzo vya mto ule toka vinavyotokea huko kwenye zile chemchemi za kutilia maji katika eneo lile, kwa sababu maji katika eneo lile ni mwaka mzima. Hiyo siyo kwamba yanavunwa yale ya mvua, lakini maji yanatoka kwenye chemchemi ambazo ziko katika maeneo mbalimbali na ndiyo maana tunapata fursa na nguvu ya kuanzisha yale mabwawa ya kuzalisha umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale panategemewa kuzalishwa umeme zaidi ya megawati 180, kitu ambacho tunafikiria tu kwamba mgawanyo uwe nusu kwa nusu. Nasema, bwana, kila mwamba ngoma huvutia kwake vilevile. Asilimia kubwa ya ule mto na eneo kubwa ni letu siye, lakini na zile *infrastructure* ambazo zinahitajika kujengwa katika eneo lile ziko kwetu. Nafikiri hao watakaoenda kukaa;

Mawaziri na watu wengine, waangalie uwiano wa kugawana na siyo tu kwa kujenga mahusiano ya kusema kwamba tunaridhiana nusu kwa nusu, hapo tupaangalie kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nitachangia katika hii Kamisheni ni uanzishwaji wa viwanda. Tuhamasishe maeneo yale ambayo yanazalisha kokoa katika maeneo mbalimbali ya Kyela, basi kuwepo na kiwanda ambacho kitaweza kuzalisha *Chocolate* na vitu vingine kuanzishia wananchi wetu ajira na fursa nyingine mbalimbali za kiuchumi zitakazokuwepo kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo vilevile inafungua corridorile kuweza kuwa na mpango wa kujengwa reli kutoka huko Mchuchuma mpaka Lindi lakini ikaunganisha mpaka kwenye reli ya *TAZARA*. Itazidi kufungua fursa kubwa za kiuchumi na kulifanya eneo lile kuwa moja katika eneo, wanaita *economic zone*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili kwa nchi yetu limekuwa likitumika isivyo na faida; yaani likitumika kikawaida. Hii sauti ya kuanzisha Kamisheni ilianza miaka mingi, lakini tushukuru Mungu sasa hivi Serikali imefika mahali pa uamuzi wa kuianzisha na kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wataalam mbalimbali wa Wizara zote zinazohusika na Kamisheni hii kukaa na kuanzisha miradi ambayo itaweza kuwasaidia wananchi kushiriki nao hasa kwenye uhifadhi wa mazingira ya eneo lile, kwa sababu kila eneo mto unapopita mazingira yanakuwa ni mazuri, lakini kutokana na kazi na shughuli za kibinadamu, mazingira yale yanaharibiwa kwa njia moja au nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wangu niombe hasa Wizara ya Kilimo kuititia mifugo, eneo hili lilindwe na lisiiingizwe mifugo. Tutalimaliza! Tutauua ule mto na matokeo yake maji yale yatashindwa kutiririka kama yanavyotiririka hivi sasa. Haya ni mambo ya msingi. Tunaweza kuanzisha mambo

mazuri, lakini kuna lingine tukalisahau ambalo linaathiri mazingira ya pale. Kwa hiyo, nawaomba sana wahusika wa Mikoa, Wilaya na maeneo mengine kuweza kuepuka uingizwaji wa ngombe wengi katika maeneo yale pale ambayo yanatumika kwa kilimo sasa hivi kikubwa. Kule Zanzibar wanasema mchele wote unaletwa kutoka Mbeya ndio wenye soko kubwa. Kwa hiyo, nawaomba wazalishaji na viongozi walioko katika maeneo yale tuweze kutilia mkazo sana uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nimeliona kwamba ni fursa kubwa, zile meli za bandari za Itui, Itumbi na sehemu nyingine, pale sitawenza kufanya kazi vizuri zaidi, kwa sababu ufungukaji wa ile Kamisheni itaaniszha fursa kubwa ya wafanyabiashara, lakini na wenzetu wa Malawi watapata fursa kubwa ya kuleta mizigo yao katika maeneo yale na hasa kwa kutumia ile meli mpya iliyoundwa hivi sasa iliyokuwa inaanza kazi kuwa na manufaa zaidi kuliko vile ambavyo tulivyokuwa tumetegemea. (*Makofii*)

*(Hapa kengele illilia kashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rehani, kengele ya pili hiyo.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa William Tate Olenasha, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, halafu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ajiandae.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nami kupata fursa ya kuchangia mjadala unaoendelea. Napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole sana kwa Mheshimiwa Tundu Lissu kwa yaliyompata na kuungana nao vilevile kumwomba Mwenyezi Mungu amjalie apate afya njema na arudi katika shughuli zake za kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita katika hoja moja iliyotolewa kuhusiana na Azimio la Kuridhia Mkataba Kuanza Kamisheni ya Pamoja Bonde la Mto Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili ni muhimu sana kwa nchi yetu na katika hali ya kawaida, limechelewa sana. Kumekuwepo na majadiliano ya kuanzisha Kamisheni ya kusimamia bonde hili kati ya Tanzania na Malawi tokea mwaka 1976. Kwa kweli imechelewa sana kwa sababu rasilimali ambayo inatumika na nchi zaidi ya moja katika hali ya kawaida ingetakiwa iwe na utaratibu wa pamoja wa kusimamia; na katika hali ya kimazingira ambayo bonde lile lipo kwa sasa, kwa kweli Kamisheni hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ilitolewa kwamba kifungu cha *convention* hii inayozungumzia kuhusu usuluhishi wa migogoro inapingana na sheria ambayo tulipitisha ya *Natural Wealth and Resource Permanent Sovereignty Act* ya 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Tundu Lissu alitoa hoja kwamba kwa sababu itifaki ambayo tunaizungumzia inaanzisha utaratibu ambao kama kutakuwa na mgogoro kati ya Malawi na Tanzania kuhusu usimamizi wa Bonge la Mto Songwe, basi itapelekwa kwenye *Tribunal* la SADC. Yeye aliona inaingiliana na inavunja sheria ambayo tumepitisha hivi karibuni ya kusimamia rasilimali zetu, sheria ambayo nimeitaja ya *Natural Wealth and Resource Permanent Sovereignty Act of 2017*, hasa katika Kifungu cha 11(1) mpaka (3).

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba hii au sheria hizi ni tofauti. Wakati Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Usimamizi wa Bonde la Mto Songwe inashughulika na uhusiano wa nchi na nchi, yaani katika maana ya *bilateral agreement*, sheria yetu ile ambayo nimeitaja ya *Permanent Sovereignty*, yenye we inahusika na uhusiano wa nchi yetu na wawekezaji au makampuni ambayo yanawekeza katika rasilimali zilizoko katika nchi yetu.

Kwa hiyo, katika hali ya kawaida ni mikataba tofauti; mwagine ni mkataba wa Kimataifa ambao unaongoza ushirikiano kati ya nchi mbili lakini nyingine ni sheria ya ndani inayohusiana tu na mikataba ya kutumia rasilimali zilizopo ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, ni vitu tofauti na wala hakuna hatari yoyote katika sisi kuridhia itifaki hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ni lazima tufahamu kwamba katika hali ya kawaida kama rasilimali ambayo inalindwa na sheria inatumika na zaidi ya nchi moja, haiwezekani sheria ya nchi moja ikawa ndiyo inayotawala rasilimali ile. Kwa hiyo, kwa sababu rasilimali ya Bonde la Mto Songwe ni *shared resource*, ni rasilimali ya nchi zaidi ya moja, katika hali ya kawaida ni lazima isimamiwe kwa pamoja na kwa sheria ambayo ni ya pamoja. Itifaki hiyo ambayo ndiyo tunasema sasa tunataka ianze kufanya kazi, imetengenezwa kwa utaratibu wa itifaki za Jumuiya ya Kusini mwa Afrika *SADC* ambayo sisi ni wanachama na Malawi vilevile ni mwanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa pamoja tulishakubali huko nyuma tulipojiunga kwamba masuala yote ambayo yanahusiana na maji au rasilimali ambazo zinamilikiwa kwa pamoja, kama kuna migogoro, migogoro ile itaamuliwa kwa kutumia *Tribunal* au Mahakama ya *SADC*. Kwa hiyo, niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba hakuna sheria yoyote iliyovunjwa, tuko sahihi kabisa. Sisi tukiridhia Azimio hili wala hatutakuwa tumevunja sheria yetu ambayo sisi wenyele tumeipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile hoja ile iliekea kutaka kujenga hoja kwamba sisi hatuheshimu sheria za Kimataifa tunapotunga sheria kama ile ya kwetu *The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty Act, 2017*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunaheshimu sheria za Kimataifa na ndiyo maana hata leo hii tupo hapa tunazungumzia kuhusu *Bilateral Convention*, ni sheria ambayo kwa mwonekano wake, kwa hali yake ya kawaida ni Sheria

ya Kimataifa, bado tunaendelea kuheshimu, lakini kuheshimu kule haitunyimi sisi kuendelea kulinda rasilimali zetu ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu wa kusuluuhisha migogoro ambapo tunafikiri italinda zaidi rasilimali zetu, itatupa nafasi kubwa zaidi ya kuweza kusimamia rasilimali zetu bila kuingiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, napenda kuunga mkono hoja ya Azimio lililopo mbele yetu. Nashukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, atafuatiwa na Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Samahani, kumbe nilishamtaja. Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa nami nichangie kwa kifupi tu kuhusu moja ya mazimio yaliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mshituko mkubwa nilioupata kwa taarifa uliyotupa hapa kuhusu Mbunge mwenzetu, naungana nawe kabisa kumwombea mwenzetu apate ahueni haraka na vilevile namwomba Mwenyezi Mungu atupe ustahimilivu mkubwa katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalazimika kusimama kama nilivyosema, kuchangia kuhusu Azimio la Kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Tanzania na Malawi. Kuanzishwa kwa Kamisheni hii ambako kuna miradi chini yake kadhaa ya maendeleo kwa wananchi, ni sawa kabisa na kutumia jiwe moja na kuua ndege watatu kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa Azimio hili litawanufaisha watu zaidi ya laki tatu; ni idadi kubwa sana hii ambayo iko katika hilo bonde hasa kupitia miradi yao hiyo ya umwagilajji, miradi hiyo ya maji safi na vilevile miradi ya umeme, kama ambavyo wenzangu wameeleza nisingependa kurudia.

Pili, tutakuwa tumetatua tatizo sugu la muda mrefu la Mto Songwe kupindapinda kubadilisha njia yake kila wakati na kusababisha watu waliokuwa Tanzania kuwa wa Malawi mara nyingine na Wamalawi kuwa Watanzania. *TRA* najua watashangilia sana kusikia hili, maana wanaowadai kodi, mara nyingine wanashindwa kwenda kuwadai maana tayari wako Malawi kutokana na maamuzi ya huo mto.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingine wengine hapa tunategemea kura kwa Watanzania wetu. Kuna kipindi nimewahi kukuta ngome yangu kubwa yote imehamia Malawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya ndiyo mambo ambayo watu wote kwa kweli katika Bonde hili watashangilia sana kwamba Azimio hili linaenda kutatua tatizo lillolikuwa sugu kati ya Tanzania na Malawi kuhusu mpaka huo ambapo tuliwahi kufikia hata mahali hata eti kufikiria kujenga nguzo katikati ya huo mto. Kutokana na haya mabwawa matatu, hakutakuwa na mafuriko ya kutushangaza tena eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Azimio hili linatupa fursa maalum, fursa muhimu ya maelewano zaidi kati ya Tanzania na Malawi. Sasa hivi tumeanza ushirikiano, nami nina uhakika huu utakuwa ndiyo msingi wa maelewano zaidi na zaidi kati ya nchi zetu hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie tu kitu kimoja kwamba nilikuwa namwangalia rafiki yangu ananiangalia hapa, kwamba mimi eneo langu pale Kyela halijawahi kuhamia Malawi. Sasa tusije tukaanza kueleweka vibaya

hana, halijawahi. Muda wote mimi niko mbali kidogo na huo mto, lakini naongelea tu kwa meneo yote ambayo yanahusika Wilaya ya Kyela.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa Azimio hili, kwa uamuzi huu kupitia Wizara yetu ya Maji na Umwagiliaji, kwa sababu watafaidika sana katika mradi huu; ni pamoja na Wilaya yangu, Jimbo langu la Uchaguzi la Kyela, hasa Kata zetu za Ngana, Katumbasongwe, Ikimba, Njisi, Ikolo, Ngonga, Bujonde, wote hapa katikati tutafaidika sana na Azimio hili tunalolipitisha leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisipoteze muda wako mwingi, naomba tu kusema, naunga mkono Azimio hili. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana *Engineerlsack Kamwelwe*, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer Lwenge*, Waziri wa Maji. Mheshimiwa Dkt. Susan Kolimba ajiandae.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuungana na wenzangu kwa masikitiko makubwa sana kwa tukio ambalo limetokea mchana wa leo. Mimi nakaa *Area 'D'*, nimesikia bunduki, lakini baadaye nakuja kupata taarifa kwamba ni Mbunge mwenzangu ambaye amejeruhiwa. Kwa kweli inasikitisha sana, kwa siku ya leo inaleta uwoga kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa shukrani kwa Kamati ya Bunge ambayo inashughulikia miundombini ya maji kwa michango yao mizuri ambayo wametushauri kuanzia tulipoanzia michango hii kwenye Kamati. Pia nashukuru sana Maoni ya Kambi ya Upinzani ambao wameunga mkono moja kwa moja kwenye jambo hili. Nashukuru kusema kwamba kwenye masuala kama haya, kwa sababu tunajenga nchi kwa pamoja, sisi wote ni Watanzania, kwa hiyo, inabidi tuungane tuache suala la tofauti za itikadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyoongea, tayari tuna *Interim Secretariat* na imeshafanya kazi kubwa sana. Hii *Interim Secretariat* Ofisi yake iko Kyela, nami nimeshatembelea pale. Ndani ya Watumishi; tuna Watumishi wa kutoka Malawi na Watumishi wa kutoka upande wa Tanzania. Makubaliano yaliyopo ni kwamba hata tutakapokuwa tumekamilisha hii Kamisheni, ikisharidhiwa ni kwamba Ofisi zitakuwa Kyela.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tangu Sekretarieti ilipoanza, Serikali ya Malawi na Serikali ya Tanzania wanachangia hela kuendesha ile Sekretarieti ya mpito; na imefanya kazi kubwa sana. Imeshakamilisha *feasibility study*, imeshakamilisha *detailed design* na imefanya semina mbalimbali na mikutano mbalimbali na Wafadhili na kutangaza kuhusu huu Mradi wa Bonde la Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari kuna *indication* kubwa kwamba Wafadhili wanasubiri tupitishe hili ili sasa mazungumzo ya mwisho yaweze kufanyika, tufanikiwe kutekeleza ule mradi. Kwa hiyo, suala kama hili Waheshimiwa Wabunge kwa kuliunga mkono, sisi kwa kweli kama Watanzania na kama Wabunge na Wizara ya Maji tunafarijika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia juzi kulikuwa na Mkutano wa *SADC*, nami Mheshimiwa Waziri alinituma niende kule. Katika miradi miwili ambayo imepita; imepitishwa na *SADC*, ni pamoja na huu Mradi wa Songwe. Umepitishwa kwa sababu una *components* tatu ndani yake kama alivyokuwa amezungumza Mheshimiwa Mwakyembe. Tutazalisha umeme pale, tutatengeneza skimu za umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna hekta za mwanzo 6,200; na kati ya hekta hizo, hekta 3,150 ziko upande wa Tanzania na hekta 3,050 ziko upande wa Malawi. Kwa hiyo, wananchi wa maeneo ya Tanzania na huku watafaidika na umeme na bado watafaidika na kilimo cha umwagiliaji, kilimo chenye uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia maji yatachakatwa majisafi na salama. Kwa hiyo, sehemu ya maji yatakwenda upande wa Tanzania na sehemu ya maji watatumia watu wa Malawi. Kwa hiyo, sioni katika mpangilio kama huo ambaao tuna-share umeme, tuna-share huduma ya maji safi na salama na tuna-share kilimo cha umwagiliaji, jamanii undugu utazidi hapo. Unatarajia kuwe na ugomvi kweli hapo? Hata matatizo mengine yaliyopo kwenye lile Ziwa Nyasa, tuna imani kabisa kwamba utatuзи wake sasa utakuwa rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge katika michango yao wamezungumzia suala la ushirikishaji wa jamii. Tangu mwanzo hii *Interim Secretariat* ilivyoanza, imeshirikisha wananchi kutoka ngazi za Vitongoji, imekuja kwenye Vijiji, mpaka Kata, mpaka Wilaya. Wameshirikishwa na *minutes* zipo na taarifa hizi tumezitoa kwenye Kamati. Kwa hiyo, kila mwananchi yuko *aware* na suala hili na wanalisubiri kwa hamu kabisa kwamba Kamisheni hii ipitishwe na Bunge letu ili ianze kufanya kazi, wao wanasubiri kupata maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, hebu tujaribu kuiangalia mipaka kwa wale ambaao wanaishi kwenye mipaka. Kama maendeleo yakiwa upande mmoja kwingine kukawa hakuna maendeleo, maisha yanakuwaje katika hilo eneo? Kwa maana ya hii Kamisheni kwamba maendeleo yatakayopatikana yatakuwa *shared* upande wa Tanzania na upande wa Malawi. Kwa hiyo, tutazidi kuimarisha undugu wetu na ushirikiano utakuwa mkubwa. Migogoro mingine midogo midogo wakati mwngine unaitatua *automatically* kwa kuweka huo ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tunawashukuru sana na tunawaomba kwa kuititia kwenye michango ambayo wengi mlipata nafasi ya kuchangia, wengi mnaridhia na hili. Kwa hiyo, mwisho kabisa tunawaomba mridhie ili hatua nyingine ziweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, namalizia kwa kushukuru tena, ahsanteni sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa *Engineer Lwenge*.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami nitoe masikitiko yangu kwa Mbunge mwenzetu kushambuliwa na majambazi. Kwa kweli, tunampa pole sana na tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu aweze kumsaidia apone haraka aje afanye kazi zake za Kibunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla wenu kwa namna mlivyochangia, hakuna hata mmoja aliyepinga kwamba tusiianzishe hii Kamisheni ya kuendeleza Bonde la Mto Songwe. Nashukuru kwa sababu siyo kawaida, mara nyingi kuna wengine wanapinga tu hata mazuri, lakini kwa leo angalau kwa namna moja au nyingine wote wameunga mkono kwamba hii Kamisheni ni muhimu ianzishwe kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu walioko kwenye Wilaya tano. Katika Wilaya hizi tano vijiji 48 vitanufaika na miradi hii ambayo imeibuliwa kwa manufaa ya nchi zote mbili upande wa Tanzania na upande wa Malawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza kwa maoni ambayo yametolewa na Kamati ya Bunge, yote haya katika mkataba huu ambao tumesaini kati ya Malawi na Tanzania, vifungu hivi vyote viko *very flexible* kwamba hakuna kifungu ambacho hakina namna ya kurekebisha. Madaraka yote ya kurekebisha vifungu hivi tumeipa lile Baraza la Mawaziri. Baraza la Mawaziri la pande zote mbili watakuwa na uwezo wa kuongeza jambo lolote jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba mambo mengi mazuri haya ambayo mmeyaleta Waheshimiwa Wabunge, tutaangalia namna ya kuyapeleka katika kuboresha mkataba wetu ili uweze kuleta manufaa zaidi ili tuweze kuendeleza bonde hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa sababu hawa wananchi wa vijiji 48 ambao ni zaidi ya 315,000, kwanza

watapata umeme wa uhakika. Kwa awamu ya kwanza ambayo tunajenga Bwawa la Songwe Chini ambalo litawenza kutoa megawati 180 Tanzania tutaanza na mgawo wa Megawati 90 ambazo tutaziingiza kwenye gridi ya Taifa. Kwa sababu azma yetu ni kupeleka umeme vijiji kwa sehemu kubwa, hivi vijiji 48 nina hakika kwa mpango huu watapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hizi hekta 6,000 za kilimo cha umwagiliaji. Wakati madhara ya mto huu ulivyo kuwa unafurika mara kwa mara, hata hiki kilimo cha umwagiliaji kilikuwa kinakuwa tatizo kwa sababu mashamba ya wananchi maeneo ya Kyela na lleje, yalikuwa yanajaa maji kiasi ambacho iliathiri sana kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yale. Tukija kuboresha sasa tukajengea miundombinu ambayo imeboreshwa, nina hakika sasa kutakuwa na kilimo endelevu na tunainua uchumi kwa ajili ya wananchi wanaoishi maeneo haya. Kwa hiyo, ni kama wengine walivyosema, kwamba mkataba huu umechelewa, ungekuja mapema zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tujue kabisa kwamba tumeanza kuzungumza uanzishwaji wa kitu cha namna hii toka mwaka 1976, lakini tumekuwa tunapanda ngazi kidogo kidogo. Tulipofika mwaka 2001 ndiyo tukaanzisha ile Kamisheni ya Mpito au *Interim Secretariat* ambayo nayo imefanya kazi kubwa ikiwa ni pamoja na kujenga hii Ofisi ya Makao Makuu hapo Kyela. Kwa hiyo, ofisi tayari ipo imeshajengwa; na tutaanzia pale katika kusimamia sasa miradi hii iliyoibuliwa itakayoleta manufaa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lissu alikuwa na mashaka, alifikiri kwamba katika kusaini mkataba huu alienda Lwenge peke yake. Naomba nimtoe wasiwasi kwamba hakwenda Mheshimiwa Lwenge peke yake, ilikwenda kama Serikali ikiwa na wataalam wote waliobobea katika sheria, akiwepo Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, masuala ya sheria yote yamezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Olenasha amefafanua vizuri namna ya kutekeleza miradi inayokuwa inashirikisha zaidi ya nchi moja, lakini katika kutatua migogoro, hili suala la kwenda kwenye *SADC* au *UN*, hiki ni kitu cha mwisho kabisa. Tumeweka hatua ya kwanza na kwa maelewano tuliyokuanayo katika miaka yote hii hatufiki huko, kwa sababu kazi tunayoifanya ni ya manufaa kwa nchi zote mbili. Ndiyo maana nasema kwamba sasa tunaimarisha uhusiano wetu kwa nguvu zaidi kwa *ku-develop* miradi inayotunufaisha Malawi na Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata hili suala la mgogoro wa mpaka au mgogoro wa Ziwa Nyasa nina hakika tumeanza vizuri kwa sababu hiki kitakuwa ni kichocheo kimojawapo ambacho kimetuunganisha zaidi Malawi na Tanzania katika kufikia muafaka wa jambo hili ambalo linazungumzwa la matumizi au rasilimali za Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wetu una namna ya kutoka kama nchi moja ikionekana inakiuka makubaliano, tumesema kwenye Kifungu cha 18 kwamba nchi moja inaweza ikavunja mkataba inapoona mwenzie hatekelezi yale tuliyokubaliana kwa kutoa *notice* ya miezi sita kwa maandishi, kwa hiyo, kuna namna ya kutoka, lakini sitaki tukifike huko kwa sababu hatuvezi kutoka na kwa sababu pia, hii miradi ambayo imeibuliwa ya kujenga umeme na miradi mingine, tayari wafadhili wameshaonesha nia, kama nilivyowasilisha pale mwanzo. Wameshaonesha nia ya kutusaidia ili tuweze kuendeleza Bonde hili la Mto Songwe kwa manufaa ya nchi hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba maoni yote ambayo Waheshimiwa Wabunge mmetoa, tutaendelea kuyaboresha. Kwenye *Council*, katika zile Wizara sita, kuna Wizara ya Fedha pia ipo. Kuna mmoja alikuwa nataka kuhakikishiwa kama kuna wataalam wa fedha watakuwepo. Wizara ya Fedha ni mojawapo katika Wizara ambazo zinaingia kwenye *Council*, kuna Wizara ya Ardhi, Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Ushirikiano wa Kimataifa, Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali na Wizara ya maji. Ila kwenye

Mkataba wetu tumeweuka nafasi ya ku-*opt advisor* yeoyote au Wizara yoyote ambayo tunafikiri kwa muda ule tunapokuwa tunajadili tunaweza tukamwingiza kwenye *Council* ili kusudi aweze kusaidia, kutegemea ni jambo gani tunalolishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mkataba uko vizuri, uko *flexible*. Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge kwa namna mlivyochangia, niwashukuru tena kwa maana kwamba sasa tunakwenda kuanzisha hii Kamisheni ambayo itatusaidia kwa maendeleo ya wananchi wetu wa pande zote mbili. Pia, tutaondoa huu wasiwasni wa wananchi wetu ambapo mto kila mara ukifurika walikuwa mara wanakuwa Malawi, mara wanakuwa Tanzania; ili kusudi waweeze kufanya maendeleo endelevu, sasa watakuwa na uhakika wako Tanzania na wameshaendelezwa, wameshapata mahitaji mengi ya kuwainua kiuchumi. Kwa hiyo, nina imani kabisa baada ya utekelezaji wa mradi huu, tutakuwa na jambo la kujivunia kwa kuendeleza rasilimali za maji za Bonde la Mto Songwe kwa faida ya nchi zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, nirudie tena kukushukuru wewe kwa namna ulivyoendesha mjadala huu. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa pande zote mbili kwa namna walivyochangia; na nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wengine ambao pia wameweza kuchangia na kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja ili Kamisheni hii sasa iweze kuanzishwa, ya Ushirikiano Kati ya Malawi na Tanzania kwa ajili ya Kuendeleza Bonde la Mto Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makof)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Malawi liliridhiwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono na kwa hiyo, Bunge limeridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mta Songwe kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Malawi.

Sasa namwita Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Susan Kolimba. Tutamalizia na Mheshimiwa Mwigulu Mcembba.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa ruhusa yako na kwa heshima kubwa niweze kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu, hoja ya kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kuchangia hoja hii, nitachangia hoja ambazo zimetolewa na baadhi ya Wabunge kuhusu hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza ilitolewa na Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud Ally Khamis ambaye alikuwa anaitaka Serikali iweke mkazo katika kusimamia alama za mipaka kwani tayari kumekuwa na tuhuma za kuondoa alama hizo katika mipaka ya Sirari na maeneo mengineyo. Naomba nitoe maelezo juu ya utekelezaji wa Serikali juu ya hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la urekebishwaji wa mipaka ya nchi linafanyika kuitia mazungumzo baina ya nchi na nchi. Tayari Serikali imekwishaanza majadiliano na nchi ambazo zinapakana nazo na hivi karibuni nafikiri mmesikia, Tanzania ilifanya majadiliano na Serikali ya Uganda kuhusu mpaka katika Mkoa wa Kagera ambayo

yameshakamilika na hatua inayofuata sasa ni kujenga na kuimarisha alama za mpaka ule. Aidha, Serikali inajiaanda kupitia upya mpaka wa nchi hizi mbili hasa kwenye upande ule wa ziwani kati ya Tanzania na Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa upande wa mpaka wetu wa nchi ya kwetu pamoja na Kenya, mazungumzo yalishakamilika na tayari Serikali imeshatoa mchango wake katika kugharamia, kujenga na kuziimarisha alama za mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kwa upande wa nchi za Malawi, majadiliano bado yanaendelea. Kama mlivyosikia mara ya mwisho, Tanzania pamoja na Malawi waliiwtwa na lile jopo la Marais Wastaafu kule Kusini ili kujadili suala la mpaka wa Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa tofauti zozote zinazojitokeza kati ya nchi na nchi na hasa zinazohusu masuala ya mipaka, zitakuwa zinaendelea kusuluuhishwa kwa njia ya mazungumzo na kwa amani kwa faida ya pande zote mbili kwa sababu hawa ni majirani zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya pili ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud Ally Khamis. Hoja hii ilikuwa inahusu Ibara ile ya 12 (e) ya Itifaki inayozitaka nchi wanachama kushirikiana katika kukabiliana na wahamiaji haramu. Niseme tu kwamba nchi yetu imekuwa ikipokea wahamiaji haramu kutoka nchi za Eritrea na Ethiopia wanaokwenda Afrika Kusini, ambapo tatizo ambalo kwa Tanzania tumeshaliskia mara nyingi na limekuwa ni changamoto; Serikali ihakikishe kuwa nchi ya Kenya haiwaruhusu watu hao kupitia kuja kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kwa kusaini Itifaki hii, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki watatumia mikakati ambayo iko ndani ya Itifaki na kuhakikisha kwamba hivi vyanzo na njia kuu na Vituo vya

Wahamiaji haramu ambavyo viro kwa sasa hivi, vitaondolewa kwa kuitia Itifaki hii ambayo sasa hivi tunairidhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nawaomba sana tuweze kuiunga mkono Itifaki hii ipite ili mikakati iliyowekwa na Serikali na kwa kuitia Itifaki hii, changamoto hii ambayo inapatikana kwenye nchi yetu na nchi za jirani itakuwa imekwisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwigulu Nchomba, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuhitimisha hoja, lakini kwa ruhusa yako, kabla sijahitimisha hoja, naomba niseme mambo mawili. La kwanza, kama ambavyo mmesikia Mbunge mwenzetu ameshambuliwa kwa shambulio baya na watu wasiojulikana, lakini taarifa rasmi mtapewa. Tutatoa kwa utaratibu kadiri tutakavyoongozwa na Bunge hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa tu za awali ni kwamba Madaktari wamejithidi kwa kiwango cha hali ya juu kuweza kutoa huduma ya kwanza. Nimechelewa kuja hapa, nilikuwa pale na Mheshimiwa Spika, *briefing* ya mwisho tuliyopewa ni kwamba wamefanya vizuri wameweza kudhibiti damu zilizokuwa zinatoka. Kwa hiyo, wamesema hatua ya awali ya huduma ya kwanza walijotoa imeenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la awali tu kwa upande wa Wizara ya Mambo ya Ndani, japo tutatoa tamko rasmi, lakini tunasema jambo hili lilitokea ni jambo ambalo halikubaliki; nasi kama Wizara ya Mambo ya Ndani na kama Serikali, hatutaruhusu na hatutaacha jambo hili lipite hivi hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeelekeza Polisi Mkoa wa Dodoma waweke vizuizi njia zote zinazotoka Dodoma na zinazoingia Dodoma na wasambae kuweza kuwasaka hao wote ambao wamehusika na tukio hili, tukio ambalo linapaka matope sura na heshima ya nchi yetu na tukio ambalo linapaka matope Serikali yetu ambayo inashughulikia masuala ya usalama wa raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, iwe kwa sababu za kisiasa, iwe kwa sababu ya hujuma, iwe kwa sababu za ugomvi na iwe kwa sababu za za kijambazi, yote hayo tutasaka kuhakikisha kwamba wale wote ambao wamehusika na jambo hilo wanafikishwa katika mkono wa sheria ili kuweza kukomesha vitendo hivyo viovu ambavyo havijazoleka katika nchi yetu. Watanzania wote tumwombee mwenzetu ili Mungu ampe afya njema na afya yake iimarike aweze kuendelea na kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, taarifa rasmi itatolewa kwa utaratibu ambao Kiti chenyewe kitatoa kwa masuala yote ya kiusalama pamoja na kiafya baada ya kuwa wenzetu wamefikia hatua ambayo wanaweza wakatoa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia, nimeona wameunga mkono Azimio hili. Nami niendelee kusitiza kwamba Azimio hili ni zuri, lina faida nyngi. Mambo mengi yalikuwa yakifanyika bila kuwa na misingi hii ambayo itakuwa imewekwa na Azimio na baadaye ambayo itapelekea uwepo wa sheria, kanuni na taratibu za kuweza kuyashughulikia mambo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nilisema wakati wa kutoa hoja; na kama ambavyo wachangiaji wameelezea nikitoa na pongezi kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje aliyetoka kusema hivi punde, yatatusaidia katika kushughulikia masuala yaliyo ya kimipaka lakini na yaliyo ya kiujirani mwema hasa yanayohusiana na

masuala ya kiusalama wa watu wetu pamoja na mali zao wa nchi hizi mbili na wageni wanaokuja katika nchi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, itatusaidia hata kwenye maisha ya kila siku, masuala haya ambayo tumeyasemea yanayohusu mambo ya migogoro, shughuli za kiuchumi zinazoingiliana katika mipaka yetu. Kwa mfano, watu wetu wanaokaa jirani na mipaka amba wana shughuli zinazoendana na zinazoingiliana, wao kwa asili zao hawatambui mipaka. Tunaamini uwepo wa Azimio na taratibu za kubadilishana taarifa na kubadilishana uzoefu wa kushughulikia uhalifu, itawasaidia watu wetu waweze kufanya shughuli hizo kwa njia ambayo ni salama na endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kutimiza matakwa ya mikataba ambayo nchi yetu imeingia, nchi yetu ni nchi kiongozi katika uanzilishi wa jumuiya hii na katika uendeshaji wa jumuiya hii. Kwa hiyo, yale ambayo yanakubaliwa kama nchi wanachama ni wajibu wetu pia kama nchi kuweza kutekeleza na kuridhia na hasa baada ya kuwa tumeshajiridhisha na manufaa ambayo nchi yetu itapata kupitia jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huku tukipokea hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liridhie Azimio lake la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Community Protocol on Peace and Security*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofî)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja illiamulia na Kuafikiwa)*

(Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki lilitiridhiwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono. Kwa hiyo, Azimio la kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki limeshakubaliwa na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya na nawapongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa hoja zao ambazo walizileta mbele ya Bunge ambazo Bunge limeridhia. Nachukua fursa hii kuwapongeza kwa sababu ni mara chache ambapo hoja zinaletwa na zinaungwa mkono na pande zote za Wabunge waliowakilishwa humu Bungeni. Kwa hiyo, nawapongeza sana.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na pongezi hizo, nalazimika kuwakumbusha masharti ya Kanuni ya 154 na sitaisoma kwa sababu ni ndefu kidogo, lakini kanuni hii tumejiwekea kwa ajili ya kuangalia namna bora ya kutoa salamu za pongezi na pole. Kwa sababu kesho Bunge litaendelea, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kufuata masharti ya Kanuni ya 154. Spika kesho kama nilivyosema kwamba atazungumza kuhusu mambo haya, lakini Bunge litakapoendelea basi tuzingatie masharti hayo.

Kwa upande wa Bunge, Mheshimiwa Spika akitoa pole ama pongezi, anakuwa amesema kwa niaba ya Wabunge wote; na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, akisema pole ama pongezi, anakuwa ametoa kwa niaba ya Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya leo. Kwa mujibu wa Kanuni ya 28(4) naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya kesho Ijumaa, tarehe 8 saa tatu asubuhi.

(Saa 12.15 Jioni Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 8 Septemba, 2017, Saa Tatu Asubuhi)